Nipashe
Ijumaa Machi 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579872
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Mwanafunzi darasa la saba ajinyonga hadi kufa

UKURASA 2


UCHUMI
BUFE
Rais Akufo: Tabianchi inakaribisha njaa Afrika
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Changamoto ya ualbino imemnoa kufikia ujasiriamali uliokamilika
UCHUMI
BIASHARA KATIKA PICHA
KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19
Takwimu za Uchumi Ukurasa 20

UKURASA 13

# Wahamiaji haramu mbaroni mikopo ya elimu

UKURASA 2


Joyce Ndalichako
Abdulrazaq Badru

## Kiwanda kikubwa cha mbolea kujengwa TZ

**NI** uwekezaji kutoka Ujerumani, chatokana na matunda ya mazungumzo ya JPM na Kansela Merkel, mamia ya ajira kumwagwa... *Endelea ukurasa wa 2*



## Ripoti kuamua hatima Lugumi

UKURASA 3

MICHEZO **AUSSEMS: MAPAMBANO YANAENDELEA** UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Wahamiaji haramu wadaiwa kulamba mkopo elimu ya juu

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

IDARA ya Uhamiaji mkoani Kagera inakusudia kuwafikisha mahakamani watu watano akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Rwagati katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Joseph Kinyonyi, kwa tuhuma za kushirikiana na wahamiaji haramu na kuwawezesha wanafunzi wawili wa vyuo vikuu kupata vyeti vya kuzaliwa na kutumia fedha ambazo ni haki ya Watanzania kinyume cha sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Kagera, Pendo Buteng'e, alisema watakaofikishwa mahakamani mbali na mwenyekiti wa kijiji ni Beatrice Rweyemamu na Frida Kagemlo, ambao walijaza vyeti vya kuzaliwa vya wahamiaji hao kama mama mzazi, pamoja na wanafunzi hao Tumaini Francis anayesoma Chuo Kikuu cha Dare es Salaam na Peace Francis anayesoma Chuo Kikuu cha Mwenge, Moshi.

Buteng'e alisema baada ya uchunguzi walibaini kuwa wanafunzi hao wawili wote ni raia wa Rwanda na kuwa Bukoba kuna mama yao anayeitwa Marie Msabima, anayeishi kwa kibali na anafanya kazi katika Taasisi ya Bethania Christian Aid Foundation iliyoko Kemondo Bukoba Vijijini.

"Tulipochunguza tulibaini wanachuo wote wawili ni ndugu na sio raia wa Tanzania ni raia wa Rwanda, lakini walizaliwa Tanzania na wazazi ambao ni wa Rwanda, wamesoma kuanzia elimu ya msingi, sekondari na sasa vyuo vikuu hapa

INAENDELEA UK 8



Rais John Magufuli, akimkabidhi zawadi ya picha ya Mlima Kilimanjaro mgeni wake Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Qatar, Sheikh Mohammed bin Abdulrahman al Than, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Kiwanda kikubwa cha mbolea kujengwa nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel, juzi amezungumza kwa njia ya simu na Rais Dk. John Magufuli na kumhakikishia kuwa Ujerumani ipo tayari kukuza zaidi uhusiano wake na Tanzania hususani kusaidia juhudi za kuimarisha uchumi.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, ilisema Markel amempongeza Rais Magufuli kwa juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwamo kupambana na rushwa na kuimarisha miundombinu. Kufuatia mafanikio hayo Markel amesema Ujerumani itawaleta wafanyabiashara watakaowekeza katika maeneo mbalimbali ya kuimarisha uchumi ikiwamo kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea, ambacho kitakuwa kikubwa kuliko vyote barani Afrika.

Merkel alisema Ujerumani imedhamiria kuunga mkono juhudi za ujenzi wa viwanda nchini Tanzania na kwamba ana matumaini kuwa kiwanda kikubwa cha mbolea kitakachojengwa nchini kitasaidia kuongeza kipato cha wananchi na kuimarisha kilimo na nchi nyingine za Afrika.

Alitoa wito wa kuimarishwa kwa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) na kumwalika kwa mara ya pili Rais Magufuli kutembelea Ujerumani, ziara ambayo itatanguliwa na ziara ya mawaziri wa Tanzania kukutana na mawaziri wa Ujerumani.

Kwa upande wake Rais Magufuli alimshukuru Merkel kwa kumpigia simu na kueleza dhamira yake ya kukuza zaidi uhusiano wa Tanzania na Ujerumani na kubainisha kuwa Tanzania itahakikisha inajenga mazingira mazuri katika maeneo yote ya ushirikiano yakiwamo ya biashara na uwekezaji.

Rais Magufuli alimpongeza Markel kwa uongozi wake wa zaidi ya miaka 13 akiwa Kansela wa Ujerumani na amemhakikishia kuwa Tanzania itadumisha na kukuza zaidi ushirikiano huo kwa manufaa ya pande zote mbili.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

March 21, 2019,

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya jumapili **Tarehe 22/03/2019** kampuni ya EFFCO SOLUTION LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MWANZA USAGALA** kuelekea NGAKA COAL MINING, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T339DEC/T634DCV**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.5 |
| Upana | - | mita | 3.50 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika: **DODOMA hadi NGAKA COAL MINING Kupitia MIKUMI**, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215130302

# Mwanafunzi la saba ajinyonga hadi kufa

**Na Gurian Adolf, KATAVI**

MWANAFUNZI wa darasa la saba Shule ya Msingi Ifukutwa, mkoani Katavi, Ephraim Kijungu (15), amejinyonga hadi kufa kwa kutumia fulana yake kwa madai ya kuchoshwa na manyanyaso.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa tatu asubuhi jirani na nyumba aliyokuwa wakiishi pamoja na kaka yake ambaye ndiye alikuwa mlezi wa mtoto huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Damas Nyanda, alithibitisha kutokea kwa kifo cha mwanafunzi huyo.

Alisema mwanafunzi huyo alikuwa akiishi kwa kaka yake, Edgar lskini na kaka huyo alikuwa akiishi kwenye mashamba yake na kumwacha mdogo wake nyumbani wakiwa na shemeji yake.

Alisema kabla ya tukio la kujinyonga alikuwa akiwaambia wanafunzi wenzake pamoja na majirani kuwa ipo siku atajinyonga kutokana na mateso anayoyapata hapo nyumbani kwao baada ya kuona hakuna sababu ya kuendelea kuishi na bora afe ili akapumzike.

Miongoni mwa mateso aliyokuwa akiyalalamikia ilikuwa ni kitendo cha kujihangaikia ili apate huduma za msingi pamoja ya kuwa ni mwanafunzi kwa kufanya vibarua.

Aidha, ilidaiwa alikuwa akipata vipigo vya mara kwa mara kutoka kwa walezi wake bila ya kufanya kosa lolote.

Kamanda Nyanda alisema siku ya tukio mwanafunzi huyo alikuwa amelala chumbani kwake ndipo usiku aliamka na kutoka nje bila kaka yake na shemeji yake kujua.

Alisema kulipokucha waliamka na kuendelea na shughuli zao na hakukuwa na shaka yoyote ya juu ya mwanafunzi huyo mpaka ilipotimia majira ya saa tatu asubuhi, majirani walipouona mwili wa marehemu huyo ukiwa unaning'inia juu ya mti wa mwembe jirani kidogo na nyumbani kwao.

Majirani hao walitoa taarifa polisi na kufika eneo hilo na kuukuta mwili wa marehemu ukiwa unaning'inia baada ya kujinyonga kwa kutumia fulana yake.

Nyanda alisema mwili wa marehemu ulichukuliwa na kupelekwa katika chumba cha kuhifadhi maiti katika hospitali teule ya Mkoa wa Katavi na baada ya kufanyika kwa uchunguzi wa kitabibu mwili huo ulikabidhiwa kwa ndugu zake.

Mpaka sasa hakuna mtu au watu waliokamatwa kuhusiana na tukio hilo na polisi bado wanaendelea na uchunguzi wa kifo hicho.

# Ripoti kuamua hatima ya Lugumi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amesema wakati wowote kuanzia sasa mmiliki wa Kampuni ya Lugumi, Said Lugumi, atawasilisha wizarani ripoti ya maendeleo ya kazi aliyoagizwa aikamilishe.

Kampuni hiyo ilikuwa inatekeleza mradi wenye thamani ya Sh. bilioni 37 wa kusimika mfumo wa utambuzi wa alama za vidole kwenye vituo vya polisi nchi nzima baada ya kushinda zabuni miaka minane iliyopita.

Miezi saba iliyopita, Lugola alimpa miezi minne mfanyabiashara huyo kuikamilisha kazi hiyo vinginevyo atampeleka Mahakama ya Mafisadi.

Alipoulizwa na Nipashe jana kuhusu utekelezaji wa agizo hilo, Lugola alidai amezungumza na Lugumi na amemweleza kuwa anaandaa ripoti ya maendeleo ya kazi hiyo.

"(Lugumi) amesema anaandaa ripoti ya maendeleo ya kazi ambayo alipatiwa aifanye, tunaisubiri, wakati wowote kuanzia sasa ataiwasilisha kwetu," Lugola alidai.

Julai 31, mwaka jana, waziri huyo alitoa miezi minne kwa Lugumi aliyejisalimisha ofisini kwake siku hiyo, kuhakikisha kampuni yake inakamilisha kazi iliyopewa na serikali.

Lugumi alijisalimisha ofisini kwa waziri baada ya kuagizwa ripoti siku hiyo.

"Tumekubaliana na Lugumi ndani ya miezi minne kuanzia sasa awe amekamilisha kazi aliyopewa ya kufunga mashine hizi na kama atashindwa ndani ya kipindi hicho, ajue Mahakama ya Mafisadi (Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu) inamsubiri," Lugola alidai siku hiyo.

Aprili 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ikipitia utekelezaji wa mapendekezo yake ya miaka ya nyuma, ilibaini kampuni hiyo ilikuwa haijatekeleza kikamilifu mradi huo.

Kutokana na changamoto hiyo, kamati hiyo iliwataka kufika mbele yake watendaji wakuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi kujieleza kwa kuwa Kampuni ya Lugumi ilikuwa imelipwa zaidi ya asilimia 90 ya fedha za mradi huo, huku yenyewe ikiwa haijafika hata asilimia 30 ya utekelezaji wake.

PAC baadaye iliamua kuunda kamati ndogo iliyoongozwa na Japhet Hasunga (sasa Waziri wa Kilimo), kufuatilia utekelezaji wa mradi huo baada ya maelezo ya

INAENDELEA UK. 8

# Simu milioni 1.7 zafungwa

**Na Beatrice Shayo**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) imezifunga simu 1,682,667 zilizokuwa zikitumika katika mitandao mbalimbali kutokana na kuripotiwa kuibwa na nyingine kubainika kutokuwa na viwango vinavyotakiwa.

Mwenyekiti wa Bodi ya TCRA, Dk. Jones Kilimbe, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana, alipotoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu na Mfumo wa Kuratibu na Kusimamia Mawasiliano ya Simu (TTMS).

"Idadi hii inajumuisha simu zilizobainika kutokufikia viwango vinavyotakiwa, simu zilizonakiliwa namba tambulishi na zile zilizoripotiwa kuibwa au kupotea," Kilimbe alisema.

Aliongeza kuwa mfumo huo pia umesaidia upatikanaji wa takwimu za mawasiliano ya simu za ndani yaliyofanyika baina ya watoa huduma za mawasiliano ya simu pamoja na simu za kimataifa zinazoingia na kutoka nchini kwa mujibu wa kanuni za mawasiliano.

Alisema wamebaini mawasiliano ya simu za kimataifa zinazoingia kwa njia za ulaghai (illegal routes) na kwamba sasa yamepungua kutoka asilimia 65 mwaka 2013 hadi kufikia chini ya asilimia 10 mwaka 2018.

"Bila mfumo huu, tulikuwa tunapigwa sana, asilimia 65 ya simu zote zilizofanyiwa majaribio zilikuwa zinapitia njia za panya, sasa zipo chini ya asilimia 10," Dk. Kilimbe alisema.

Alidai kuwa hakuna ulaghai kwa simu za ndani kwa kuwa watoa huduma wana mifumo thabiti kusimamia mitandao yao.

Alisema kukua kwa teknolojia ya mawasiliano pamoja na kuongezeka kwa simu zenye uwezo mkubwa, kumeongeza matumizi ya mitandao ya kijamii ikiwamo Skype, Google Voice, Viber, Talktone, WhatsApp na Facebook.

"Kuongezeka kwa matumizi hayo tatizo lake ni kwamba tuliwajulisha tunapata mapato kutokana na simu zinazopigwa, waheshimiwa mnavyosafiri kwenda hata nchini Kenya, mnapiga simu kwa WhatsApp hampigi moja kwa moja ili tupate hela, maana yake mnatukosesha mapato," Dk. Kilimbe alisema.

Mwenyekiti wa PAC, Nagenjwa Kaboyoka, alisema kamati yake iliona kuna haja ya kutembelea TCRA na kukagua mfumo huo ili ujue unavyofanya kazi na uwazi wake.

Alisema kuwa awali kulikuwa na malalamiko kwamba fedha zinapotea, hivyo walitaka kuona kama mfumo huo wa TTMS umesaidia kudhibiti mianya iliyokuwa inapoteza fedha.

"Kamati yangu imejiridhisha na hata maswali mengine yamejibiwa kwa ufasaha, tumeona jinsi mfumo unavyofanya kazi na data zote tumeziona jinsi simu zote zinazopigwa zinanaswa na fedha zilizotolewa, hivyo serikali inaweza kujipatia mapato kwa uhakika na hakutakuwa na wizi kwa simu za nje ya nchi," alisema.


## BEST GROUP (T) LIMITED

Debt collection, Auctioneer, Commission Agent, Court Broker & Legal Consultant

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC (ACB)** Tutauza kwa **MNADA WA HADHARA** dhamana za mikopo ya wadaiwa ambazo ni **NYUMBA NA VIWANJA,** Mnada utafanyika saa **4:00 asubuhi** mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA/ MAHALI ILIPO | TAREHE | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ama Abdallah Kipende | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano kisarawe mkoa wa pwani | 03/04/2019 | Ukonga |
| 2 | Mariam Castory Ngolo | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya sangara kata ya Chanika | 03/04/2019 | Ukonga |
| 3 | Tandi Sam Sikalangwe | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Pugu Bombani | 03/04/2019 | Ukonga |
| 5 | Happy Zebadia Mbilinyi | Vifaa vya Dukani,Nguo,viatu,Sandles,Mikoba ya kike vyote vipo ofisini Best Group | 03/04/2019 | Ubungo |
| 5 | Abdallah Seif Matimbwa | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Viwege Majohe | 05/04/2019 | Ukonga |
| 6 | Innocent Andrew Uggi | Kiwanja chenye hati ya mauziano kilichopo maeneo ya Magole | 05/04/2019 | Ukonga |
| 7 | Jamila Kondo Gema | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye leseni ya makazi Na.ILA/KPW/KPN20/57 Mtaa Kipunguni Kata Kipawa | 05/04/2019 | Ukonga |
| 8 | Khamis Haji Faki | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja Na.473, Kitalu "N" Pugu Mwakanga | 05/04/2019 | Aggrey |
| 9 | Paschali Gabriely Masesa | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Mbezi Guluguruni | 06/04/2019 | Ukonga |
| 10 | Christina Dominick Simba | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Mbezi Luis | 06/04/2019 | Ukonga |
| 11 | Nassoro Ally Nassoro | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye leseni ya makazi Na KND/MBB/KNN6/63 Mtaa Kanuni Kata ya Mabibo (mdhamini (Amisa Ally Chaurembo) | 06/04/2019 | Ukonga |
| 12 | Nkonda house of food | Nyumba yenye hati ya mauziano iliyopo Tabata Kimanga Manispaa ya Ilala | 09/04/2019 | Ubungo |
| 13 | Selemani Hemed Selemani | Nyumba iliyopo Mbagala Kibonde Maji Hati ya Mauziano | 09/04/2019 | Aggrey |
| 14 | Omari Saidi Mbwirani (Mdhamini Latifa Zuberi Masukira) | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye Leseni ya Makazi Na.TMK/CHB/NZA19/15 iliyopo kwa jina la LATIFA ZUBERI MASUKIRA iliyopo maeneo ya Sanza A Kata ya Charambe | 09/04/2019 | Ukonga |
| 15 | ABUKA CO. LTD (Mdhamini Alilius Butembero Adolph | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja chenye hati ya mauziano maeneo ya Boko Chama | 10/04/2019 | Ukonga |
| 16 | Shabani Jumanne Maganga | Nyumba iliyopo eneo la Vigwaza yenye hati ya mauziano | 12/04/2019 | Ubungo |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/766-309913**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**
**P. O. BOX 699**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 022 2118340-3**

215132802



## KUMBUKUMBU



**APAISARIA ARNOLD KILEWO**
**3/3/1947 - 22/3/2019**

LEO IMETIMIA MIAKA **MIWILI** TANGU ULIOPOTUACHA GHAFLA. UNAKUMBUKWA SANA NA MUME WAKO, WATOTO, KAKA NA DADA ZAKO, WAJUKUU, NDUGU NA MARAFIKI ZAKO.

***NI OMBI LETU ROHO YAKO IENDELEE KUPUMZIKA KWA AMANI HUKO MBINGUNI.***

**"NAJUA YA KUWA WAWEZA KUFANYA MAMBO YOTE, NA YA KUWA MAKUSUDI YAKO HAYAWEZI KUZUILIKA" (AYUBU 42:2).**

615131702



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (kulia), akizungumza na Hodan Addou, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN-Women), pamoja na Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Alvaro Rodriguez (katikati), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# JPM awaalika wawekezaji wa Qatar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alikutana na kufanya mazungumzo na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Qatar, Sheikh Mohammed bin Abdulrahman J.A. Al Thani, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema viongozi hao walizungumzia uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya nchi hizo mbili na dhamira yao ya kuhakikisha unaendelezwa na kukuzwa zaidi hususani katika uwekezaji kwenye gesi, madini, utalii na miundombinu ya barabara, bandari, nishati, reli na huduma za kijamii.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Magufuli alimshukuru Sheikh Mohammed kwa kuja kwake hapa nchini pamoja na ujumbe wa wawekezaji wenye dhamira ya kuwekeza nchini na kumwomba ampelekee salamu za shukrani kwa Mtawala wa Qatar, Sheikh Tamim bin Hamad Al Thani kwa kuendeleza uhusiano na Tanzania.

Rais Magufuli alisema Tanzania ina fursa nyingi za uwekezaji zikiwamo uchakataji wa gesi, madini, utalii na usafiri wa anga, hivyo akamwomba Sheikh Mohammed kuwahamasisha wafanyabiashara wa Qatar kushirikiana na Tanzania kuwekeza katika maeneo hayo.

"Natambua kuwa Qatar mna utaalamu wa kuchakata gesi na sisi tunayo gesi nyingi. Kwa hiyo nawakaribisha mje tushirikiane kuwekeza katika sekta ya gesi. Pia natambua kuwa nyie ni wanunuzi wakubwa wa dhahabu na sisi tunayo dhahabu nyingi na hivi sasa tumeanzisha vituo vya ununuzi wa dhahabu. Nawakaribisha mje mnunue dhahabu na tutawapa ushirikiano wote mtakaouhitaji," alisema Rais Magufuli.

Aidha, taarifa hiyo ilisema Rais Magufuli aliiomba Qatar kushirikiana na serikali ya Tanzania katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo uzalishaji wa nishati ya umeme, ujenzi wa reli, barabara na madaraja na amemwalika Mtawala wa Qatar kufanya ziara Tanzania.

Sheikh Mohammed kwa upande wake, alimshukuru Rais Magufuli na serikali yake kwa kuendelea kushirikiana na Qatar katika masuala mbalimbali na kubainisha kuwa Qatar inathamini uhusiano huo.

## Malawi yapokea tani 200 za mahindi toka Tanzania

**Na Grace Mwakalinga,**

**KARONGA**

MSAADA wa tani 200 za mahindi na 15 za dawa, magodoro na vyandarua ambao umetolewa na Rais Dk. John Magufuli kwa watu walioathirika na mafuriko nchini Malawi umewasili na kukabidhiwa kwa Serikali ya Malawi kwa ajili ya kuwafikishia waathirika wa maafa hayo.

Malori manane yaliyobeba shehena ya tani 200 za mahindi na moja lililosheheni dawa, magodoro na vyandarua yaliwasili wilayani Karonga yakitokea Tanzania. Msaada huo ulikabidhiwa nchini Malawi na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Wiliam Ntinika, ambaye aliiwakilisha Serikali ya Tanzania.

"Tunakabidhi msaada huu ambao umetolewa na Rais Magufuli nchini kwa Rais wa Malawi, Mutharika, tani 200 za mahindi, dawa, magodoro na vyandarua msaada huu tunaihakikishia Serikali ya Tanzania umeufika hapa Malawi ukiwa salama," alisema Ntinika. Msafara huo kuelekea Wilaya ya Karonga, nchini Malawi uliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, ambaye alisema msaada huo ni alama ya upendo na undugu uliopo baina ya Tanzania na Malawi.

Alisema Serikali ya Tanzania ilitoa msaada huo kutokana na kuwapo kwa uhusiano mzuri baina ya wananchi wa Malawi na Tanzania na kusisitiza kuendelea kushirikiana nyakati zote.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Serikali ya Malawi, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Karonga, Raphael Mkisi, aliishukuru Serikali ya Tanzania huku akisema kuwa wilaya 13 kutoka mikoa saba ya Malawi zimeathirika na mafuriko hayo ambayo yamesababisha zaidi ya watu 60 kupoteza maisha.

Mkisi alisema msaada huo mkubwa utasaidia kuziba pengo la uhitaji kwa waathirika wa mafurikio hayo ambayo mbali ya kusababisha vifo pia yameharibu miundombinu ya barabara na majengo nchini humo.


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAM A**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA Mjini
Usimamizi wa mirathi NA.16/2019

Ombi la **YUSUPH MOHAMED**
Msimamizi wa mirathi ya marehemu **MOHAMED YUSUPH**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 28/3/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa

Tarehe 21/03/2019

115132402

**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ**

**DAVID J MWANTIKA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 209 BNW.**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

TAARIFA YA POLIS **MB/TR/RD/304/2019.**

115132202

**KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA**

**TANZANIA FOREST CONSERVATION GROUP** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili T 573 ARY PIKIPIKI HONDA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/03744/2019.**

115131002

**KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA**

**ASIA O. CHAMBEGA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari TOYOTA COASTER yenye namba za usajili **T.278 ABT** Chassis **n.o HB320000666,** Engine no.**12H902515**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi:**TAN/RB/523/2019**

215129702

**KADI YA GARI IMEPOTEA**

**CHARLES BEKONI RUSSEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 334 AHA DAIHATSU TERIOS.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **MS/RB/03742/2019.**

115131302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
**MOROGORO MJINI**


Usimamizi wa mirathi **No;65/2019**

Ombi la **ELNESTINA ROMAN MADAN'GWA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **VICTORY JUMA KIGWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **22/03/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe **21/03/2019.**

215130702

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Emanuel Ledio** anatangaza kupotelewa na vyeti cha kidato channe chenye index namba P.302/74 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1988 katika Kituo cha Arusha Centre, na cheti kingine chenye index namba P.302/73 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1989 katika Kituo cha Arusha Centre.

**Polisi Taarifa: AR/RB/8041/2019**

115129502

**KADI YA GARI IMEPOTEA**

**HIRCON CONSTRUCTION COMPANY LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 835 AQQ FUSO** MITSUBISHI.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **TR/RB/03743/2019.**

115131102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

SUMMER COMMUNICATION CO LTD
S.L.P 211,
NJOMBE

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe **22-03-2019** kampuni ya **SUMMER COMMUNICATION CO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka NJOMBE kuelekea SONGEA, gari hizo zenye namba za usajili: **T 688 CDH / T 102 CWK.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.0 |
| Upana | - | mita | 3.0 |
| Kimo | - | mita | 4.5 |

3. Njia itakayotumika **NJOMBE hadi SONGEA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115131202

## HABARI KITAIFA

# TBS, ZBS watakiwa kudhibiti njia za panya

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, imeishauri Menejimenti ya Shirika la Viwango nchini (TBS), kushirikiana na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), ili kudhibiti njia zote za panya zinatotumika kuingiza bidhaa zisizo na ubora.

Wajumbe wa kamati hiyo walitoa ushauri huo juzi, jijini Dar es Salaam, walipotembelea shirika hilo kujionea shughuli mbalimbali za udhibiti wa ubora zinazofanywa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Murad Murad, alisema TBS lazima isimamie mipaka ya Tanzania kuhakikisha hakuna bidhaa hafifu zinazoingia na kusababisha madhara kwa watu.

"Tunataka kuwe na usimamizi na ukaguzi wa uhakika katika mipaka na bandari zote na hata kwenye njia za panya kwa sababu kuwapo kwa bidhaa zisizokuwa na viwango kwenye soko kunawafanya mwonekane hamfanyi kazi wakati mna mitambo ya kisasa," alisema Murad.

Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, alilitaka shirika hilo kutayarisha viwango vya madini kwa kuwa sasa hakuna viwango vya aina hiyo hapa nchini.

Kuhusu uhaba wa wafanyakazi wa shirika hilo, Waziri Kakunda aliahidi kuhakikisha linakuwa na wafanyakazi wa kutosha ili kusaidia kukabiliana na tatizo la bidhaa zisizokuwa na viwango nchini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, shirika hilo lina wafanyakazi 470, na kwa sasa linahitaji nyongeza ya wafanyakazi 280 ili kufikisha idadi ya watumishi 750.

Waziri Kakunda alikiri kuwa shirika linahitaji wafanyakazi 750 ambao hata hivyo alisema bado ni wachache kulinganisha na majukumu ya kila siku ya shirika hilo.

Alisema kwa sasa kuna vitu vingi vinahitajika kufanywa na serikali ikiwa ni pamoja na kurasimisha bandari bubu 21 kuwa bandari halali hatua ambayo itasababisha hitaji la wafanyakazi wengine.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Ngenya, alisema shirika hilo linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ya rasilimali watu, mishahara midogo na watumishi kutopandishwa madaraja tangu mwaka wa fedha 2016/17.

Alisema changamoto nyingine ni ufinyu wa nafasi za maabara na gharama za kununua

vifaa, utayari wa umma na jumuiya ya wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa viwango katika kulinda afya na usalama wa walaji.

Dk. Ngenya alitaja changamoto nyingine kuwa ni wafanyabiashara wasio waaminifu

wanaoingiza bidhaa kwa njia za panya na hivyo kusababisha uingizwaji wa bidhaa zisizo na viwango.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Kamati hiyo, Juma Ntimizi, alishauri elimu ya viwango kwa Watanzania izidi kutiliwa mkazo ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mjumbe mwingine wa kamati hiyo Said Kubenea, alishauri mishahara ya watumishi wa shirika hilo iboreshwe ili kuwaondolea vishawishi vya rushwa watumishi hao.

# Gondwe aagiza vijiji kufanya mikutano kila Ijumaa

**Na Dege Masoli,** HANDENI

MKUU wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe, ametaka mikutano mikuu ya serikali za vijiji kufanyika siku moja wilaya nzima kila Ijumaa ya wiki ya kwanza.

Aidha, ametishia kuwafikisha kwenye Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (Takukuru) viongozi wote wasiofuata miongozo, kanuni na

taratibu za fedha ili kulinda uwajibikaji na matumizi mabaya ya mali za umma.

Gondwe aliyasema hayo wakati wa mkutano wa wadau wa elimu wilayani hapa ambao uliandaliwa na asasi isiyo ya kiserikali ya Tree of Hope ya nchini na kufanyika mjini Handeni kwa ufadhiliwa na Shirika la Foundation for Civil Society.

Alisema suala la serikali za vijiji kutoitisha mikutano mikuu kwa

mujibu wa kalenda limekuwa changamoto kubwa kwa viongozi wengi na kulalamikiwa na wananchi.

Alisema kalenda aliyoitangaza ndiyo itakuwa mwarobaini kwa

viongozi wasiowajibika na kwamba yeye na maofisa wake watafanya ziara za kushtukiza katika vijiji kufuata kalenda hiyo ili kubaini watakaokaidi agizo hilo.

Kwa upande wa miongozo ya fedha, Gondwe alisema atawapeleka Takukuru viongozi ambao hawatafuata taratibu, kanuni na sheria za fedha na kwamba lengo ni kulinda uwajibikaji na kutaka kufuta matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Awali Mratibu wa mradi huo wa uhamasisha uwajibikaji wa jamii na mamlaka zinazohusika katika kuboresha huduma za elimu, Goodluck Malilo, kwenye taarifa yake ya robo ya pili ya kuanzia Februari hadi Machi 2019, alisema vijiji vinne vilifanyiwa madodoso na kubaini udhaifu kwa baadhi ya viongozi katika uwajibikaji.

Kwa mujibu wa Malilo, maeneo yaliyofanyiwa madodoso na asasi hiyo ni ya vijiji vya Kwedizinga, Michungwani, Kabuku nje na Komsanga na yalifanyika mazungumzo na wadau mbalimbali na kubaini kasoro hizo.

Alitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni kukosekana uwiano wa ruzuku kwa mwanafunzi wa shule za msingi na baadhi ya walimu kutotambua kiwango halisi cha ruzuku cha kila mwanafunzi na hivyo kushindwa kutoa majibu sahihi yanapotokea malalamiko.

Kasoro nyingine ni kutobandikwa kwenye mbao za matangazo fedha za ruzuku zinazotolewa na serikali katika shule, matumizi ya ruzuku yasiyozingatia miongozo iliyopo, upatikanaji wa fedha usiozingatia uhitaji na matarajio na viongozi wa vijiji kutokuwa na uwazi na uwajibikaji.






Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ihakiki mashtaka kubaini waliobambikwa

**HIVI** karibuni zimethibitika taarifa za kubambikwa mashtaka raia anayeelezwa kuwa hakuwa na hatia huko mkoani Tabora. Suala lake limepata ufumbuzi baada ya kuandika barua na kumwomba Rais John Magufuli, amsaidie.

Rais alitoa maelekezo na kesi ilifuatiliwa ikabainika kuwa hakuwa na hatia ya mashtaka aliyokuwa amefunguliwa mahakamani na sasa ameachiwa huru, japo polisi inadai kuwa inaendelea kumchunguza.

Hatua ya uchunguzi iliyothibitisha kuwa hakuwa na hatia zinaleta maswali mengi, na kubwa ni kwanini watumishi wa watu ambao ni polisi wawasingizie raia mashtaka na kuwafungulia kesi za jinai za kuzusha hadhi zao?

Ndiyo maana tunaona kuwa unahitajika uchunguzi kufahamu kwanini walinzi wa usalama wa raia na mali zao wabambike kesi za kihalifu na jinai raia wasio na hatia. Pengine, ni suala ambalo linahitaji majibu ili hatua zichukuliwe kurekebisha udhaifu huo.

Kwa vile imethibitika kuwa watu wanabambikwa kesi na polisi, tunaona kuwa kuna haja ya kuchunguza washtakiwa walioko mahakamani, wafungwa magerezani ili kuwasaidia. Ni kwanini watu wasio na hatia waendelee kusota mahabusu na magerezani?

Tunaona kuwa ni wakati sasa wa kuangalia mashtaka dhidi ya washtakiwa na wafungwa walioko magerezani.

Tunaishauri serikali kuona namna ya kuzitumia Wizara za Mambo ya Ndani ya Nchi, Sheria na Katiba pamoja na Wizara ya Afya (Idara ya Ustawi wa Jamii), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG) pamoja na wadau wengine inayoona wanaweza kuhusika kuunda timu ya kutembelea magereza yote nchini na kuangalia majalada ya mashtaka yaliyoko mahakamani.

Tunaamini kuwa kunahitajika mawasiliano ya ana kwa ana baina ya mfungwa, mshtakiwa na faili la kesi yake au hukumu yake.

Uhakiki ni muhimu, lakini pia timu iangalie upya utaratibu wa kuwafungulia watu mashtaka na kupendekeza marekebisho ili kuuboresha kama itahitajika.

Haina maana kufungua kesi kubwa ya mauaji ambayo kwa sheria ya Tanzania haina dhamana wakati washtakiwa wamesingiziwa.

Huko ni kuiongezea serikali gharama kubwa za kutunza magerezani nguvu kazi ambayo ilihitajika kuzalisha mali kwa maendeleo ya nchi.

Uchunguzi ufanyike kubaini uhalali wa maelezo ya polisi na magereza wanaposema ushahidi haujakamilika inamaanisha nini? Kwa nini haujakamilika kwa miaka kadhaa?

Mawakili wa serikali wanafuatiliaje wakisikia ushahidi haujakamilika? Kwanini kuendelea kuahirisha kesi kwa sababu ya kusema upelelezi unaendelea?

Inawezekana kigezo hicho kikatumiwa kama njia ya kumkandamiza raia ambaye amefunguliwa mashtaka ya kubambikwa kesi.

Polisi na jamii iangalie athari za kumbambikia mtu kesi ambazo ni kusababishia kumshusha hadhi yake kwenye jamii, kumyumbisha kiuchumi, kumwathiri kisaikolojia, kimwili, kumdhalilisha na kwa ujumla kubadilisha utaratibu mzima wa maisha yake. Inawezekana hata kusababisha wengine kujiua kwa kuona kuwa hawana wa kuwasaidia wala wa kuwatetea.

Ndiyo maana tunaishauri serikali kuwa sasa ni wakati wa kuangalia uhalali wa mashtaka, mtu akifunguliwa kesi ya unyang'anyi, uwapo ushahidi angalau na maelezo ya mwanzo ya walalamikaji, vitu vilivyoibwa na ukweli uonekane kuwa kuna jambo la jinai limetendeka au ni uzushi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Wiki ya Maji ifanyie kazi mabomba kupasuka

Na Salome Kitomari

**KAULIMBIU** ya maadhimisho ya Wiki ya Maji mwaka huu ni: "Hakuna atakayeachwa; kuongeza kazi ya upatikanaji huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa wote katika dunia inayobadilika kitabianchi".

Kuongeza kazi ya upatikanaji huduma ya maji na usafi wa mazingira, inaendana na udhibiti wa maji yanayotiririka ovyo mitaani, ambayo yangewafikia wananchi, ingeongeza idadi ya wanaopata huduma ya majisafi na salama.

Usafi wa mazingira unaendana na kuhakikisha majitaka yanaondoshwa kwa wakati, mifumo ya majitaka inadhibitiwa, kuhakikisha hakuna majitaka yanayotiririka ovyo mitaani na kusababisha magonjwa ya mlipuko au uharibifu mwingine.

Licha ya jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka nchini, bado kuna maeneo yenye changamoto kubwa ya kudhibiti upotevu wa maji, ambayo wakati mwingine haihitaji rasilimali fedha nyingi au muda.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), kila mwezi inatuma madai ya ankara za maji kwa wananchi na baada ya siku kadhaa, inawakumbusha kuhakikisha mhusika analipa deni lake. Ujumbe huo hueleza kiasi cha maji ulichotumia na fedha unazodaiwa kulipa. Baada ya siku kadhaa unakumbushwa, kuwapo operesheni ya kukata maji nyumba kwa nyumba na kumtaka mhusika kulipa ankara kabla ya kukatiwa huduma hiyo.

Utaratibu huo ni mzuri sana kwa kuwa umerahisisha ulipaji wa ankara za maji na unamkumbisha mhusika, kila inapofikia hatua ya kukatiwa huduma, hakuna wa kumlaumu. Kwa ujumla, mamlaka hii na nyingine zinafanya kazi nzuri kwa kuwa, sasa kiwango cha upatikanaji maji jijini Dar es Salaam, hakifananani na miaka iliyopita. Wananchi hawakuwa na huduma hiyo na maji kugeuka kuwa bidhaa adimu na ghali.

Kwa nguvu hiyo ya kudai ankara za maji, nilitarajia uwajibikaji, kwa maana ya kuhakikisha mabomba yanayopoteza maji ovyo yanadhibitiwa, siyo mitaa kuwa na madimbwi ya maji, ambayo yangetumiwa na wananchi, kupitia mabomba.

Jijini Dar es Salaam, ni kawaida kukuta maji yanatiririka ovyo kwa muda mrefu, pasipo udhibiti yatumiwe na watu na mwishowe mamlaka husika zinapata fedha.

Unaweza kupita mitaa ukadhani mvua ilinyesha siku hiyo, lakini kitakachokuonyesha kuwa mvua haikunyesha, ni maeneo mengine hayajalowa, ila kuna madimbwi ya maji katika makazi ya watu, ambayo maji yake yangetumiwa na wahitaji wengine.

Wakati mwingine, cha kushangaza wakati maji yanamwagika wananchi walioko katika mtaa wa pili au wa tatu hawana maji, kwa kuwa yanafunguliwa kwa awamu.

Waswahili wana usemi, hoja kwa vielelezo. Nami nitumie kielelezo. Katika eneo la uwanja ulioko karibu na Kanisa Katoliki Salasala, kuna mahali maji yanatiririka utadhani ni mfereji wa mvua.

Ni muda mrefu hali hiyo imedumu na siyo eneo lililojificha. Lakini, wananchi wanashangazwa kukosekana jitihada za haraka kuzuia upotevu huo wa maji.

Wakati yanatiririka, wananchi wa mitaa kadhaa hawana huduma ya maji kwa takribani wiki mbili, kwa kuwa tu anayepaswa kufungua hajaamua kufungua, jambo linalowafanya watu wajiulize maswali; maji yanaachwa yakimwagika kiasi hicho, maana yake yangedhibitiwa yangewafikia wananchi ambao wangelipa ankara na serikali kupata fedha.

Pia, eneo la Barabara ya Salasala, kuna mahali maji yanavuja kama vile ni mfereji wa maji, lakini kwa muda mrefu hakuna jitihada za kukabiliana na hali hiyo, kuhakikisha maji yanawafikia wananchi walipaji wa ankra.

Eneo la Sinza, nako ni kawaida kuona maji yanamwagika kwenye mitaa mbalimbali, jambo linaowafanya wananchi wajiulize, kazi nzuri ya kuboresha miundombinuna huduma ya maji, inashindwa kufanyika kudhibiti upotevu wake.

Kama kaulimbiu inavyosema, hakuna atakayeachwa katika kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji, basi jitihada zifanyike kudhibiti maji yanayopotea, ambayo yangewafikia wananchi, wangefurahi sana na mamlaka ingepata fedha. Eneo jingine lililopo kwenye kaulimbiu, ni usafi wa mazingira, imekuwa tatizo jingine kubwa la majitaka kusambaa mitaani bila ua udhibiti. Mfano halisi, ni eneo la Mwenge madukani, kuna tatizo la chemba kumwaga majitaka na udhibiti wake unasuasua.

Yapo maeneo mengi yenye matatizo ya aina hiyo, hivyo katika kutekeleza kaulimbiu ya mwaka huu, ni vyema hatua zikachukuliwa kudhibiti upotevu wa maji na majitaka yanayosambaa ovyo mitaani.

## HABARI KITAIFA

# Watanzania 2,000 wasomeshwa India

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA 2,369 wamepatiwa mafunzo nchini India, kwenye maeneo muhimu ya vipaumbele katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Naibu Katibu Mkuu (Sayansi) katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Profesa James Mdoe, alisema hayo katika sherehe za mwaka za "Siku ya ITEC" zilizofanyika Ubalozi wa India nchini, jijini Dar es Salaam, Machi 19.

Mpango wa India wa ushirikiano wa kiufundi na uchumi, una lengo la kutoa mafunzo ya kujenga uwezo na kukuza taaluma kwa watumishi wa umma katika nchi zinazoendelea na ulianzishwa na Serikali ya India tangu mwaka 1964.

Siku ya ITEC huwaleta pamoja watu wote waliohudhuria mafunzo hayo nchini India.

Prof. Mdoe alisema Tanzania ni moja ya wanufaika wakuu wa nafasi nyingi katika mpango huo wa ITEC, kufuatia Watanzania wapatao 2,369 kupatiwa mafunzo nchini humo katika maeneo muhimu ya vipaumbele, ndani ya kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Prof. Mdoe pia akiongelea kituo bora cha Tehama cha ushirikiano baina ya India na Tanzania (India-Tanzania Centres of Excellence in ICT) kilichopo Taasisi ya Teknolojia, Dar es Salaam (DIT) na kile cha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (Nelson Mandela African Institute of Science & Technology) kilichopo Arusha, alisema kimetoa msaada wa vitabu 131,000 kwa ajili ya shule za sekondari kwa masomo ya Hisabati na Sayansi, pamoja na msaada wa dawa wenye thamani ya shilingi bilioni mbili ambao umetolewa na Serikali ya India kwa Serikali ya Tanzania.

"Msaada wa mashine ya tiba ya maradhi ya saratani (Bhabhatron) ni ya kisasa pamoja na mashine ya mionzi, ambazo zote zimetengenezwa nchini India," alisema.

Alisema mashine hizi zipo katika Hospitali ya Bugando, Mwanza ikiwa ni msaada uliotolewa na Serikali ya India. Prof. Mdoe aliishukuru serikali na Ubalozi wa India kwa msaada huo.

Naye Balozi wa India nchini Tanzania, Sandeep Arya, alisema mpango wa ITEC upo maeneo mbalimbali ya ushirikiano baina ya India na Tanzania ikiwamo juhudi mpya za uanzishaji wa e-ITEC, mkazo katika maeneo yenye maslahi kwa Tanzania kama huduma za afya, kilimo, ujasiriamali, miundombinu, miradi muhimu ya maji ambayo Serikali ya India imetoa mkopo nafuu, mapendekezo ya e-VBAB mpango wa elimu kwa njia ya mawasiliano (tele-education programme) katika vyuo vikuu vitano na mpango wa tiba kwa njia ya mawasiliano (tele-medicine programme) katika hospitali tano nchini.

# Kigogo atumbuliwa kwa kuuza shamba

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemsimamisha kazi Ofisa Ardhi wa Kanda ya Kaskazini Mashariki, Thadeus Riziki, baada ya kuuza shamba la Amboni Estate lililoko jijini Tanga kinyume na utaratibu.

Waziri Lukuvi amechukua hatua jana, wakati wa mkutano wa hadhara uliokuwa na lengo la kusikiliza kero za wananchi na kutatua migogoro ya ardhi kwa wakazi wa Jiji la Tanga uliofanyika katika viwanja vya Tangamano.

Alisema kuwa ofisa huyo wa ardhi, wakati akiwa na cheo cha ofisa ardhi wa Jiji la Tanga aliuza shamba la Amboni kwa mwekezaji ilhali sheria ilielekeza shamba hilo liwekwe katika utaratibu wa kufutiwa hati na Rais.

"Nimeamua kumsimamisha kazi ofisa huyo ambaye nasikia hivi juzi, amependishwa na kuwa ofisa kanda kutokana na kubariki mauziano ya shamba ambalo lilitakiwa kufutwa," alibainisha Waziri Lukuvi.

Aidha, aliiagiza Halmashauri ya Jiji la Tanga kuhakikisha shamba hilo linarudi mikononi mwa serikali kwa ajili ya kuanza taratibu za kulifutia hati.

"Mnapaswa kumfanyia tathmini mwekezaji yule ya mali zisizohamishika ili mjue ametumia ekari ngapi pamoja na wananchi walioko muwafanyie uthamini kwa gharama zenu bila ya kuwa na ubaguzi kwa kuwa haya makosa mliyafanya wenyewe," alisema.

Pia aliwataka watendaji wa jiji hilo kuhakikisha wanasimamia sheria na taratibu za ardhi kama zinavyoelekeza badala ya kuendelea kufanya kazi kwa malalamiko bila ya kuchukua hatua.

"Tanga mna maeneo mengi ya mashamba ambayo yameshindwa kuendelezwa, lakini sijui kwanini mmekuwa wagumu kufuta mashamba hayo ili Rais Magufuli aweze kuridhia na kuyagawa kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za maendeleo," Lukuvi alisema.

Aidha, katika kusikiliza kero za migogoro ya ardhi ilionyesha kesi nyingi zinatokana na wananchi wengi kuchukua fidia ilhali wakiwa hawajui thamani ya maeneo yao.

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, aliwataka wakazi wa Jiji la Tanga kuwasilisha kero zao za ardhi kwa waziri huyo kwa kuwa yupo kwa ajili ya kuhakikisha anatatua migogoro iliyopo.

"Kama mnavyojua Serikali ya Rais Magufuli ni ya hapa kazi tuu, hivyo niwaombe wananchi elezeni kero zile ambazo ni za ukweli ili waziri aweze kuzifanyia kazi kwa haraka," alibainisha DC Mwilapwa.


**MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA**

TFDA
Tanzania Food & Drugs Authority

## TAARIFA KWA UMMA

**21 Machi, 2019**

### UFAFANUZI JUU YA TAARIFA ILIYOTOLEWA KWENYE GAZETI LA TANZANITE

1. Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inapenda kutoa ufafanuzi juu ya taarifa iliyotolewa kwenye gazeti la Tanzanite, Toleo Na. 392 la Alhamisi tarehe 21 Machi, 2019 iliyokuwa na kichwa cha habari "TRA, TBS TFDA Zijitathmini".

2. TFDA imepitia kwa kina taarifa hiyo na imebaini haina ukweli.

3. Mwandishi aliyeandika taarifa hii hajafanya uchunguzi wa kutosha ili kuweza kufahamu vizuri taratibu za kazi na jinsi udhibiti unavyofanyika kwenye mipaka aliyoinukuu.

4. TFDA imeweka mfumo mzuri wa udhibiti wa bidhaa za dawa, vyakula, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi vinavyopita kwenye vituo vya forodha.

5. Mfanyabiashara yeyote anayetaka kuingiza bidhaa tajwa nchini anatakiwa kwanza asajili bidhaa yake na kisha aombe kibali cha kuingiza bidhaa (Import permit) kabla ya kuleta mzigo.

6. Vibali hutolewa ndani ya masaa 24 kwa bidhaa zilizosajiliwa kupitia mfumo wa kielektroniki (Online application system). Baada ya hatua hii, shehena za mizigo zinazoingia nchini hukaguliwa na Wakaguzi walioko kwenye vituo vya forodha kabla ya kuruhusiwa.

7. Bidhaa ambazo hazikidhi vigezo zinapokutwa kwenye vituo vya forodha huzuiliwa kuingia nchini, huteketezwa au kurudishwa zilipotoka.

8. Mwandishi wa gazeti tajwa hajaainisha ni aina gani ya nyaraka ya bidhaa zilizoghushiwa au kuwa na takwimu zozote kuthibitisha kilichoandikwa. Taarifa hiyo imekuwa ya kiujumla jumla bila kuwa na uthibitisho wowote.

9. Ikumbukwe kuwa TFDA ni taasisi yenye ithibati ya ISO 9001: 2015, Maabara yake ina ISO/IEC 17025: 2015 na taasisi ya kwanza barani Afrika kuthibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa na mifumo bora na thabiti ya udhibiti wa dawa (Maturity Level 3).

10. Ni vyema waandishi wakajenga utamaduni wa kufika TFDA ili kupata taarifa vizuri badala ya kuandika taarifa zisizo na uthibitisho na kuchanganya umma.

**Imetolewa na:**

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),**
**Makao Makuu,**
**Mtaa wa Mwanza, Block T,**
**Kiwanja Na. 6, S.L.P 1253,**
**DODOMA, Tanzania.**

**Simu ya mezani: +255 26 2320156**
**Simu za kiganjani:+255 658 445222/+255 685 701735**
**Simu ya bure (Toll free): 0800110084**
**Barua pepe: info@tfda.go.tz**
**Tovuti: www.tfda.go.tz**

215133202

# Wahamiaji haramu wadaiwa kulamba mkopo elimu ya juu

INATOKA UK 2

nchini, walipata vyeti vya kuzaliwa kwa kutoa taarifa za udanganyifu," alisema na kuongeza:

"Katika cheti cha kuzaliwa cha Tumaini majina ya mama yake yanasomeka Beatrice Rweyemamu na Peace majina ya mama yake yanasomeka Frida Kagemlo, na baada ya kupata vyeti vya kuzaliwa walivitumia kuomba mkopo wa elimu ya juu na kupewa wakati hiyo ni haki ya Watanzania," alisema.

Alisema kuwa taarifa za maombi ya mkopo zilithibitishwa na mwenyekiti huyo wa kijiji wakati akijua kuwa taarifa zilizotolewa na wahusika ni za uongo.

Butenge alisema wanakamilisha taratibu ili waweze kuwafikisha mahakamani watu hao watano.

Akijibu tuhuma hizo Mwenyekiti wa Kijiji Kinyonyi, alisema kuwa wakati akiwasainia fomu hakufahamu kama sio raia kwa kuwa aliwaona katika kituo cha kulelea watoto wa mitaani cha Bethania na kudhani wamelelewa hapo kama wanavyolelewa watoto wengine yatima na wa mitaani.

Aidha, wanafunzi hao Peace na Tumaini wanaotuhumiwa kuwa ni wahamiaji haramu, walisema kuwa hawakufahamu kama hawastahili kupata haki hiyo maana walizaliwa na kusomea Tanzania.



Takataka zikiwa zimetelekezwa bila ya kuzolewa katika Barabara ya Tandale Sokoni, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho kinaweza kusababisha magonjwa na milipuko kama vile kipindupindu. **PICHA: JOHN BADI**

# Tetemeko lazua taharuki Mbeya

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

TETEMEKO la Ardhi lililodumu kwa muda wa sekunde 30 katika baadhi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, limesababisha madhara jijini Mbeya kwa kubomoa nyumba nne na baadhi ya familia kukosa makazi.

Tukio hilo lilitokea ghafla jana saa 6:04 mchana na kusababisha taharuki miongoni mwa wananchi, huku baadhi wakitelekeza biashara zao na kutimua mbio na wengine wakikimbia ofisi zao kujiokoa.

Tetemeko hilo lilitokea wakati viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Mbeya walipokuwa kwenye sherehe za maadhimisho ya Siku ya Elimu ya Mkoa huo na kusababisha baadhi ya washiriki kuingiwa na hofu.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwaambia washiriki wa sherehe hizo kuwa vyombo vya usalama vimewahakikishia kuwa kilichotokea ni tetemeko na hivyo hawatakiwi kuwa na hofu.

Baada ya kupata taarifa za nyumba za watu kubomoka, Nipashe ilifika maeneo ya Ilemi na Isanga na kushuhudia nyumba nne za maeneo ya Isanga na Ilemi zikiwa zimeanguka, huku waathirika wakiendelea na jitihada za kurudisha nyumba zao kwenye hali ya kawaida. Mmoja wa waathirika hao, Rashid John, mkazi wa Kata ya Isanga eneo la Igodima A, alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa sita akiwa na binti yake ndani anamwandalia mwanawe chakula na ghafla aliona nyumba ikitikisika na kishindo kikitokea ardhini.

Alisema hakuelewa tatizo, lakini alivyoona upande wa nyumba umeanza kuanguka akambeba mwanawe na kukimbilia nje ili kujinusuru. Alisema ataendelea kuishi kwenye nyumba yake ili kulinda mali zake na kwamba anafanya jitihada za kutafuta pesa ili kujenga ukuta wa nyumba.

# Ripoti kuamua hatima ya Lugumi

INATOKA UK 3

watendaji wakuu wa wizara na Jeshi la Polisi mbele ya kamati kutoridhisha.

Hata hivyo, ripoti ya kamati ndogo ya PAC haikusomwa bungeni, lakini Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema moja ya mapendekezo ya kamati hiyo ni serikali kuhakikisha mradi huo unatekelezwa ili kuokoa mabilioni ya shilingi yaliyolipwa kwa Kampuni ya Lugumi.

Julai Mosi, mwaka jana, Rais John Magufuli alitengua uteuzi wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Dk. Mwigulu Nchemba na wakati akimwapisha Lugola kushika nafasi hiyo, alieleza kuwa moja ya mambo yaliyochangia kutumbuliwa kwa mtangulizi wake wizarani hapo ni kutochukua hatua dhidi ya Lugumi.

Siku chache baada ya kuapishwa, Lugola alimtaka Lugumi kufika ofisini kwake kujieleza na baadaye akampa miezi minne mfanyabiashara huyo kukamilisha kazi aliyopewa na serikali, vingine atafikishwa katika Mahakama ya Mafisadi.

Akitangaza uamuzi huo mbele ya waandishi wa habari Julai 31, mwaka jana, Lugola alisema Rais Magufuli ameanzisha mahakama hiyo kwa ajili ya mafisadi na tangu ianzishwa bado ina uhaba wa wateja.

Alisema endapo Lugumi atashindwa kutekeleza kazi aliyopewa, afahamu wazi atakuwa mteja wa mahakama hiyo.

"Katika mkataba huu, serikali ilishatoa fedha, hivyo kinachohitajika ni kufungwa mashine au fedha kurejeshwa. Yeye (Lugumi) amechagua kufunga mashine, ndiyo maana tumempa huu muda ili akamilishe kazi," Lugola alisema.

Siku 10 kabla ya Lugumi hajajisalimisha ofisini kwa Lugola, waziri huyo alitangaza mbele ya waandishi wa habari kuwa alikuwa amempa siku 11 Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, kumsaka Lugumi na kumfikisha ofisini kwake kutokana na sakata la mkataba tata kati ya kampuni yake ya Lugumi Interprises Limited na Jeshi la Polisi.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ilibaini kuwa licha ya kulipwa asilimia 90 ya fedha za utekelezaji wa mradi huo, kampuni hiyo ilifunga mashine za kielektroniki 14 kati ya 106 za kuchukua alama za vidole katika vituo vya polisi 14 kati 106.


P.O BOX 3072, TEL. NO: 0717-425708, 0687-461667, 0717-616227

**MARUDIO YA MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **UCHUMI COMMERCIAL BANK LIMITED,** Tutauza kwa mnada wa hadhara,dhamana/mali za wadaiwa walioshindwa kurejesha mkopo wa Bank hiyo, Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo kama ifuatavyo:

| NO. | DHAMANA | TAREHE/MUDA |
|---|---|---|
| 1. | KIWANJA NA.1579.KITALU 'F' ENEO LA NJIA PANDA HIMO | 23/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2. | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA.168,KITALU 'A' KARATU MJINI | 24/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | KIWANJA NA.217,KITALU 'T' KARATU MJINI | 24/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA.8 KITALU 'T' HATI NA:37614,KARATU MJINI | 24/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5. | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA.1304 KITALU 'G' WILAYA YA KARATU | 24/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 6. | NYUMBA ILIYOPO KIWANJA NA.5 KITALU 'J' KARATU MJINI | 24/03/2019 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELA |

215133402

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa malipo ya 25% ya fedha taslimu papo hapo baada ya nyundo ya Dalali kutua na salio la 75% liwe limelipwa ndani ya siku 14 tokea siku ya Mnada.
2. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada kurudiwa.
3. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo.
4. Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwenye ofisi zetu za **MOROGORO SABASABA STREET** near Omary Mahita Mosque au tupige simu zilizopo hapo juu au wasiliana na **UCHUMI COMMERCIAL BANK LIMITED MAKAO MAKUU.**


# Maalim Seif, Zitto wapokewa kwa shangwe Z'bar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Maalim Seif Sharif Hamad, amepokewa kwa shangwe na nderemo alipowasili Zanzibar akitokea Tanzania Bara.

Maalim Seif ambaye aliongozana na Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alitangaza kujiunga na chama cha ACT Wazalendo Jumatatu ya wiki hii.

Aliwasili jana jioni kwa boti na kupokewa na umati wa wafuasi wake waliokuwa na shauku na kumuona baada ya kuwasili visiwani hapa.

Alipowasili alipelekwa kwenye ofisi zilizokuwa za CUF ambako nako alipokewa kwa shangwe na nderemo, huku wafuasi wake wakiwa wamevalia sare za ACT- Wazalendo wakiimba nyimbo za kumpongeza.

Baada ya Maalim Seif kujiunga na chama hicho, zilizokuwa ofisi za CUF ikiwamo ile ya Makao Makuu Mtendeni, zilibadilishwa rangi na kupakwa rangi za ACT- Wazalendo.

Licha ya majengo hayo kubadilishwa rangi, pia wafuasi wa Maalim Seif juzi na jana walichoma bendera na sare za CUF.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema chama hicho hakina ugomvi na serikali ila kinapigania haki ya demokrasia.

Alisema mwanasiasa huyo kujiunga na ACT-Wazalendo kutaongeza kasi na ari ya kudai demokrasia na kwamba chama hicho hakina ubaguzi wa rangi, dini wala ukabila, hivyo watu wote wanakaribishwa kujiunga.

Alisema chama hicho kina azima ya kutetea wananchi wanyonge wapate haki zao za kidemokrasia, haki ya kufanya siasa pamoja na haki ya kukosoa pale wanapoona mambo hayaendi sawa.

Zitto alisema chama chake kinataka kuikomboa Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuwa uhuru wa kidemokrasia umeminywa.

Akizungumzia kuhusu Muungano, Zitto alisema wananchi wa pande mbili hizo wanataka muungano sawa unaonufaisha pande zote mbili.

"Ukiwekeza Zanzibar katika viwanda bidhaa zinazozalishwa haziwezi kuuzwa Tanzania Bara, hivyo Muungano huu hautoi fursa sawa, kuna mambo mengi ya kurekebisha hapa," Zitto alisema.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kuungana na chama cha ACT-Wazalendo kwa kuwa nia ya chama hicho ni kuwa na nchi yenye uhuru, maendeleo na umoja wa kitaifa. Pia Zitto alipokea wanachama wapya ambao ni wafuasi wa Maalim Seif na kuwakabidhi kadi za chama hicho.

HABARI KITAIFA

# Waomba elimu kutambua bidhaa hafifu

**Na George Tarimo,** IRINGA

WAFANYABIASHARA mkoani Iringa wameliomba Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu bidhaa zinazofaa kuwapo sokoni na zisizofaa baada ya kufanya msako wa kushtukiza na kukuta bidhaa hafifu zikiwa sokoni.

Mmoja wa wafanyabiashara wa maduka ya bidhaa za vilainishi vya mitambo, Shadrack Innocent, alisema changamoto kubwa inayowakumba ni msako wa kushtukiza na kuishauri TBS kufanya msako huo maeneo ya bandari na viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ili kukomesha tatizo la bidhaa hafifu kuingia kwa wafanyabiashara wa kawaida au sokoni.

Innocent alisema kuwa wafanyabiashara wengi hawana elimu ya bidhaa zinazoingia sokoni na wanaenda kununua kwa ajili ya kuuza, kama wangekuwa na elimu hali hiyo isingetokea.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano kutoka TBS, Roida Andusamile, alisema kuwa shirika hilo linafanya ukaguzi wa bidhaa sokoni na viwandani ili kujiridhisha bidhaa zinazozalishwa kama zinakidhi matakwa na viwango vya kitaifa.

Alisema ukaguzi huo ulifanyika mikoa ya Mbeya, Sumbawanga na Iringa na walilenga kukagua bidhaa za aina tatu ambazo ni mabati, nguo za ndani za mitumba pamoja na vilainishi vya magari na mitambo.

Alisema kuwa ndani ya mikoa hiyo wamekutana na changamoto ya uwapo wa bidhaa hafifu sokoni hasa za mabati ambazo zinatakiwa kuondolewa.

"Tumekamata bidhaa ambazo hazifai ikiwamo nguo za ndani ya mitumba, mabati na vilainishi zenye thamani za shilingi milioni 247, hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya wazalishaji wa bidhaa hafifu sokoni na uthibiti wa uingizaji wa bidhaa hafifu sokoni utaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha soko la Tanzania linakuwa na bidhaa bora," Andusamile alisema.

Alisema kuwa watajiimarisha katika maeneo ambayo bidhaa zinaingia ikiwamo mipakani, bandari mbalimbali, viwanja vya ndege, lengo likiwa ni kuhakikisha bidhaa zinazoingia zina ubora, huku akiomba wananchi kutoa taarifa za uwapo wa bidhaa feki.

Mkaguzi wa TBS, Baraka Mbajije, alisema wamebaini changamoto kadhaa kwenye masoko katika mikoa hiyo hasa uwapo wa bidhaa nyingi za nguo za ndani za mitumba katika soko la Sido la jijini Mbeya.

Mbajije alisema kuwa wamepata jumla ya belo 31 zenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa wauzaji wadogo na changamoto kubwa waliyokutana nayo ni wauzaji wadogo kutokuwa tayari kuwataja waingizaji wakubwa wanaowauzia.

Mbajije alisema kuwa Sheria ya Viwango namba 2 ya mwaka 2009, kifungu cha 20 (6) imekataza usambazaji, uzalishaji au uuzaji wa bidhaa ambazo hazikidhi matakwa ya viwango na sheria hiyo hiyo imeelekeza kifungu cha 27 kwamba "ukikutwa unasambaza bidhaa hafifu na mahakama ikithibitisha utatozwa faini ya shilingi milioni 50-100."

Alisema kuwa kifungu cha 30 kinaeleza kama mtu akikubaliana na matakwa ya viwango kama ilivyoelekezwa na mkaguzi na akaridhia penati ambayo inatolewa na Mkurugenzi Mkuu wa TBS ni kumtoza kiasi kisichozidi Sh. milioni 20.

Alisema kuwa madhara ya kuvaliwa kwa nguo za ndani za mitumba ni ugonjwa wa ngozi pamoja na kupatwa na ugonjwa wa kansa.

Naye Mhandisi Donald Manyama ambaye ni Mkaguzi Mwandamizi wa TBS, alisema kumekuwa na uchakachuaji wa mabati ya 'Msauz' kwa kuongeza geji 30 badala ya 28 na hivyo kuwapotosha wananchi na kuwauzia bidhaa ambazo hazistahili.

Ofisa Biashara Mkoa wa Iringa, Gervas Kahemela, alisema mkoa una utaratibu wa kukagua bidhaa hafifu sokoni kupitia maofisa biashara wa halmashauri, lakini Mkuu wa Mkoa, Ally Hapi, amekuwa akikutana na baadhi ya wafanyabiashara wa kila makundi kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu uwapo wa bidhaa feki.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda ambaye pia ni mlezi wa CCM Mkoa wa Manyara, akiwa na mavazi ya jadi aliyovishwa na wazee wa kimila wa Kimasai kwenye ziara yake wilayani Simanjiro jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wahamiaji 19 haramu wakamatwa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATU 19 wanaodaiwa kuwa ni raia wa Ethiopia wamekamtwa na Jeshi la Polisi mkoani humo, wilayani Nyamagana, wakidaiwa kufichwa katika nyumba ya Benedictor Gervas (57).

Akizungumzia kukamatwa kwa watu hao, Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Muliro Jumanne, alisema watu hao walikamatwa Machi 19, majira ya saa 11:00 baada ya kupatikana kwa taarifa za kiintelijensia.

"Ni kweli tumewakamta wahamiaji hawa haramu tumewakuta katika chumba walichopangiwa na mtuhumiwa Manka Kagulu (23), ambaye ni mpangaji wa nyumba ya Gervas siku tatu kabla ya kukamatwa kwa wahamiaji hao," alisema Muliro.

Aidha, katika tukio la pili Kamanda Muliro, alisema wanawashikilia waganga wa jadi 16 wakiwa nyara za serikali na kati yao 10 ni wanawake kwa tuhuma za kupiga ramli chonganishi ambazo zinasababisha maafa makubwa ndani ya jamii.

"Waganga hao wanaopiga ramli chonganishi tumewakamata na nyara za serikali ambazo ni mikia ya nyumbu miwili, magamba ya chatu, vipande vya mayai ya mbuni, pembe za wanyama pori, mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya simba, ngozi ya nyegere, vipande vinne vya ngozi ya wanyamapori wa aina tofauti," Muliro.

Aidha, Jeshi la Polisi pia limekamata watuhumiwa wanane wanaodhaniwa kujuhusisha na matukio ya kiuhalifu wakiwa katika hatua za awali za kupanga njama za kutenda uhalifu, hata hivyo, polisi mkoani hapa wamepania kusambaratisha mtandao huo.

# Mbaroni kwa madai ya kutaka kujiua

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga, linamshikilia msichana mwenye umri wa miaka 17, wilayani Kahama kwa kosa la kujaribu kujiua kwa kunywa vidonge vingi na unga wa betri za remote baada ya kudaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wa mama yake mdogo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Richard Abwao, tukio hilo lilitokea Machi 18, majira ya saa tisa alasiri katika Kijiji cha Mwime Ilindi Kata ya Zongomela, Halmashauri ya Mji ya Kahama.

Alidai kuwa msichana huyo alijaribu kujiua kwa kunywa vidonge vingi pamoja na unga wa betri za remote uliochanganywa na maji kwa madai ya kumuiga mtoto wa mama yake mkubwa Yohana Petro (19) aliyekunywa vidonge vingi kwa lengo la kujiua.

Aidha, Kamanda Abwao alidai, chanzo cha tukio hilo ni wa wazazi wa Petro kuwa na mgogoro wa muda mrefu na mama yake Magdalena Lucas (39), kumtuhumu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mume wake.

Pia alidai baba mzazi wa Petro, Petro Dalali (41), amekuwa akimtuhumu mtoto wake Yohana kutoka kimapenzi na msichana huyo ambaye ni mtoto wa shemeji yake.

Alidai kuwa Machi 18, Yohana alifika nyumbani kwa msichana huyo na kuingia ndani kisha kunywa vidonge vingi na msichana huyo alipoona hivyo naye alimeza vidonge vilivyobaki na kuponda unga wa betri na kunywa na maji.

Aliendelea kudai kuwa wazazi wa pande zote mbili, Dalali na Magdalena na mzazi wa msichana huyo wanashikiliwa na polisi kwa mahojiano.

Aidha, alisema msichana huyo na Yohana wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama wakiwa chini ya ulinzi na hali zao zinaendelea vizuri na ushahidi utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kujaribu kujiua.

# Vijiji 1,800 vyapata umeme wa REA

**Na George Tarimo,** IRINGA

VIJIJI 1,800 nchini vimefikishiwa huduma ya umeme kupitia miradi ya umeme inayotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa awamu ya tatu, huku vingine vikiwekwa kwenye mpango wa uboreshaji kufikisha huduma hiyo muhimu katika vijiji vyote nchini.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema hayo juzi kwenye ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ya kukagua miradi ya umeme inayotekelezwa na REA katika vijiji vya Ngano wilayani Iringa na Idinginayo, Mji Mdogo wa Ilula wilayani Kilolo.

Mgalu aliwataka makandarasi kufikisha huduma ya umeme kwenye taasisi za serikali zikiwamo shule, zahanati na makanisa, huku akiipongeza kampuni ya Sengerema kwa kujiongeza na kufanya hivyo pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) na REA kwa kutoa huduma bora.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mariam Ditopile, alisema lengo la serikali katika kufikisha huduma ya umeme vijijini ni kuchochea maendeleo kupitia sekta zote ikiwamo sekta binafsi ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya serikali ya uchumi wa kati.

Ditopile alisema Bunge na Serikali vinajitahidi kushirikiana kuhakikisha kwa namna yoyote wananchi wanapata umeme ndiyo maana changamoto wanazoziona baada ya miradi ikiwamo suala la wigo na kupitiwa kwa taasisi, pia wanataka wananchi wapate umeme kwa gharama nafuu.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Iringa, Mohammed Abdallah, alisema katika maeneo ambayo umeme wa REA umefika, wananchi wameendelea kuchangamkia huduma hiyo, huku viwanda vidogo pia vikiendelea kuanzishwa hali inayoashiria uwapo wa kiu ya muda mrefu ya huduma hiyo kwa wananchi.




Laura Demestek anayefanya kazi ya kujitolea kwenye Shirika la CUSO International, akielezea namna wanavyopambana kutokomeza ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, kwenye mkutano wa wadau wa kupinga matukio ya ukatili mkoani Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Matatani akidaiwa kumbaka mgonjwa wa kifafa

**Na Gurian Adolf,** NKASI

POLISI mkoani Rukwa inamshikilia mhudumu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere, Nicholas Bakayemba (35), kwa tuhuma za kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 38 anayedaiwa kuwa na ugonjwa wa kifafa.

Mwanamke huyo anaishi nyumbani kwa wazazi wake katika kijiji cha Kipundu, Kata ya Kipundu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Mathias Nyange, hakuweza kupatikana kuthibitisha kutokea kwa mkasa huo.

Hata hivyo, taarifa kutoka katika jeshi hilo zilieleza kuwa baada ya taarifa za tukio hilo kufikishwa katika Kituo cha Polisi Wilaya ya Nkasi, jeshi hilo lilianza kumsaka mtuhumiwa huyo.

Kwa mujibu wa mtoa taarifa, mtuhumiwa huyo awali alikuwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mbwende kabla ya kuhamishiwa katika Ofisi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere kama muhudumu wa ofisi.

"Mtuhumiwa alifika nyumbani kwa wazazi wa mwanamke huyo, juzi, majira ya saa nne asubuhi na kumkuta akiwa peke yake ndipo alipomuomba maji ya kunywa na kumkamata na kisha kumbaka," alidai mmoja wa ofisa wa Jeshi la Polisi wilayani humo kwa sharti la kutoandikwa majina yake gazetini kwa kuwa si msemaji wa jeshi hilo.

Alidai kuwa polisi ilifanikiwa kumnasa mtuhumiwa huyo jana majira ya saa saba mchana na anaendelea kushikiliwa kwa mahojiano na anatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya uchunguzi wa awali kukamilika.

# Shehena kilo 2,200 bangi yateketezwa

**Na Anthony Gervas,** RORYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Polisi wa Tarime na Rorya, limeteketeza bangi yenye uzito wa kilo 2,212 ambayo ilikamatwa katika operesheni maalum iliyoanza Agosti 20, mwaka jana hadi Machi 20, mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime-Rorya, Henry Mwaibambe, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa watuhumiwa wa dawa hizo za kulevya walikimbia kabla ya kukamatwa.

"Leo (juzi) tuna kazi ya kuteketeza dawa za kulevya aina ya bangi kilo 2,212 ambazo tulizikamata katika operesheni maalum endelevu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huu ambayo ilianza Agosti 2018, hadi Machi 20, mwaka huu. Tuliomba kibali mahakamani lakini watuhumiwa walikimbia kabla ya kuwakamata," alisema.

Kamanda Mwaibambe alisema kuna zipo kesi kubwa 15 za bangi katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime, ambazo zinawakabili watuhumiwa 41 na vielelezo 28 vilivyokamatwa na dawa hizo pamoja na magari manane.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mwaibambe aliwaonya watu katika mkoa huo wa kipolisi kuachana na kilimo cha bangi na biashara ya dawa za kulevya kwa kuwa watakaobainika wataangukia katika mikono ya dola.

Aliwataka wananchi hao kufanya kazi zingine za uzalishaji mali ambazo ni halali ili kuepukana na usumbufu na hasara wanazozipata wakulima wa aina hiyo pamoja na wasafirishaji wa dawa hizo hatari.

Pia alisema katika operesheni hiyo, jeshi hilo pia lilikamata katoni 10 za pombe kali aina ya viroba vilivyokuwa vikitokea Uganda kwa ajili ya biashara ambavyo pia viliteketezwa na watuhumiwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Charles Kabeho, alisema watu watakaokamatwa wamelima bangi watawajibika kwa kuyafyeka mashamba hayo na kuchukuliwa hatua za kisheria.

# Wafanyabiashara wa mifugo walilia tozo kubwa mnadani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
LONGIDO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, imekumbana na kilio cha wafanyabiashara wa mifugo kutoka Tanzania kwenda nchini Kenya wakilalamikia ushuru mkubwa wanaotozwa. Walisema kwa sasa wanatozwa Sh. 15,000 hadi Sh. 30,000 kwa ng'ombe mmoja na Sh. 4,500 hadi Sh. 7,500 kwa mbuzi mmoja. Walisema tozo hiyo ni kubwa na inawafanya wengi washindwe kumudu.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ambaye aliambatana na kamati hiyo, pamoja na Katibu Mkuu wake Profesa Elisante Ole Gabriel walishuhudia kilo cha wafanyabiashara hao. Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Saruni Laizer, alitoa ombi hilo mbele ya kamati hiyo, akidai tozo hilo limesababisha watu wengi kushindwa kupeleka mifugo kwenye mnada wa mifugo. Tozo hiyo inatozwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mujibu wa sheria. Alisema awali kabla ya wizara kuchukua mnada huo kutoka kwa Halmashauri ya Longido, kwa siku yalikuwa yanaingia magari 25 ya ng'ombe na magari 30 ya mbuzi, lakini kutokana na tozo kubwa siku hizi kwa siku linaingia gari moja tu la ng'ombe na gari nne za mbuzi.

Alisema mnada huo ulikuwa unakutanisha wafanyabiashara kutoka mikoa sita hapa nchini ikiwamo kanda ya kaskazini ambao walikuwa wanautumia kama kituo cha kusafirishia mifugo kwenda nchi jirani ya Kenya na kwamba kama serikali haitachukua hatua za haraka za kupanga tozo rafiki utakufa.

"Mheshimiwa Naibu Waziri tuliwahi kulalamikia juu ya tozo hizi kuwa ni kubwa na kwamba siyo rafiki kwa wafanyabiashara leo (jana) mbele ya kamati hii wabunge nataka niwaambie kuwa kiatu kinatubana na kinakaribia kuleta kidonda cha kukamua usaa. "Naomba nikutahadharishe kuwa ni vyema ukatununulia kiatu kipya, kuliko kutumia gharama kubwa ya kuja kutibu kidonda," alisema.

Alisema hivi sasa wafanyabiashara wengi wanatorosha mifugo kwenda nje ya nchi, huku serikali ikipata hasara kubwa kutokana na tozo kubwa waliyoweka, ambapo hawakushirikisha wafanyabiashara wakati wa kuandaa kanuni hiyo inayotaka wafanyabiashara kulipa tozo hizo kwa ajili ya kupeleka mifugo nje ya nchi. Baada ya maelezo hao wajumbe wa kamati hiyo walionekana kukerwa na kitendo cha wizara kutoshirikisha wafanyabiashara hao ambao ni wadau wakubwa.

Akizungumza kwa niaba ya wabunge hao Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mahmoud Mgimwa, aliitaka wizara kuwasilisha kwao malalamiko yote ya wafanyabiashara katika mnada huo, ili marekebisho ya kanuni hiyo ya kutoza Sh. 30,000 kwa ng'ombe na mbuzi Sh. 7,500 ifanyiwe marekebisho kabla ya kuanza kwa Bunge la Bajeti.

Kuhusu halmashauri kupata ushuru wa Sh. 1,000 kwa ng'ombe mmoja na wizara kuchukua Sh. 4,000 na zingine kwenda serikali kuu, mbuzi Sh. 500 na wizara Sh. 1,000 kamati hiyo ilipinga vikali na kuitaka wizara kugawana nusu kwa nusu kwenye tozo za ushuru kwa sababu mnada huo ulikuwa mali ya halmashauri na wizara ikaupora kinyemela. Akizungumza kwa niaba ya wabunge wenzake Mbunge wa Babati Vijijini, Jitu Son, alisema mnada huo ulikuwa ni mradi mkakati wa Halmashauri ya Longido ambapo ulifadhiliwa na MIVARF, lakini umeporwa na wizara hivyo ni vyema wakagawana mapato hayo asilimia 50 kwa 50.



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wakazi wilayani Longido, wakati alipotembelea wilaya hiyo na kamati yake kujionea mradi wa maji wa Sh. bilioni 15.8 zilizotolewa na serikali. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wampongeza JPM kuwatua ndoo kichwani

**Na Cynthia Mwilolezi,**
LONGIDO

WAKAZI wilayani Longido, wamempongeza Rais John Magufuli, kwa kuwaondolea adha kukosa huduma ya maji, baada ya mradi wa maji wa Sh. bilioni 15.8 kutoka chanzo cha Mto Simba, wilayani Siha, Mkoa wa Kilimanjaro, kukamilika Machi 31, mwaka huu.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji inayoongozwa na Mwenyekiti, Mahmoud Mgimwa, iliyotembelea wilaya hiyo kujionea miradi ya maji na mifugo, mmoja wa wakazi hao, Theresia Kishuma, alisema uamuzi wa Rais Magufuli kuwapelekea maji wilaya yao ni cha kupongezwa kwa kuwa ameokoa maisha yao na mifugo.

Alisema tangu nchi ipate uhuru tatizo kubwa la wilaya hiyo lilikuwa ni maji.

"Lakini nashindwa hata kusema, naomba tu wabunge nyie mtufikishie kwa Rais pongezi na furaha zetu kwa kuwa ametutua ndoo kichwani, tumeteseka sana na mifugo yetu, kuna wakati ilikufa kwa sababu ya ukame uliotokana na ukosefu wa mvua na kukosa maji kwa sababu ya wilaya yetu ni kame," alisema.

Aliomba wabunge hao kuhakikisha wanasimamia maji hayo yatoke mfululizo bila kukatika ili wasahau machungu ya nyuma waliyokuwa nayo.

Naye Judith Lyimo, aliomba kamati hiyo, huku akitoa machozi ya furaha kufikisha pongezi zao kwa Rais Magufuli, kwa kuwakumbuka wakazi wa wilaya yao na mifugo ambayo ndio tegemeo lao asilimia 99.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mahmoud Mgimwa, aliahidi kufikisha pongezi zao kwa Rais na kuwataka wananchi hao kulinda miundombinu ya maji ili idumu miaka mingi.

Naahidi pia tutarudi tena hapa Longido kuangalia kama mnatunza mradi huu wa gharama kubwa na naagiza Mkuu wa Wilaya endapo miundombinu itaharibiwa sehemu fulani kamata watu wote wa eneo hilo ili iwe fundisho kwa uovu huo, maana wanapaswa kufichua wahalifu sio kuwaficha," alisema.

Awali akisoma taarifa ya maji wilayani humo, Katibu Tawala, Toba Nguvila, alisema mradi huo japo mpya umeanza kukabiliwa na changamoto ya kutobolewa mabomba kwa baadhi ya maeneo kunakosababishwa na ukosefu wa maji ya binadamu na mifugo yao licha ya mabomba ya maji kupita katika vijiji vyao.

"Baadhi ya wakazi wa vijiji wameona mabomba yamepita maeneo yao na wao hawana maji wanaamua kutoboa ili mifugo yao na wao wapate maji sasa hili ni tatizo kubwa," alisema.

Wakichangia suala hilo baadhi ya wabunge wa kamati hiyo, Justine Monko wa Jimbo la (Singida Kaskazini), Katani Ahmad Katani (Tandahimba) na Pascal Haonga, (Mbozi), walisema wakazi wa wilaya hiyo asilimia kubwa ni wafugaji hivyo na mahitaji ya maji kwao makubwa.

Walishauri serikali kuhakikisha wanakopitisha mabomba ya maji kuweka maeneo ya wananchi kupata huduma hiyo vinginevyo kutoboa mabomba ni lazima kwa sababu haiwezekani maji yanapita kwenye vijiji vinne yakaenda kijiji cha nane huku yalikopita wakikosa maji hayo.

"Mkiwapatia maji haya wananchi wenyewe watakuwa walinzi wa miundombinu hii, vinginevyo mtatumia nguvu kubwa na bado wananchi wataendelea kuharibu miundombinu hii, dawa hapa wapeni maji," alisema Haonga.

## 45,000 wapata huduma ya afya ya kinywa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI 45,000 katika mikoa takribani 23, ya Tanzania Bara na Visiwani wamenufaika na mafunzo ya kupata huduma ya elimu, uchunguzi wa afya ya kinywa na meno kutoka kwa wataalamu wa Chama cha Afya ya Kinywa na Meno hapa nchini.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Afya ya Kinywa na Meno Duniani juzi, Rais wa chama hicho nchini, Dk. Ambege Mwakatobe, alisema hadi kufikia siku ya kilele cha maadhimisho, walishatoa huduma kwa wananchi 45,000 kutoka mikoa 23 ya Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema tangu siku ya ufunguzi wa shughuli ya utoaji wa huduma hiyo, matumaini yake jamii itakuwa imenufaika na huduma hiyo, tangu walipozindua matembezi ya kuhamasisha afya ya kinywa na meno Machi 14, mwaka huu, hadi walipohitimisha kufikia siku ya maadhimisho Machi 20.

Aliongeza mategemeo yao yalikuwa kuwafikia wananchi 47,000, katika mikoa 23 ya Tanzania Bara na Visiwani.

Hata hivyo, alisema Shirikisho la Afya ya Kinywa na Meno, limeripoti kwa kutoa utafiti kwa kugundua athari za magonjwa yapatayo 291 katika nchi 37 duniani.

Alisema kupitia tafiti hizo, zinaonyesha watu wenye magonjwa sugu ya fizi wanahusishwa kwa karibu na magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza kama msongo wa damu, kiharusi, kisukari, magonjwa ya figo na uwezekano wa kuzaa watoto wenye uzito mdogo.

Alieleza matatizo ya kinywa na meno yana jumuisha kutoboka kwa meno, magonjwa ya fizi na mfupa wa taya, saratani na maambukizo kwenye maeneo ya uso, taya na shigo, matatizo ya mdomo wazi, kuumia mifupa ya taya, mdomo, ulimi pamoja na meno.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema magonjwa hayo, yanasababishwa na utumiaji wa sigara, tumbaku, na ugoro, unywaji wa pombe kupita kiasi, ulaji wa vyakula hatarishi na kutokufanya mazoezi ya mwili.

Alisema mwaka 2018, walitoa huduma za elimu ya afya, ushauri na matibabu kwa zaidi ya watu 38,000, nchi nzima na ilipelekea kupewa tuzo ya kimataifa ya "Most Educative Award" iliyotolewa na Shirikisho la Vyama vya Afya ya Kinywa na Meno Duniani (FDI).

# Mgambo atupwa jela miaka miwili mashtaka 13 rushwa

**Na Paul William,** SAME

MAHAKAMA ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro imemhukumu, Askari Mgambo, Tufike Tumaini, aliyekuwa akikabiliwa na mashtaka 13 ya rushwa, kutumikia adhabu ya miaka miwili jela, baada ya kutiwa hatiani.

Tumaini ametiwa hatiani kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 600,000.

Kabla ya kutoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi wa Wilaya hiyo, Judith Kamala, aliieleza mahakama hiyo kuwa mshtakiwa ametiwa hatiani baada ya kukiri makosa matano kati ya 13 yanayomkabili.

Askari huyo anadaiwa kutenda makosa hayo kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Namba 11 ya Mwaka 2007.

Katika kesi hiyo Namba 27 ya Mwaka 2019, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Suzan Kimaro, alidai kuwa mshtakiwa alikiri kuwakamata na kuwaweka mahabusu wazazi 10 ili kuwasukuma kutoa rushwa kwa kuhusika katika ucheleweshaji wa usajili wa watoto kujiunga na muhula wa masomo.

Mwendesha mashtaka huyo amedai kuwa kesi hiyo inawakabili washtakiwa wawili akiwamo pia Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Dawson Daniel.

Mwenyekiti huyo, yeye alikana makosa hayo na hivyo mashtaka dhidi yake yataanza kusikilizwa Aprili 18, mwaka huu.

Alisema kuwa, katika kesi hiyo wazazi 10 wanawatuhumu washtakiwa wote wawili kwa kuwakamata, kuwaweka mahabusu na kuwadai rushwa kwa kuwatuhumu kuchelewesha kuwasajili watoto wao kujiunga na muhula wa masomo kwa mwaka 2019 katika shule za sekondari.

Nje ya Mahakama, Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kilimanjaro, Moses Oguda, alitoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za rushwa na kuwa tayari kutoa ushahidi mahakamani pale wanapohitajika ili wanaokosa uadilifu katika utumishi wa umma waweze kupata adhabu stahiki kwa mujibu wa sheria.

"Wanaofanya vitendo vya kuomba na kupokea rushwa wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria hivyo wananchi tunawaomba mtoe taarifa na pia mje kutoa ushahidi pindi mtakapohitajika na wale wanaofanya vitendo hivi kama ni watumishi wa umma waweze kuondolewa kwenye utumishi wa umma ili kubaki na watumishi waadilifu na wanaoridhika na mishahara yao," alisema Oguda.



Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali NMB, Filbert Mponzi, akimpa maelekezo Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino (katikati), wakati wa uzinduzi wa soko la dhahabu mjini Geita. Kulia ni Meneja wa NMB tawi la Geita, Mathias Nkullua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yataja chanzo cha kukithiri ajali

**Na Paul William,** MOSHI

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Kilimanjaro, limesema ajali nyingi zinazotokea katika eneo hilo ni kutokana na baadhi ya madereva kuendesha vyombo vya moto bila leseni.

Hayo yamebainishwa jana na Kaimu Kamanda wa Kikosi hicho, mkoani hapa, Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Eliasi Mkubulo, katika mafunzo maalum kwa watumishi wa Gereza Kuu la Karanga ili kuwawezesha kutambua sheria za usalama barabarani.

Mkubulo alisema kuwa, watumiaji wengi wa vyombo vya moto hawana elimu ya kutosha juu ya usalama barabarani, ambapo Jeshi la Polisi limekuwa likihakikisha linaeneza elimu ili kuwafikia walengwa wa kujua sheria na kuzitafsiri barabarani.

Alisema kuwa kwa sasa kumekuwapo na changamoto ya baadhi ya wananchi wanaondesha magari pamoja na pikipiki kutokuwa na leseni na kwamba hali hiyo inaweza kuhatarisha maisha na kuwataka wananchi wasio na leseni kuacha kuendesha vyombo hivyo.

"Sheria ya nchi inaeleza wazi kuwa mwananchi atakayekamatwa akiendesha chombo cha moto bila kuwa na leseni atafikishwa mahakamani chini ya Kifungu Namba 76 ya Sheria Namba 10 ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 na kupewa adhabu stahiki," alisema Mkubulo.

Mkubulo alisema kuwa, kupitia mafunzo hayo yatawasaidia watumishi wa magereza kujikumbusha sheria za usalama barabarani, lakini pia kwa watumishi wasio na leseni kupitia mafunzo hayo ya siku tano yatasaidia kupata leseni.

Aidha, kamanda huyo alidai kuwa kwa sasa ajali za magari katika Mkoa wa Kilimanjaro zimepungua, lakini tatizo lipo kwa waendesha bodaboda ambapo ajali za pikipiki zimekuwa zikiongezeka na hii ni kutokana na madereva wake kutotambua sheria za usalama barabarani.

Naye Kaimu Kamanda wa Gereza la Karanga, Mrakibu Msaidizi wa Magereza, Hamiss Nyaku, alisema kuwa, mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka ambapo serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamekuwa wakipambana kuhakikisha wanapunguza ajali nchini.

Nyaku alisema kuwa, watumishi wa magereza wamekuwa wakisongwa sana na shughuli za majukumu na kusababisha kukosa muda wa kwenda katika vyuo vya udereva kujikumbushia sheria za barabarani, hivyo ujio wa mafunzo hayo utasaidia kuibua hali ya kuzitambua sheria za barabarani.

## Matukio ya ujambazi yawaliza wananchi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WANANCHI wa Kijiji cha Kimaroroni, Kata ya Kilema Kati, wilayani Moshi, wameiomba Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa kuingilia kati suala la usalama katika kata hiyo, kufuatia kukithiri kwa matukio ya ujambazi.

Aidha, wananchi hao, wameliomba Jeshi la Polisi kukitazama Kituo cha Polisi Kilema Kati kwa madai kwamba askari wake wanatoa siri za raia wema.

Wakizungumza kwa sharti la kutotajwa majina yao, wakazi hao wamesema tayari zaidi ya matukio matano yametokea kwa mwaka mmoja na wananchi wameporwa mali na kujeruhiwa kwa silaha za jadi na bunduki.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Hamis Issah, alipoulizwa juu ya taarifa hizo alishangazwa na kudai kwamba polisi hawawezi kuzuia hisia za wananchi.

Aidha, wananchi walitaja baadhi ya matukio ya uhalifu waliyoyatolea taarifa na kupewa namba KIL/RB/253/2018 na KIL/RB/44/2019 na kwamba hawaoni hatua zinazochukuliwa.

"Matukio ni mengi na moja wapo ni la Machi 18, mwaka huu, ambapo watu wanaodhaniwa majambazi walivamia nyumba ya Mbuya wakiwa na silaha mbalimbali, walijeruhi kwa kuwakata na mapanga maeneo tofauti ya mwili," alisema.

Walisema wanashindwa kuwataja wahalifu kwa madai polisi wanafichua siri, huku pia wahalifu nao hujigamba kupata msaada wa kutolewa polisi kwa kuwa wanandugu ngazi za juu ikiwamo polisi na serikalini.

Kwa upande wao majeruhi wa tukio la ujambazi walilazwa Hospitali ya Kilema, Anthony Mbuya (69) na mwanawe Elvis Mbuya walisema walivamiwa majira ya saa 8 usiku na watu wenye silaha wakitaka fedha na walipokosa waliwajeruhi kwa mapanga.

"Ghafla nilisikia watu wapo ndani na waliingia na kukata umeme, baadaye walinikamata na kunishambulia kichwani na mikononi...sikujua nini kiliendelea maana nilipoteza fahamu," alisema Mbuya.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Aloycia Lyaruu, alithibitisha madai ya wananchi na kuongeza kuwa askari katika kituo hicho hawana silaha na kushindwa kutoa msaada pale anapohitajika.



Ukurasa 16

JASHO LA MKAA ENDELEVU;
Mwanzo wa Sh. laki umewapa kuku 500 waliojaa bandani, mtaji mpya mil. 25/-



Ukurasa 19

Unayajua mauzo ya moja kwa moja?

# BUFE

Ijumaa Machi 22, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI



## Rais Akufo: Tabianchi inakaribisha njaa Afrika

Ukurasa 15



# Changamoto ya ualbino imemnoa kufikia ujasiriamali uliokamilika

- Alia nyumbani hadi kwenye ndoa
- Kauza togwa, karanga, mkaa, sasa...
- Umri wa bibi, ndoto iko palepale

**Na Romana Mallya**

MWASITI Ramadhan, ni mama mlemavu wa ngozi, mjasiriamali 'mbibi' na msusi maarufu jijini Dar es Salaam, anayepatikana katika jengo la Machinga Complex, lililopo wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam.

Ana umri wa miaka mingapi sasa, jibu ni 'mbibi wa kweli' akiwa na miaka 68, lakini kwa kauli na matendo kachangamka mno, akisaka pesa.

Ukimuuliza swali jingine, ni mtaji wa kiasi gani alioanza nao? Mama

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## BIASHARA KATIKA PICHA

Ukurasa 17




KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Uchumi Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

**Biashara**

**Kielezo**

TSI 3,481.50 -0.13
DSEI 2,065.75 +4.99

Thamani za Hisa (bln) 19,911.50

Mauzo 84,632,700.00

Hisa 625,309

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| ACA | 6,000 | -1.64% |
| JHL | 9,250 | -0.54% |
| NICO | 165 | -2.94% |
| USL | 10 | -33.33% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| EABL | 4,660 | +2.64% |

BIASHARA

# Changamoto ya ualbino ime kufikia ujasiriamali uliokam

**Inatoka Uk.13**

Mwasiti ana jibu kuwa ni Shilingi 10,000, ambayo hana kumbukumbu na mwaka aliyoanza nayo, ila anachokirejea 'alipokuwa msichana.'

Nipashe ilimshuhudia katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani iliyopita hivi karibuni, akiwa mstari wa mbele 'akijimwaga' na kaulimbiu "Badili Fikra Kufikia Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu."

Mjasiriamali huyo, mkazi wa Kinondoni, anasema kuingia kwake katika biashara hiyo miaka 40 iliyopita, ni kutokana na changamoto aliyokabiliana nayo wakati huo kuanzia kwenye familia na jamii.

"Mimi ni mtoto wa kwanza kati ya watoto saba na kati yetu peke yangu ndiyo mwenye ulemavu wa ngozi. Unyanyapaa wa kundi letu ulianza tangu zamani, hata yale mapenzi ya wazazi kwa mtoto yalikuwa ni tofauti baina ya wale waliozaliwa bila matatizo," anasema.

Mwasiti hilo ndilo lilimuingiza kwenye biashara hiyo mapema, akinuia kujikimu mapema kimaisha, huku akilalamika alikumbana hata na mgogoro mzito kutoka kwa mumewe.

Mwasiti, mama wa mtoto mmoja, anasimulia kuwa wakati bado yupo kwa wazazi wake akiwa na umri mdogo, alianza kuuza karanga, kukaanga maandazi na mwishowe akajikita kwenye uuzaji wa togwa, ili apate riziki.

"Nimeuza hadi togwa ili tu nipate chochote maisha yasonge. Unajua ukiingia kwenye biashara, halafu unaona bado haufanikiwi, utajikuta unajaribu biashara hii, kesho ile ndivyo nilivyokuwa nafanya. Mwishowe niliachana na biashara ya togwa na kuanza kuuza mkaa," anasimulia.

Mwasiti anasema wakati akiuza tongwa mwaka 1972, ndipo alipompata mtoto wake wa kiume, ambaye baba yake alimkataa. Anasimulia: "Kabla ya baba wa mtoto wangu, nilikuwa na uhusiano na mwanaume mwingine ambaye alinipa ujauzito wa kwanza ambao ulitoka.

"Huyu baba wa mtoto wangu niliyejifungua mwaka 1972 baada ya kubaini nina ujauzito naye alikataa, nikamlea mtoto wangu mwenyewe kwa togwa hadi alipotimiza miaka minane."

> **"Nakumbuka mara ya mwisho alivyokuja aliniambia, anakwenda akifanikiwa atarudi Tanzania kuchukua watoto wake aliokuwa amewazaa. Sijawahi kumuona tena, sijui ni mzima au la maana sina mawasiliano naye."**



Mwasiti Ramadhan. **PICHA: ROMANA MALLYA.**

**Vituko vya ndoa**

Mwasiti anasimulia kwamba, wakati mwanawe alipokuwa na umri wa miaka minane, alikutana na mwanaume mwingine aliyemuoa na anaendelea: "Nilikuwa naishi na mume wangu kwenye nyumba ya familia na mwaka 2009 akanigeuka..."

Mwasiti anasema alianza kuona vituko kutoka kwa mume wake ambavyo anadai ilikuwa na sura ya jinai, ambayo alilazimika na familia yake kuifikisha polisi na hata shauri likafika mahakamani wakatengana.

Mwasiti anasema, biashara ya mkaa aliyoifanya kabla ya usajiriamali wa usukaji vikapu, aliiacha alipogundua inamletea athari kiafya, aliamua kurithi kazi ya mama yake mzazi.

"Mama yangu alikuwa anapenda kusuka mikeka nilikuwa naangalia hatua kwa hatua anavyofanya, nilifanikiwa kuelewa lakini sikutaka kuisuka mikeka, nikajifunza namna ya kuten-

UCHUMI

**Mwanzo wa Sh. laki umewapa kuku 500 waliojaa bandani, mtaji mpya mil. 25/-**

Ukurasa 16

UCHUMI

**Siku Iringa walipotafakari namna wanavyoukalia uchumi wa maziwa**

Ukurasa 18

BIASHARA

**Unayajua mauzo ya moja kwa moja?**

Ukurasa 19

# emnoa
# hilika



geneza vikapu kwa ajili ya biashara," anaeleza.

Mwasiti anasema, kikapu chake cha kwanza alichosuka alikiuza kwa bei ya shilingi 5,000 na ndipo alipoingia rasmi kwenye biashara aliyodumu hadi sasa, bila ya kutaja siku aliyoanza.

"Kwa sasa nimechukua kizimba kwenye jengo la Machinga Complex Ilala, ambako kila mwezi ninalipa kodi ya Sh. 30,000.

> **"Lakini, ndoto yangu haijatimia nimeishia kuwa mjasiriamali mdogo, ambaye naingiza fedha ya kujikimu kimaisha na wakati mwingine hukosa kabisa kutokana na hali ya biashara."**

Kwa mwezi nina uwezo wa kufuma vikapu 10. Wateja wangu ni wadogo wadogo, hivyo faida inategemea ninaweza kupata Sh. 50,000 kwa mwezi au pungufu," anaeleza.

Huku akizungumzia malengo yake, anasema bado hajatimiza ndoto yake aliyokuwa nayo na anaendeleza simulizi yake:

"Nilipozaliwa na nilipojiona nipo tofauti na wenzangu, nilitamani siku moja niwe mfanyabiashara mkubwa na mlipa kodi mkubwa katika nchi yangu.

"Lakini, ndoto yangu haijatimia nimeishia kuwa mjasiriamali mdogo, ambaye naingiza fedha ya kujikimu kimaisha na wakati mwingine hukosa kabisa kutokana na hali ya biashara."

Mwanamke huyo anasema, licha ya kuwa na umri mikubwa wa miaka 68, bado hajakata tamaa na anaamini kuna siku ndoto yake itatimia, ikiwa watajitokeza watu wa kumwongezea mtaji wa biashara yake.

**Changamoto**

Anataja changamoto anazokumbana nazo kwenye ujasiriamali wa ufumaji vikapu, ni kwamba anatumia muda mrefu katika ufumaji huo wa vikapu na hajafikia kwenye usajiriamali wa kutumia vifaa maalum.

"Wenzetu wanatumia mashine maalum kusuka vitu hivi, mimi bado natumia mikono. Ndio maana kwa mwezi naishia kusuka vikapu saba au pungufu ya hapo," anasema na kufafanua:

"Nilitamani niwe kama wenzangu niwe na biashara kubwa, kwa bahati mbaya sina mtaji. Sikusoma, basi naishia huku niliko, ila sijakata tamaa.

"Ninaiomba serikali na wadau wanisaidie mtaji. Bahati nzuri mimi ni mnufaika wa mafunzo yanayotolewa na Shirika la Under The Same Sun (UTSS)."

Anaeleza kuwa kupitia mafunzo yanayotolewa na shirika hilo, ameweza kujifunza kutengeneza vitu mbalimbali zikiwamo uokaji wa keki, sabuni, shanga na usindikaji vyakula.

Mwanawe 'azamia'

Kuhusu mtoto wake, anasema 'alizamia' kwenda nje ya nchi na alirudi Tanzania mara tatu, kisha akaondoka tena. Anaeleza: "Tangu ameondoka hadi sasa ni miaka 20 hajawahi kurudi tena.

"Nakumbuka mara ya mwisho alivyokuja aliniambia, anakwenda akifanikiwa atarudi Tanzania kuchukua watoto wake aliokuwa amewazaa. Sijawahi kumuona tena, sijui ni mzima au la maana sina mawasiliano naye."

**Kutoka UTSS**

Ofisa Taaluma wa UTSS, Grace Wabunhu, ambaye naye ana ualbino, anasema shirika hilo lina programu ya kuwasaidia wanawake wenye ualbino au wenye watoto walio na ualibino kwa kuwapatia mafunzo yatakayowawezesha kujikimu kimaisha.

"Kati ya wanawake wanaonufaika na programu hiyo, wapo ambao watoto wao wapo chini ya ufadhili wa shirika, lakini wakirudi katika maisha ya kawaida hawajiwezi.

"Kwa hiyo, tunawasaidia kidogo. Tumewawezesha kufungua kikundi cha wanawake wenye ualbino au watoto wenye ualbino kwa Dar es Salaam na mkoani Mwanza," anasema Grace.

Anaeleza kwamba, kinachofanywa na UTSS ni kuwajengea uwezo wanawake, kwa kuwapa mafunzo kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Grace anasema, mkoani Dar es Salaam, kuna jumla ya wanawake tisa wameshayapata na wameunda kikundi na kimeshasajiliwa.

"Kama tunavyojua wadhamini wengi hutoa fedha za kuwajengea uwezo, ambayo ndio haya mafunzo. Kwa hiyo, tunaomba watu binafsi na serikali kuviangalia vikundi hivi kwa kuwawezesha zaidi kimtaji au mikopo, kwa sababu wanawake hawa kama Mwasiti, tayari ana kianzio cha mtaji, lakini anahitaji kuinuliwa zaidi afikie ndoto yake," anasema.

# Rais Akufo: Tabianchi inakaribisha njaa Afrika



Rais Nana Akufo.

**Na Jenifer Julius, Accra, Ghana**

MATAIFA ya Kiafrika yanaelezwa yako hatarini kukumbwa na njaa, kutokana na mabadiliko ya tabianchi kama hatua ya kupunguza joto la dunia kwa walau nyuzi mbili haitochokuliwa mapema.

Akizungumza jijini hapo, katika mkutano wa Wiki ya Mabadiliko wa Tabia Nchi unaoendelea Accra Ghana , Rais Akufo Addo wa nchini hapo, anasema nchi yake imeamua kuingia katika kampeni kupunguza joto la dunia kupitia sekta ya kilimo.

Anasema, katika utekelezaji wake imewekeza kwenye kiwanda cha kijani, ikianzisha mradi maalum unaojulikana kama 'One Village One Dam' (kijiji kimoja bwawa moja) unaolenga kupunguza joto la dunia kupitia kilimo.

Rais Addo anasema, ni mradi utakaohakikisha zaidi ya miti milioni 20 itapandwa na vijana nchini kwake, ili kukabiliana na mabadiliko hayo, ambayo ni tishio kwa dunia kwa jumla.

"Mabadiliko ya tabianchi ni tishio kubwa katika kufikia mipango ya malengo endelevu ya dunia (SDG's), kwa kuwa inasababisha kuwapo majanga kama vile kuchafuka kwa bahari, mafuriko na ukame," anasema Rais Akufo.

Nchi za Afrika, zinaelezwa kuathitika sana kwa sababu uchumi wake haujitoshelezi kupambana na mabadiliko hayo ya tabia nchi na hazina uwezo wa kukabiliana na mabadiliko hayo vilivyo.

Rais Addo amezitaka nchi za Afrika kutenga bajeti za kutosha, kukamilisha utekelezaji miradi yake inayolenga kupunguza joto la dunia.

Anasema, mabadiliko ya tabia nchi pia yanatishia ukuaji uchumi, hivyo anazitaka nchi za Kiafrika kufuata Mkataba wa Mazingira wa Paris, kuhusiana na upunguzaji wa joto la dunia.

Waziri wa Mazingira wa Ghana, Frimpon Baoteng, anasema mabadiliko ya tabia nchi ni changamoto kubwa inayosababisha ukame na kukauka kwa mito mikubwa nchini kwake na Afrika.

Wakati nchi za Afrika zikijadiliana namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, inaelezwa majanga yatokanayo na uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana katika sehemu nyingi.

Hivi karibuni, zaidi ya watu 300 nchini Msumbiji walipoteza maisha, kutokana na mafuriko, huku nchi za Zimbabwe na Malawi zikiathiriwa na kimbunga cha kitropiki.

**BEI YA MAZAO >>** MCHELE 184,167 | ULEZI 141,100/-

**FEDHA >>** RAND 159.34 | KSH 22.75 | USH 0.6197 |

BIASHARA

JASHO LA MKAA ENDELEVU;

# Mwanzo wa Sh. laki umewapa kuku 500 waliojaa bandani, mtaji mpya mil. 25/-

- Wajenga banda mil. 16/-; mbioni kuwa kampuni
- Wote waajiriwa wa mshahara kwenye mradi wao

**Na Christina Haule, Morogoro**

MRADI wa ufugaji kuku unaoendeshwa na kikundi kinachojulikana kama 'Bosi Kuku' katika kijiji cha Mlilingwa, Kata ya Tununguo, Ngerengere wilayani Morogoro, kazi zake zimewasha taa ya mafanikio.

Hiyo ni kutokana na mafanikio ya kumiliki mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 25 sasa, ikiwa ni matokeo chanya ya Mradi wa Mageuzi katika Sekta ya Mtaa Tanzania (TTCS), maarufu kama mkaa endelevu.

Selemani Mwishehe, mwenyekiti wa kikundi hicho cha wanachama 12 kilichoanzishwa mwaka 2015; kinamama watatu na wanaume tisa, alipozungumza katika maonyesho ya wazi ya shughuli za mkaa endelevu kijijini Mlilingwa, ana mengi.

Anataja mzizi wa mafanikio kupitia mradi wa uchomaji mkaa, ulianza kila wiki walipokutana na kila mmoja alichanga fedha shilingi 10,000 na kukusanya shilingi 120,000. Mtaji ulipofika shilingi milioni moja, walianza kutengeneza banda dogo.

Mwishehe anasema, walianza kwa kununua mbegu za vifaranga kwenye shamba la kuku na walipokua waliwauza na kubakiza wachache, kwa ajili ya kuendeleza mradi.

Pia, anasema fedha zingine za mapato ya mauzo, walitumia kutotoa mayai 1000 kwa wakati mmoja na kuuza kuku 1000, kila baada ya miezi mitano waliowapatia. Walivuna kati ya shilingi milioni 12 hadi 13.

Mwishehe anasema, hadi sasa wameshauza kuku mara tatu tangu kuanza mradi na wamejenga banda kubwa la kuku lenye thamani ya shilingi milioni 16.

Anafafanua kuwa, mpaka sasa wana kuku 500 na 100 kati yao ni jogoo na majike 400 na mbolea itokanayo na kinyesi cha kuku, wanawauzia walima mboga, pia wanauza mayai, vifaranga na kuku wakubwa.

Katika kuhudumia, anasema wanatumika katika nafasi ya wafanyakazi na wanalipana ujira shilingi 300,000 kila mwezi, lengo ni kupandisha daraja mtaji mradi uwe kampuni, badala ya kikundi.

**Changamoto**

Mwishehe anasema kuwa, mabanda yao ni madogo hayakidhi hitaji la idadi ya kuku walio nao na wanaoongezeka.



Nyuwaji Bakari, Katibu wa Wachoma Mkaa wa Mlilingwa, Morogoro, akieleza jambo kuhusu uandaaji wa mkaa endelevu. **PICHA: CHRITISTINA HAULE.**



Kuku wa kienyeji, aina ya mradi unaoendeshwa na kikundi cha Bosi Kuku. **PICHA: MTANDAO.**

> **"Pili, namna gani rasilimali misitu zitawanufaisha ili waweze kuona rasilimali hizo ni mali yao kwa kupata faida ya moja kwa moja kama vile kupata bima za afya na shughuli za maendeleo mahali walipo."**

Mtazamo wao ni kuwa na mabanda manne kukidhi hitaji la uzalishaji kuku 4,000 wakubwa watakaoweza kuingiza kati ya shilingi milioni 48 hadi 52 kila miezi mitano inapopita.

Kuku hao wanaweza kuhudumiwa panapokuwapo banda lenye wastani wa mita 80, linaloweza kuingiza kuku 1,000. Ushauri wake kwa vijana wengine wanaojishughulisha na mkaa endelevu, waungane kwenye vikundi wawekeze katika namna wanavyoshauriwa.

Mmoja wa wana - kikundi hicho cha kuku, Barat Gatilali, anasema amefanikiwa kujenga nyumba ya vyumba vitatu yenye thamani ya shilingi milioni 3.5, kitu ambacho hakuwa nacho kabla ya mradi.

Anasema kushamiri kikundi hicho, ni matokeo ya mradi mkaa endelevu kuwa mazuri kwao na kuna uwezekano wakawaachia wenzao shughuli hiyo, ili baadaye nao wapate mitaji ya kuanzisha biashara zitakazowasaidia.

Barat anasema, ni namna yenye nafasi kuondokana na uharibifu wa mazao ya misitu, pia wanaachiana fursa ya kupiga hatua.

Mwenyekiti Halmashauri

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Morogoro, Kibena Kingo, anasema halmashauri hiyo imetenga shilingi milioni 26, kwa ajili ya kuwakopesha vijana kuendeleza miradi yao.



Kaimu Katibu Tawala Msaidizi wilaya ya Morogoro, Hilary Sagala, akitoa maelekezo kwa wafugaji wa kikundi cha Bosi Kuku (hawapo pichani), alipotembelea banda lao, kwenye maonyesho ya wazi ya shughuli za mkaa yaliyofanyika katika Kijiji cha Mlilingwa, wilayani Morogoro. **PICHA: CHRITISTINA HAULE.**

Kingo anasema, tayari kuna kitengo maalum kimeshafikisha katika halmashauri vikundi vinavyotambuliwa na sasa, kazi ya ukaguzi unafanyika, kabla ya kuviidhinisha vipatiwe fedha hizo.

"Kwa hawa tumeona leo ni kweli wanafanya (kazi), ukiwapa wataendeleza. Nina uhakika kamati ya fedha itakayokaa mwezi huu itawasikiliza.

"Kwa bahati nzuri leo viongozi wengi tumekiona hiki kikundi kwa hiyo tunalo la kusemea kwenye kikao," anasema Kingo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mlilingwa, Raheli Abdueli, anasema kijiji hicho kimepanga kutumia zaidi ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya shughuli za kijamii na uhifadhi misitu kijijini.

Pia, anasema wameshakusanya shilingi milioni 155 zitokanazo na tozo za leseni 144 za uvunaji mkaa, kijijini humo.

Betty Luwuge, ni Ofisa Mawasiliano wa TTCS, anasema, wamekuwa wakihamasisha wananchi vijijini wanaozalishaji mkaa endelevu, wajiunge na kuendeleza biashara ndogo, ili kupunguza msukumo au mahitaji ya kwenda msituni.

Anasema, biashara au shughuli mbadala wanazoweza kufanya, inasaidia kuendeleza kuhifadhi misitu ya nchi na hizo biashara zinaonyesha kuwa na mafanikio.

Katibu Tawala Moro

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Morogoro, Hilary Sagala, anasema elimu inayotolewa na mradi huo ni nzuri na inapaswa kuwa endelevu kwa vizazi vijavyo, kuwawezeshwa walioko shuleni warithi.

Anasema sekta ya misitu ni muhimu sana katika kuleta maendeleo na kunufaisha sekta zingine na kwamba elimu nzuri ikizidi kutolewa, itasaidia jamii ikiwamo vijana kupata ajira tosha kupitia uhifadhi endelevu wa misitu.

Sagala anasema, misitu inayosimamiwa vyema na kuwa endelevu italeta mchango katika sekta zinazotegemea mifumo ya ikolojia ya misitu ya asili, kama vile kilimo, maji na nishati na maendeleo ya kisasa ambayo serikali inategemea.

Hivyo, anawahimiza wajumbe kujitoa katika kuhifadhi misitu ya asili iliyopo kwenye ardhi za vijiji kwa kuwa ndipo takwimu zinaonyesha kutoweka kwa misitu kwa kiwango kikubwa kutokana na shughuli za kibinadamu.

"Nimeelezwa kuwa dhana ya mkaa endelevu ni chanzo kimojawapo cha uhifadhi misitu, ambayo hutumia eneo dogo la msitu," anasema.

**Meneja Mradi**

Meneja wa mradi huo, Charles Leonard, anasema mradi wake umekuwa muhimu kimkoa, hususan wilayani Morogoro, inakohakikisha wananchi wake wanapata maendeleo kutokana na rasilimali miti zinazowazunguka.

Anataja mifano ya mafanikio, ni madarasa ya shule za msingi yaliyojengwa kwa fedha hizo na wananchi kuingizwa kwenye huduma ya bima ya afya.

Pia, shughuli mbalimbali za maendeleo yote kwao zinafanyika kutokana na mapato kupitia uvunaji endelevu wa rasilimali miti kwa ajili ya mkaa endelevu na mbao.

Anasema, mradi unalenga kuhifadhi rasilimali miti kwa njia endelevu zinazonufaisha wananchi kupata faida za moja kwa moja, wanaboresha maisha yao, huku wakipunguza uharibifu wa misitu unaoendelea nchini.

"Nchini tuna takribani hekta milioni 48.1 za misitu na zaidi ya asilimia 90 ni misitu ya miombo, wakati kwenye hekta hizo milioni 48.1 zaidi ya nusu zipo katika ardhi za vijiji.

"Nchi hupoteza misitu hekta zaidi ya laki 4 na misitu hiyo hupotea katika ardhi za vijiji, hivyo sote tuna jukumu la kuangalia namna gani tunapunguza uharibifu wa misitu katika ardhi za vijiji," anasema Leonard na kuongeza:

"Pili, namna gani rasilimali misitu zitawanufaisha ili waweze kuona rasilimali hizo ni mali yao kwa kupata faida ya moja kwa moja kama vile kupata bima za afya na shughuli za maendeleo mahali walipo."

Anasema, mradi huo unatekelezwa katika vijiji 30, kati yake 20 Wilaya ya Kilosa; na vitano kwa kila wilaya za Mvomero na Morogoro.

Vijiji vilivyoko Morogoro, ni Mlilingwa, Matuli, Lulongwe, Tununguo na Diguzi, ambavyo vyote vimeshawezeshwa kwenye Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi na kunatolewa mafunzo kwa wazalishaji mkaa na mbao.

Ni mradi unaotekelezwa na Shirika la Kuhifadi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) kwa kushirikiana na mtandao wa jamii wa usimamizi wa misitu Tanzania (Mjumita) na Shirika la Kuendeleza Nishati ya Asili Tanzania (TaTEDO), mfadhili mkuu akiwa Shirika la Maendeleo la Ushirikiano la Uswis (FDC), kuanzia Machi 2012.

## BIASHARA KATIKA PICHA




Meneja wa Mawasiliano na Matukio wa Vodacom Tanzania (PLC), Christina Murimi (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya shilingi 500,000/- mmoja ya washindi kupitia kampeni ya Vodacom M-Pesa Tuzo Points, Christian Myamba, fundi cherehani na mkazi wa Sinza, Dar es Salaam. Kupitia kampeni hii wateja 140 wa Vodacom walizawadiwa shilingi 25,000/-kila mmoja na baada ya kampeni kumalizika wateja 10 wa Vodacom nchi nzima watazawadiwa shilingi 500,000/- kila mmoja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Kinamama wakisubiri wateja wa uji na chai katika stedi ya mabasi ya Mawasiliano jijini, Dares Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mchuuzi wa matunda akiwahudumia wateja katika Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. Bakuli moja la matunda aliuza kwa bei ya 1,000/-. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

**BEI YA MAZAO >>** MAHINDI 52,200/-| MAHARAGE 175,208/-

UCHUMI

# Siku Iringa walipotafakari namna wanavyoukalia uchumi wa maziwa

- RC aahidi kushikia 'bango' iwezekane
- Nchini kunanywewa robo ya mahitaji
- Alalama soko lipo, wauzaji wasuasua



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitazama ukamuaji ng'ombe wa maziwa katika shamba la ng'ombe la Asas, nje kidogo ya Mji wa Iringa, mwaka juzi.
**PICHA: MTANDAO**

**Na George Tarimo, Iringa**

HIVI karibuni, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alikutana na jumuiya ya wafugaji kutoka mikoa ya Iringa na Njombe, kujadili maendeleo ya sekta hiyo kwa ukanda uliopo hapo.

Katika kauli yake ya ufunguzi wa mkutano, Hapi anawataka wafugaji wa ng'ombe wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, watumie fursa za uwapo wa soko la uhakika la maziwa nchini, kuzalisha kwa wingi bidhaa hiyo, ili wafaidika na soko hilo.

Anasema, fursa mojawapo ni kipindi kilichopo serikali imeongeza kodi kwenye bidhaa za maziwa yanayoingia nchini, kutoka nje.

Ni mkutano uliolenga kuwajengea uwezo wafugaji na wadau wa sekta ya maziwa, ambao ni wafugaji wadogo, hapo akiwataka wafuge katika njia za kisasa, kwa kuwa mkoa Iringa umetenga maeneo maalumu ya wawekezaji wa mifugo.

Hapi anafafanua kuwa, wilaya zote za Iringa, Iringa Vijijini, Kilolo na Mufundi, zimetenga maeneo ya kutosha za kuendeshea ufugaji.

"Tuwaite wawekezaji waje kuwekeza katika sekta ya mifugo Iringa. Inayo hali ya hewa nzuri, ardhi nzuri, sasa nimewatengea maeneo zaidi ya hekta 100,000. Changamkieni hii fursa kwa ajili ya kuinua kipato chenu na taifa letu," anasema Hapi.

> **"Iringa Vijijini ina ng'ombe zaidi ya 150,000, lakini asilimia kubwa ni ng'ombe wa kienyeji na sio kwamba nachukia ng'ombe wa kienyeji, hapana.**

**Atafuta mikopo**

Anaahidi kuongea na uongozi wa shamba la mifugo la Saohill, lililopo wilayani Mafinga kwa lengo la kuwakopesha vijana na watu walio tayari kwa ufugaji wa kisasa mitamba wenye mimba, ili warejeshe mikopo hiyo taratibu .

"Tanzania kuna fursa nyingi sana lakini bado watu wake wamelala hawajaweza kuchangamkia fursa ya kufuga kisasa kwa sababu kiwanda cha Asas pekee kinahitaji maziwa lita 50,000 kwa siku, lakini kinapata lita 25,000 kwa siku," anasema. "Wafugaji wote wa Iringa, sisi kama serikali tunataka mfuge kisasa, ng'ombe wachache, lakini kwa faida iwe kubwa." anasema Hapi na kuongeza kuwa bidhaa za maziwa, ni kichocheo kikubwa cha ukuaji uchumi.

"Iringa ina fursa nyingi sana katika tasnia ya sekta ya maziwa, kutokana na kuwapo kiwanda kikubwa cha kusindika maziwa, kinachotoa fursa ya soko, ajira na uhakika wa maziwa ghafi kwa wafugaji ng'ombe kwa mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya," anasema.

**Mahitaji yaliyopo**

Hapi anasema, kiwanda hicho kinatoa fursa nyingi za ajira kupitia uuzaji maziwa katika sehemu nchini na anaeleza kila siku Iringa inachangia lita 10,000 za maziwa, huku mikoa jirani Njombe na Mbeya, inachangia lita 12,000; zote ni nusu ya mahitaji.

Anataja changamoto zilizopo ni unywaji mdogo wa maziwa, uuzwaji holela, ukosefu wa mbegu bora za malisho, ukosefu wa mitaji na huduma za mikopo.

Mkuu wa Mkoa anasema, Tanzania kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa, kila mwananchi anapaswa kunywa lita zisizopungua 200 kwa mwaka, lakini wastani wa taifa la Tanzania kila mtu anakunywa lita 47 pekee.

Hapi analaumu kiwango hicho kidogo, akilinganisha na nchi jirani ya Kenya, wastani wa unywaji wa kila mtu ni lita 100 kwa mwaka.

Anasema Tanzania kuna wa kisasa milioni 1.5 wanaotoa wastani wa lita bilioni 2.4, lakini sehemu kubwa ya maziwa hayo yanayozalishwa na viwanda vya ndani hayanyweki zaidi.

Mkuu wa Mkoa huyo anasema, sababu mojawapo iliyoifanya serikali kuongeza kodi kwa maziwa ya viwanda vya nje ni kuvilinda vya ndani.

Mkutano huo uliofanyika katika viwanja vya Kichangani Manispaa ya Iringa, uliwakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo, Shirika la Viwango la Taifa (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

**Akemea wanaosuasua**

"Maofisa mifugo tokeni ofisini, nendeni kwa wananchi mkawashauri jinsi gani wanafuga kisasa, ili waweze kuondokana na kufuga kienyeji. Sisi lengo letu tuone kila mwananchi anafuga kisasa na apate maziwa mengi na ya kutosha," anasema Hapi.

Anaeleza mshangao wake kwa wafugaji wanaohangaika, kuwekeza nguvu zao katika kilimo cha ulanzi, kinywaji kinachopendwa sana mkoani Iringa.

"Acheni na kuhangaika na vitindi vya ulanzi. Hangaikeni na kufuga ng'ombe wa kisasa, huko kuna pesa, watu wa mjini wanasema 'mshiko nje nje.' Kikienda kufyekwa, unapiga kelele, hakuna aliyetajirika kwa kuuza ulanzi," anasisitiza Hapi.

**DC Kasesela**

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, anawataka wafugaji kujiunga kwenye vyama vya ushirika, ili waweze kuuza maziwa kwa pamoja, katika soko lao kuu la mkoa ambalo lina uhakika.

Anasema wilaya yake ya Iringa ina changamoto ya wafugaji wengi wana ng'ombe wengi wa kienyeji, wasio na tija na faida wanayopata ni ndogo.

"Iringa Vijijini ina ng'ombe zaidi ya 150,000, lakini asilimia kubwa ni ng'ombe wa kienyeji na sio kwamba nachukia ng'ombe wa kienyeji, hapana.

"Ni kwa sababu wanafugwa kienyeji, mfano unakuta ng'ombe mmoja anatoa lita mbili au au tatu, lakini hawa wa kisasa anatoa zaidi ya lita 10 hadi 20 kwa siku," anasema Kasesela, ambaye kitaaluma ni mchumi na biashara.

**Mwenye kiwanda**

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Kusindika Maziwa, Fuad Asas, anatoa ufafanuzi: "Wafugaji hawa hawatakuwa wafanyabiashara kama hawaijui biashara. Wadau wote wa maziwa wanakutana na wafanyabiashara wadogo (wafugaji) ili kutambua fursa."

Fuad anasema, Iringa imeweza kuwa kitovu cha kusini mwa Tanzania na anaomba kuwapo maonyesho ya kitaifa kwa sababu fursa ya maziwa ni kubwa, sio kwa mfugaji pekee, bali mnyonyoro mzima kuanzia muuza mbolea hadi mlaji wa mwisho.

INAENDELEA UK. 20

**FEDHA >> USD 2,300.89| Pauni 3,027.97| Euro 2,613.12**

BIASHARA

# Unayajua mauzo ya moja kwa moja?

## •Ujue ushiriki wa Afrika Mashariki

Na Mwandishi Wetu

MAUZO ya moja kwa moja yanakua kwa kasi katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwamo ukanda wa Afrika Mashariki, jambo linalosababishwa na ongezeko la idadi ya watu.

Mauzo ya moja kwa moja, ni wazo la biashara ya kimataifa na linaelezewa kama uuzaji bidhaa za matumizi au huduma, kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mtu mwingine, mbali na maeneo ya maduka ya kawaida.

Taarifa ya Uchambuzi wa Ongezeko la Vijana ya Taasisi ya Maendeleo ya Afrika, inaeleza kuwa katika Afrika Mashariki, kuna wakazi zaidi ya asilimia 45; kati yao vijana wako milioni 150. Hao ni katika nchi za Kenya, Tanzania, Rwanda na Uganda.

Kupitia ripoti ya uchambuzi huo, vijana wengi wanaelezwa hawana elimu, ila kwa ujumla wana ufahamu wa teknolojia, wepesi kufuata mienendo mipya, wana hamasa ya kuweka juhudi na fikra za ujasiriamali.

Mtindo huo wa mauzo, unaelezwa una zaidi ya karne moja nchini Marekani, na takribani watu milioni 117 wanajihusisha nayo.

Katika kanda ambayo mahitaji ya ajira rasmi yanazidi kuwa na ushindani mkubwa na uhaba wa ajira rasmi, mauzo ya moja kwa moja yanatoa njia mbadala za ajira, tofauti na ilivyozoeleka kwa wale wanaohitaji kipato cha ziada au mazingira hayaruhusu ajira.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mauzo ya Moja kwa Moja, Kanda ya Kusini mwa Jangwa la Sahara, Biram Fall, anasema hiyo imesaidia kuwawezesha maelfu ya watu Afrika, wakiwamo vijana katika muongo uliopita.

"Tunaona ongezeko la kukubalika kwa mauzo ya moja kwa moja na idadi ya watu zaidi ya milioni 200 katika Afrika Mashariki, utaratibu huu unabadilisha maisha ya wengi," anasema.

**Bidhaa zake**

Anataja bidhaa zinazotolewa ni; afya, ustawi na mitindo ya maisha kupitia mifumo yake ya biashara ya mitandao kwa mamilioni ya wateja katika nchi 100 katika kusaidia watu kuishi maisha bora.

Pia Fall anataja manufaa mengine ni kutolewa njia mbadala ya kujipatia kipato kwa mhitaji wa fursa hiyo na anasema kampuni yake, imejitandaza kimataifa, ikiwa na ofisi na wakala washirika katika nchi 25 duniani kote.

Mbali na hiyo, meneja anasema kuna jumla ya maghala 50, sambamba na shughuli lukuki za uendeshaji maduka na wauzaji katika nchi mbalimbali duniani.

"Sasa kwa uwepo wake imara katika Afrika Mashariki, QNET imejizatiti katika kuendeleza mtindo wa mauzo wa moja kwa moja katika kanda hii," anasema Fall.



Eneo la Kariakoo katikati ya Dar es Salaam, ambako ni kitovu cha biashara.

> **Tofauti na biashara nyingine za kawaida ambazo zinahitaji mtaji mkubwa, rasilimali na hata uzoefu, biashara ya mauzo ya moja kwa moja inatoa fursa hii ya biashara...**

**Inafaidikaje?**

Fall anataja manufaa ya aina hiyo ya biashara kupitia uzoefu wake, akisema wamefanikiwa kuwezesha mauzo ya moja kwa moja kwa wajasiriamali, ambao wameamua kujitika kwenye biashara hiyo moja kwa moja.

"Tofauti na biashara nyingine za kawaida ambazo zinahitaji mtaji mkubwa, rasilimali na hata uzoefu, biashara ya mauzo ya moja kwa moja inatoa fursa hii ya biashara yenye gharama nafuu kwa kila mmoja anayehitaji kuianzisha, bila ya kujali kiwango chao cha elimu au uzoefu," anasema.

Kingine anachokitaja kuwa manufaa ya biashara ya moja kwa moja, ni kwamba mafunzo na maelekezo ambayo wafanyabiashara wanapatiwa ujuzi wa pekee, unaowapa ujasiri na kujitambua.

Fall, anafafanua ukuaji binafsi kikazi, hautambui utaalamu wa mtu kama mjasiriamali aliyekamilika.

**Changamoto**

Fall anasema, kama ilivyo biashara nyingine yoyote sekta ya mauzo ya moja kwa moja, pia inakabiliana na changamoto, ikiwamo matapeli wanatengeneza taswira potofu ya sekta ya mauzo ya moja kwa moja.

"Wakati tunakabiliana na changamoto hizi, QNET inatatua tatizo kwa kuelimisha umma kuwa makini na matapeli kama hao na kuwahimiza kuthibitisha uhalali wa kampuni yoyote, kufuatana na kutii kwake kwa kanuni, taratibu na sheria zilizowekwa na bodi zinazosimamia na mamlaka zinazohusika," anasema.

Fall anasema, wanakabiliana na changamoto ya kufikisha bidhaa katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mbali, ambapo ni kikwazo kingine, lakini imeweza kutatua hili kwa kuajiri wataalamu wa kufikia lengo hilo.

**Sura ya ushindani**

Fall anasema ukiachilia mbali mtindo wake wa kipekee wa usambazaji, mpango za mafunzo za kipekee zitakuwa tofauti na wengine.

Anasema, kwa sababu mafunzo yameandaliwa maalumu katika kumfundisha mkufunzi yatahamasisha ushiriki katika mafunzo haya kwa timu zao.

"Cha muhimu zaidi tunatoa mafunzo katika misingi ya maadili na kufanya masoko kitaalamu ambacho ni kiungo muhimu sana kinachokuza uadilifu miongoni mwa timu za mauzo," anasema.

Anataja wanatoa mafunzo ya bidhaa, semina kwa njia ya mtandao, utaratibu wa namna ya utendaji na mipango ya vitendo ikiwamo maonyesho ya bidhaa.

Fall anasema, mtindo huo na programu zake za mafunzo zinazotolewa zimetumika kwa mafanikio ya kupigiwa mfano katika maeneo mengine ya Afrika, hasa Afrika ya Magharibi, ambako kampuni ina uendeshaji imara wa shughuli zake.

Anasema mtindo huo unakuwa kwa kasi, kwa mafanikio kama hayo Afrika ya Mashariki.



Makontena yakipakuliwa katika Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**


# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Machi 11, 2019

| Mkoa | Arusha | DSM | Dodoma | Geita | Kagera | K'njaro | Kigoma | Manyara | Mbeya | Mwanza |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 44,000 | 70,000 | 47,000 | 57,000 | 60,000 | 45,000 | 54,000 | 51,000 | 40,000 | 62,000 |
| Mchele | 200,000 | 230,000 | 180,000 | 130,000 | 185,000 | 180,000 | 180,000 | 200,000 | 150,000 | 180,000 |
| Mtama | 35,000 | 60,000 | 35,000 | 180,000 | 100,000 | 80,000 | 80,000 | 42,000 | 105,000 | NA |
| Uwele | 35,000 | 70,000 | 35,000 | 180,000 | 110,000 | NA | 60,000 | 100,000 | NA | 150,000 |
| Ulezi | 72,000 | 140,000 | 75,000 | NA | 150,000 | 180,000 | 150,000 | 120,000 | 120,000 | 160,000 |
| Ngano | 80,000 | 130,000 | 160,000 | 180,000 | NA | 100,000 | 150,000 | 120,000 | 130,000 | NA |
| Maharage | 155,000 | 210,000 | 175,000 | 170,000 | 150,000 | 180,000 | 130,000 | 150,000 | 210,000 | 160,000 |
| Viazi Mviringo | 70,000 | 90,000 | 65,000 | 70,000 | 75,000 | 65,000 | 90,000 | 50,000 | 50,000 | 80,000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Machi 20, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,481.50 | -0.13 |
| DSEI | 2,065.75 | +4.99 |
| Thamani za Hisa (bln) | 19,911.50 | |
| Mauzo | 84,632,700.00 | |
| Hisa | 625,309 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| ACA | 6,000 | -1.64% |
| JHL | 9,250 | -0.54% |
| NICO | 165 | -2.94% |
| USL | 10 | -33.33% |
| EABL | 4,660 | +2.64% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

## Bei za hisa hadi kikao cha Machi 20, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 6,000.00 | 6,100.00 | -1.64 |
| CRDB | 125 | 125.00 | 0 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,300 | 1,300 | 0 |
| EABL | 4,660.00 | 4,540.00 | 2.64 |
| JHL | 9,250.00 | 9,300.00 | -0.54 |
| KA | 115.00 | 115.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,020.00 | 1,020.00 | 0 |
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 165.00 | 170.00 | -2.94 |
| NMB | 2,340.00 | 2,340.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| TICL | 385 | 385.00 | 0 |
| TOL | 660.00 | 660.00 | 0 |
| TPCC | 2,020.00 | 2,020.00 | 0 |
| TTP | 120.00 | 120.00 | 0 |
| USL | 10.00 | 15.00 | -33.33 |
| VODA | 800.00 | 800.00 | 0 |
| YETU | 600.00 | 600.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,256.67 | 2,274.73 |
| UGANDA SHS | 57.83 | 61.97 |
| RWANDAN FRANC | 252.52 | 255.36 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.76 |
| USD | 227,810.89 | 230,089.00 |
| POUND STG | 299,708.01 | 302,797.12 |
| EURO | 258,679.27 | 261,312.08 |
| CANADIAN $ | 170,977.85 | 172,635.80 |
| SWITZ. FRANC | 228,153.12 | 230,365.44 |
| JAPANESE YEN | 2,043.70 | 2,063.95 |
| SWEDISH KRONOR | 24,806.81 | 25,043.97 |
| NORWEG. KRONOR | 26,700.45 | 26,951.66 |
| DANISH KRONOR | 34,671.25 | 35,012.63 |
| AUSTRALIAN $ | 161,631.83 | 163,340.18 |
| INDIAN RPS | 3,311.25 | 3,343.30 |
| PAKISTAN RPS | 1,553.96 | 1,631.84 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,810.07 | 19,110.38 |
| MALAWIAN KWACHA | 291.65 | 310.84 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,621.79 | 3,652.21 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 317,598.00 | 320,773.98 |
| GOLD (T/O) | 297,996,670.12 | 301,034,159.07 |
| S. AFRICAN RAND | 15,798.26 | 15,934.14 |
| UAE DIRHAM | 62,026.49 | 62,634.82 |
| SINGAPORE $ | 168,711.32 | 170,335.36 |
| HONK KONG $ | 29,021.60 | 29,310.33 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,746.33 | 61,350.52 |
| KUWAIT DINAR | 750,488.85 | 757,719.16 |
| BOTSWANA PULA | 21,186.41 | 21,582.35 |
| CHINESE YUAN | 34,031.09 | 34,364.21 |
| MALAYSIA RINGGIT | 56,042.04 | 56,546.82 |
| SOUTH KOREA WON | 201.95 | 203.61 |
| NEWZEALAND | 156,096.02 | 157,749.02 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| 20/Mar/2019 | 3.50 | 2,316.00 | 2,298.75 | 2,300.89 |
| 19/Mar/2019 | 4.00 | 2,315.00 | 2,298.80 | 2,300.87 |
| 18/Mar/2019 | 3.67 | 2,315.00 | 2,298.90 | 2,300.34 |
| 15/Mar/2019 | 4.50 | 2,310.00 | 2,298.90 | 2,300.09 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| 20/Mar/2019 | 66,450 | 6.50 | 5.00 | 5.68 |
| 19/Mar/2019 | 15,650 | 6.50 | 4.00 | 5.70 |
| 19/Mar/2019 | 15,650 | 6.50 | 4.00 | 5.70 |
| 18/Mar/2019 | 31,250 | 6.50 | 5.50 | 5.70 |
| 15/Mar/2019 | 41,250 | 6.50 | 4.50 | 5.49 |
| 14/Mar/2019 | 31,700 | 6.50 | 5.20 | 5.41 |

# Iringa walipotafakari namna wanavyoukalia uchumi wa maziwa



Wanafunzi wa mjini Iringa, wakiwa katika Wiki ya Unywaji Maziwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**INATOKA UK. 18**

**Wananchi**

Flaviana Mbata, ni mkazi wa Njombe, anayesema awali walikumbwa na changamoto ya ubora wa maziwa, jambo analodai yalipofika kiwandani yalikataliwa, lakini baada ya kupata elimu, changamoto imefutika, kwa kuwa wanasafirisha na maziwa kupokewa kiwandani.

Hamza Chorobi, mkazi wa mjini Iringa, anashukuru kiwanda cha maziwa kwa kuwainua, kwa kuwa huko nyuma wengi walifuga kienyeji na kila mmoja alikuwa akifanya peke yake na akauza maziwa mtaani. Chorobi anasema, huko nyuma alimkabidhi mtu binafsi kuuza maziwa yake na akarudishiwa akiambiwa hayauziki kwa sababu hayana ubora.

Anasema alikutana na wenye kiwanda aliyowaelimisha waunde kikundi na kiwanda kiliwakopesha mashine ya kuandaa chakula cha malisho ya ng'ombe, sasa wamepiga hatua katika mradi. "Alituambia mtalipaje hili deni? Tukamjibu tutalipa kwa kukatwa kwenye maziwa tunayoleta kiwandani kwao," anasema Chorobi, aanyekiri mradi kumnufaisha.

Seleman Mroy, mfugaji kutoka Kijiji cha Nzihi, Iringa, anakishukuru kiwanda cha Asas kuwasaidia soko la maziwa, kwa sababu awali walipata adha ya uuzaji maziwa yao waliyoyatafutia soko kienyeji. Mroy anasema changamoto kubwa, ni kukosekana mitamba bora yenye uwezo wa kutoa maziwa mengi na bei kubwa za magari ya kubeba maziwa vijijini.

Ombi lake ni serikali kuwasaidia ruzuku ya kuwaletea unafuu katika maeneo hayo wanayokwazika, kama vile kukosekana mbegu bora za malisho ya ng'ombe.

Mwezeshaji mkutano

Baraka Zebedayo, ni mwezeshaji kutoka asasi ya Global Community, anayesema lengo la mikutano kama hiyo ni kujenga uhusiano kati ya wafanyabiashara na wafugaji.

Zebedayo anasema, mikutano hiyo imefanyika katika sehemu mbalimbali nchini, ikiwamo jijini Tanga ulikowakutanisha wafugaji zaidi ya 600 na baadaye kwenda Iringa. Maeneo hayo yote yana viwanda vya maziwa.

Ofisa Kilimo Mkoa wa Iringa, Grace Macha, anasema uwapo wa wadau hao, unaamsha ari ya uwajibikaji, hasa kwa watendaji wa serikali kuhakikisha mlaji anapata maziwa yaliyo salama.

"Katika ofisi yetu kuna rasilimali ambazo hazitumiki, kila halmashauri kuna mkaguzi wa maziwa ambaye amepata mafunzo, lakini hawafanyi kazi zile kutokana na kukosekana kwa vifaa pamoja na kubadilika kwa teknolojia," anasema Macha.

Lieita Mtimila, ni Mratibu wa Maziwa Kiwanda cha Asas, anayesema wao wanapenda kuwa na vituo vya kukusanya maziwa maeneo mengi, lakini tatizo kubwa ni ubovu wa miundombinu ya barabara na umeme.

Anasema kuwa kiwanda cha Asas kimefanikiwa kuwawezesha wafugaji 4,000 na wananchi 30,000 kunufaika nao, kutokana na uuzaji wa maziwa.

- ***Mwandishi wa Makala hii anapatikana kwa barua pepe: georgetarimo5040759@gmail.com***



## HABARI MBEYA

# Viongozi wa mila waitwa mpango kupanga upya jiji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imeanza kutoe elimu kwa wananchi kuhusu harakati za kuupanga upya mji huo ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima, wakati utekelezaji utakapoanza hasa kwenye upimaji wa maeneo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, James Kasusura, alipofanya kikao na viongozi wa mila wa jiji hilo kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa mradi wa upangaji upya wa mji huo kikao ambacho kilifanyika katika ofisi za jiji.

Kasusura alisema kwa sasa tayari wameshaanza kutoa elimu hiyo kwenye maeneo ambayo mradi wa upimaji utaanzia ambayo ni Iziwa, Iduda na Mwansekwa na kwamba wataendelea katika maeneo mengine yaliyobaki.

Alisema lengo la upimaji huo ni kuepuka ujenzi holela kwenye maeneo hayo ambayo yana makazi machache na kwamba kila mtu ambaye kipande chake cha ardhi kitapimwa atalipwa fidia.

Kasusura alisisitiza kuwa tayari serikali imeshatoa fedha kwa ajili ya fidia hizo na kwamba zingine zitaendelea kuletwa ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa asilimia 100 ili jiji hilo liwe na mwonekano unaoendana na hadhi yake. Kasusura alisisitiza kuwa upimaji wa miji hapa nchini ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2015 na hivyo lazima utekelezwe kwa nidhamu ya hali ya juu na akaeleza kuwa hakuna ujanja ujanja utakaotokea kwenye mradi huo. "Kwenye suala la fidia hilo halina ubishi, serikali imeshatupatia fedha za kutosha na zingine tutaletewa wiki hii, kila ambaye eneo lake litapimwa atalipwa fidia stahiki kwa mujibu wa sheria na naomba niweke wazi kuwa ujanja ujanja kwenye serikali hii haupo," alisema Kasusura na kuongeza.

"Ukisoma ibara ya 37 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, imeeleza kwamba miji yote ya mikoa, majiji na maeneo yote muhimu, yapimwe ili kupanga miji yetu na kuongeza thamani ya ardhi, kumbuka ilani ni mkataba kati ya rais na wananchi wake," aliongeza. Mwenyekiti wa machifu wa Mkoa wa Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga, alisema wazo la serikali la kupanga upya mji huo ni zuri na litasaidia kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisema yeye binafsi yuko tayari kushirikiana na serikali kutoa elimu kwa wananchi ili waupokee mradi huo, huku akieleza kuwa kitendo cha watu kulipwa fidia kitasaidia kuondoa migogoro isiyokuwa na maana kati ya wananchi na serikali.

Chifu Mwashinga alisema Jiji la Mbeya likipangwa vizuri litakuwa linawavutia hata watu wa maeneo mengine kwenda kutembelea na hata kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo.

"Elimu inaanza kutolewa na serikali na sisi tutakuwa nyuma yake, ikishamaliza ndio sisi tunaingia kusawazisha kwa wananchi wetu kwa kuwambia umuhimu wa maendeleo na hakutakuwa na tatizo lolote na naamini hakuna atakayepinga maendeleo," alisema Chifu Mwashinga.

Aliwataka wananchi wa jiji hilo kuwa tayari kuupokea mradi huo, huku akiipongeza serikali kwa kuutambua mchango wao na kuamua kuwaalika na kufanya mazungumzo nao.



Meneja wa Tanroad Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Narcis Choma, akizungumza na wananchi baada ya kukagua Barabara ya Lumumba eneo la Mwanga, Manispaa ya Kigoma/Ujiji. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Hanga na kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Emmanuel Maganga. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Wajikomboa kwa kupata mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

WAKAZI wa Kijiji cha Goye katika kata ya Ndato, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji baada ya kuchangishana na kujenga mradi wa maji uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 180.

Wananchi hao wanadaiwa kuwa hawakuwa na huduma ya majisafi kwa muda wa miaka 15 tangu kijiji hicho kilipoanzishwa mwaka 2004 hali iliyowalazimu kutumia maji ambayo usalama wake ulikuwa sio wa uhakika.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Zawadi Moses, alisema kijiji hicho kina jumla ya wananchi 3,637 na kwamba walikubaliana kuweka kando tofauti za itikadi za siasa na wakakubaliana kutatua changamoto hiyo ambayo ilikuwa haibagui.

Alisema wananchi hao walikuwa wanatumia maji ya visima vya kienyeji ambavyo walikuwa wanachangia na mifugo pamoja na wanyama wengine wa porini hali ambayo ilikuwa inahatarisha afya zao.

"Tulimshirikisha diwani ili atuletee wahandisi wa maji kutoka halmashauri kwa ajili ya ushauri, bahati nzuri wahandisi walionyesha ushirikiano mpaka tumefikia hatua hii, lakini nguvu kubwa ni ya wananchi ambao walikuwa wanachangishana," alisema Moses.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maji ya kijiji hicho, Obed Mwambatata, alisema wananchi walianza kuchimba mitaro ya kupitisha mabomba kutoka Mto Isinini uliopo umbali wa kilomita sita kutoka kijijini hapo mwezi Novemba 2018.

Alisema Januari walianza kujenga tangi lenye ujazo wa lita 90,000 ambao umekamilika mwezi Machi, mwaka huu na kuanza kutumika rasmi na wananchi wa kijiji hicho.

Mwambatata alisema fedha za kukamilisha mradi huo zimetokana na kodi za makusanyo ya mazao, kukodisha mashamba ya kijiji pamoja na michango ya wananchi, ambapo kila kaya ilikuwa inachangia shilingi 20,000.

"Mpaka mradi huu unafikia hatua hii hakuna fedha iliyotolewa na serikali wala wadau, zote ni juhudi za wananchi ambao walikuwa wanaacha shughuli zao za kila siku kuhakikisha mradi huu unakamilika maana walikuwa wamechoka," alisema Mwambatata.

Mwambatata kwa sasa wanahitaji kupata shilingi milioni 20 kwa ajili ya kununua mabomba ya kusambazia maji kwenye vituo, hivyo akaiomba serikali iwaunge mkono.

Diwani wa kata ya Ndato, Paulos Zambi (Chadema), alisema kata hiyo imeshindwa kupata miradi ya maendeleo kutokana na kutengwa na serikali kwa madai kuwa inaongozwa na upinzani.

Aliwapongeza wananchi wa Kijiji cha Goye kwa kujitambua bila kujali itikadi zao za vyama mpaka hatua ya kubuni miradi ya maendeleo kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe.

Alisema mbali na mradi huo pia wananchi hao waliungana na wananchi wengine wa kata hiyo kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa vinne katika Shule ya Sekondari ya Goye ambayo yaligharimu shilingi milioni 100, huku milioni tatu pekee zikitolewa na Halmashauri ya Rungwe.

## Vilainishi visivyokidhi viwango chanzo ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa baadhi ya ajali za barabarani zinazotokea nchini zinasababishwa na matumizi ya vilainishi visivyokidhi viwango kwenye vyombo vya moto hasa mafuta ya breki.

Hayo yalisemwa juzi na Mkaguzi Ubora wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Yekonia Sanga, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi walipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka yanayouza vilainishi jijini Mbeya. Katika ukaguzi huo walikamata shehena ya vilainishi vya breki za magari vya viwango vya DOT 3, vilivyopigwa marufuku kuuzwa vikiendelea kuwa sokoni, wakaondoka navyo kwa ajili ya kwenda kuviteketeza.

Alisema vilainishi hivyo vimepigwa marufuku visitumike nchini kwa sababu havikidhi viwango na ni hatari kwa waendesha vyombo vya moto kwa maelezo kuwa vinasababisha breki za magari kukatika na kusababisha ajali.

"Vilainishi vya aina hii nguvu yake ni ndogo kwa sababu vinapata moto haraka na vikishachemka vinaaza kutoa mvuke ambao unabadilika na kuwa maji ambayo yanarudi tena na kuchanganyika na mafuta, baada ya hapo kila dereva akishika breki anakuta hazishiki na ndio hapo tunashuhudia ajali," alisema Mhandisi Sanga. Alisema mbali na kusababisha ajali pia vilainishi vya aina hiyo vinaharibu vyombo vya moto na kuwaingiza hasara wamiliki wa vyombo hivyo.


Kwa upande wake Ofisa Uhusiano wa TBS, Roida Andusamile, aliwataka wafanyabiashara wa vilainishi kuacha kuwauzia wananchi vilainishi hivyo ili kuwaepusha na matatizo ya ajali na vyombo vya kuharibika mara kwa mara.

Alisema wataendelea na ukaguzi nchi nzima na kwamba wakivikuta dukani wanavichukua na kwenda kuviteketeza pamoja na kuwatoza faini wahusika na gharama za kuteketezea. Alisema mbali na kukamata na kuondoka na vilainishi hivyo, pia wataendelea kutoa elimu kwa wananchi kuepuka kutumia vilainishi hivyo na kuwaelimisha wafanyabiashara ili waache kuuza vitu ambavyo vitawasababishia hasara.

"Tumetoa sana elimu kupitia vyombo vya habari na kwa kuwaelimisha wafanyabiashara, wote wanajuwa kuwa ni kosa kuuza vilainishi hivi, lakini baadhi wanaendelea, sisi tutaendelea kutoa elimu lakini tukivikuta lazima tutoe tena elimu na mhusika lazima achukuliwe hatua," alisema Roida.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaouza vilainishi vyenye viwango, walisema soko la vilainishi vyao ni dogo kutokana na vsivyokidhi viwango kuzagaa mitaani na kuuzwa kwa bei ya chini.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Peter Chacha, alisema vilainishi vinavyoruhusiwa vinauzwa kuanzia Sh. 15,000, lakini vile visivyokidhi viwango vinauzwa mtaani Sh. 5000, hivyo watu wengi wanakimbilia kununua hivyo bila kujua madhara yake.





# CCM waanza kupasha 'misuli' uchaguzi ujao serikali za mitaa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), Dk. Bashir Ali, kesho anatarajiwa kuzindua mkakati wa kukomaza demokrasia kwenye mashina mkoani Dodoma ikiwa ni maandalizi kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu 2020.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapo, Katibu wa CCM mkoani hapa, Jamila Yusuf, alisema kuwa wana Dodoma wanawajibu wa kukomaza demokrasia mashina kisiasa, kimuundo na kiuchumi.

"Kwa mkakati huu tunategemea kufikia malengo yafuatayo, moja kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi ujao wa dola kwa maana uchaguzi mkuu 2020 na uchaguzi wa serikali za mitaa 2019," alisema.

Alibainisha kuwa wanalenga kuongeza uwajibikaji wa viongozi na wanachama ili kukifanya chama kiendelee kushika dola."Katika hili Watanzania wasikie na dunia ijue wana Dodoma wameamua kuweka mkakati huu ambao utawezesha viongozi kujenga uhusiano mzuri baina ya viongozi wa chama na serikali sambamba na viongozi wengine kama taasisi za kidini, wazee maarufu wa kimila na makundi mbalimbali katika maeneo yetu," alisema.

Katibu huyo alisema mkakati huo utaongeza kiwango cha ushiriki wa wanachama katika shughuli za maendeleo ulinzi na usalama.

"Kupitia mkakati huu tunategemea kuwezesha ofisi za mashina na matawi kujiimarisha kiuchumi ili kutatua changamoto ambazo zipo katika maeneo yao," alisema.

Aidha, alisema kupitia mkakati huo utatoa msukumo wa ujenzi na ukarabati wa ofisi za chama hasa ngazi ya mashina na matawi.

Yusuf alisema katika uzinduzi huo watagawa vitendea kazi vya chama ambavyo vitawawezesha viongozi wa chama kuanzia ngazi za mashina matawi hadi kata kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Alisema kwa kuwa Dodoma ni ngome imara ya CCM watahakikisha wanailinda kwa nguvu zote hasa kipindi hiki ambacho serikali imehamia Dodoma.

"Sisi tunajua watafika watu kila mmoja atakuja na aina yake ya tabia yake na itikadi yake, lakini sisi kama Dodoma tunajua tunao wajibu wa kuendelea kulinda itikadi yetu ya CCM," alisema.

Katibu huyo alisema vifaa hivyo vitagawanywa kwenye mashina 12,510 na matawi 1234.



Mkuu wa Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, Sezaria Makota (aliyesimama), akizungumza na wananchi katika moja ya mikutano yake jana wilayani hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Profesa Mbarawa atoa agizo kwa Ewura

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeagizwa kufanya mapitio ya bei za dawa za kutibu maji na kuishauri serikali ili kuweka gharama nafuu.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Maji Profesa Makame Mbarawa, wakati akizindua ripoti za utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/18, ambazo zinahudumia miji mikuu ya mikoa na miradi ya kitaifa kwa mwaka huo wa fedha.

Profesa Mbarawa alisema bei za kutunzia maji kwa sasa gharama zake ni kubwa, hivyo kuna haja ya mamlaka hiyo kufanya mapitio.

Aliitaka kuwasiliana na Bohari ya Dawa nchini (MSD) kwa kuwa wanaweza kuwa na gharama ndogo kuliko zinazotozwa na watu binafsi ili waishauri serikali.

"Pitieni mtushauri sisi serikali sehemu nzuri ya kununua ambayo inagharama nafuu ingawa mamlaka za maji haziwezi kufurahia kwa kuwa wanamaslahi nako," alisema.

Kuhusu utendaji wa mamlaka za maji, Profesa Mbarawa alisema zimekuwa zikisuasua kutokana na kutokuwa na elimu ya uendeshaji, hivyo watumie muda wao kuwapa elimu na semina kwa viongozi wa taasisi.

Kadhalika, alizitaka mamlaka za maji kuhakikisha wananchi waishio maeneo ya vijijini wanapata maji kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo mizuri inayosimamia sekta hiyo.

Alisema, kazi ya mdhibiti ni kudhibiti na kuweka mazingira mazuri ili sekta ikue na si vinginevyo, suala la upatikanaji wa maji litakuwa lina changamoto na kwamba suala la kuzalisha maji mengi ni tofauti na suala la usambazaji maana kunaweza kuwa na uzalishaji mkubwa wa maji, lakini usambazaji kwa wananchi ukakosekana.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Ewura, Nzinyagwa Mchany, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikiandaa utendaji wa mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini ili pamoja na mambo mengine kutathimini utendaji wa mamlaka hizo, pia kukidhi matakwa ya Kifungu cha (2) cha Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009.

# Upatikanaji wa 'pedi' waleta neema kwa wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** BAHI

UPATIKANAJI wa taulo laini za kike (Pedi), pamoja na uwepo wa vyumba vya kujihifadhia kwa watoto wa kike katika shule za msingi wilayani Bahi mkoani Dodoma, kumesaidia kuongeza mahudhurio ya wanafunzi shuleni.

Akizungumza na waandishi wa habari Mwalimu wa Shule ya Msingi Mundemu wilayani hapo, Zahiya Mbuva, alisema wanafunzi wengi wa kike wilayani humo walikuwa wanakosa masomo kila mwezi kwa zaidi ya siku saba kutokana na kuingia katika siku zao za hedhi hivyo kukosa baadhi ya vipindi.

Alisema kuwa upatikanaji wa taulo laini kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika shule yake kumechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mahudhurio kwa watoto wa kike.

Alibainisha kupitia mradi wa Usafi wa Mazingira (UMATA) unaotekelezwa na Shirika la Plan International wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike wakati wanapokuwa katika hedhi zao.

Alisema kuwa pamoja na mafunzo hayo pia wamepatiwa vifaa kwa ajili ya kutengeneza pedi kwa watoto wa kike ambazo wamekuwa wakizitumia kwa hivi sasa.


"Awali utoro kwa watoto wa kike ulikuwa mkubwa sana, wanafunzi wa kike walikuwa wakitoroka vipindi kila wanapoingia katika hedhi, lakini toka kuanza kwa huu mradi mambo yamebadilika wanafunzi wanajieleza kwa walimu wao na kupatiwa msaada," alisema.

Alisema kutokana na uwepo wa chumba cha kujihifadhia kwa wanafunzi wa kike ambacho kimejengwa maalum kimekuwa msaada mkubwa kwao.

"Hivi sasa badala ya mtoto kukimbilia nyumbani, anachokifanya hivi sasa ni kwenda katika chumba cha kujihifadhia ambacho kinakuwa na vifaa vyote kama pedi pamoja na maji na baadaye kurudi darasani kuendelea na masomo kama kawaida," alisema. Naye mwanafunzi wa darasa la saba Paulina Majengo, alisema kuwa hivi sasa wamepatiwa mafunzo ya kujihudumia wakati wanapokuwa katika kipindi cha hedhi.

Aliongeza kuwa pamoja na mafunzo hayo pia wamejifunza namna ya kutengeneza pedi za asili ambazo wanazitumia pamoja na wanafunzi wenzake.

"Zamani tulikuwa tunatoroka na kurudi nyumbani, lakini hivi sasa yupo mwalimu ambayo anatusaidia kila tunapokuwa katika hedhi," alisema Majengo.







Mchuuzi wa viatu akiweka bidhaa zake vizuri katika Mtaa wa Narung'ombe Kariakoo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Zanzibar yapigia chapuo takataka kuzalisha mbolea

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR ni miongoni mwa maeneo yenye nafasi ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya mboga iwapo taka zinazozalishwa zitahifadhiwa na kutumika vizuri kama mbolea.

Hayo yalielezwa na msimamizi wa mradi wa kusarifu taka na kuwa mbolea, Dk. Muhammed Kombo Maalim, wakati alipozungumza na waandishi wa habari walioshiriki mafunzo ya uandishi wa habari wa sayansi na teknolojia yaliyoandaliwa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), mjini Zanzibar.

Alisema kuwa Zanzibar inazalisha tani 300 za taka kwa siku, lakini kunakosekana kwa ubunifu wa kuzifanya taka hizo kuwa na faida kwa matumizi mbalimbali bila ya kuleta athari.

Alieleza kuwa kutokana na kiwango hicho kikubwa ambacho Zanzibar inazalisha, Taasisi ya Sayansi ya Bahari kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), imebuni njia bora ya kuzisanifu taka hizo na kuwa mbolea.

Alieleza kuwa mbolea hiyo itokanayo na taka imeongeza mavuno kwa asilimia 30 hasa katika uzalishaji wa nyanya zenye ubora.

"Mradi huu wa taka ulikuwa ni wa majaribio na tulikuwa tunazihifadhi takataka zinazotumika katika shehia ya Kiembe Samaki na kufanikiwa kuzitengeneza kuwa mbolea ambayo iliwanufaisha wakulima wa vijiji vya Dimani, Shakani, Mwera na Kibele," alisema.

Aidha, alieleza kuwa iwapo taka zinazozalishwa zitatumika vizuri, wakulima wa Zanzibar wataondokana na tatizo la upungufu wa mbolea katika kuendeleza hasa kilimo cha mboga.

Alisema kuwa kitendo kinachofanywa na baadhi ya wakulima cha kuweka taka katika mashamba yao kama mbolea bila ya kusarifiwa kitaalamu kunaweza kukasababisha madhara mbalimbali kwa binadamu.

Alisema kuwa kitendo hicho kinaweza kikaathiri mazingira kwa kuwa baadhi ya taka huwa na sumu, hivyo sumu hiyo kuiweka katika mimea kunaweza kukasababisha madhara makubwa.

Mtaalamu huyo alishauri kuwa ni vyema kuwa na wataalamu watakaoweza kusarifu taka na kuwa mbolea ambapo hatua hiyo itaongeza kasi ya udhalishaji wa mazao na kupunguza kuagiza mazao kutoka nje ya Zanzibar.

# Ukosefu wa masoko 'pasua kichwa' Tumbatu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

FAMILIA zilizomo katika mradi wa malezi mbadala ya watoto katika Kisiwa cha Tumbatu Kaskazini Unguja zimesema kuwa kukosekana kwa soko la uhakika kwa ajili ya bidhaa zao imekuwa ni kikwazo katika kuendeleza biashara zao.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mzazi wa watoto waliomo katika mradi huo, Rahma Ali Khamis, alisema kuwa bidhaa wanazozalisha zimekuwa zikikosa soko la uhakika hali ambayo imekuwa ikisababisha hali zao za kiuchumi kusuasua kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya kuhudumia familia.

Aliwapongeza waanzilishi wa mradi huo ambao ni Kijiji cha Kulelea Watoto Yatima na Wanaoishi katika Mazingira Magumu (SOS) kwa kuwawezesha kuwapatia mtaji kwa ajili ya kufanya biashara ndogondogo na kuweza kuhudumia familia.

Alisema kutokana na jiografia ya kisiwa cha Tumbatu hakuna mwingiliano wa watu kutoka maeneo mbalimbali, hivyo biashara wanazofanya inabidi wauziane wenyewe kwa wenyewe.

"Mimi nauza biashara ya vyakula, lakini soko siyo zuri maana wakati mwingine biashara yangu huwa hainunuliwi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali za wananchi wa kisiwa hiki ni maskini hawana fedha," alisema.

Aidha, alisema licha ya kukabiliwa na changamoto hiyo, lakini anaupongeza mradi huo kwa kuwa umemwezesha kuwaendeleza watoto kielimu pamoja na kujengewa nyumba kwa ajili ya mkaazi.

Alieleza kuwa kabla ya mradi huo alikuwa anamzigo mkubwa wa malezi wa watoto watano ambao baba yao amewatelekeza.

Naye Sheha wa Tumbatu, Jongowe Miza Ali Sharif, alizitaka familia za watoto waliomo katika mradi huo na wale ambao hawamo kuhakikisha wanawapatia malezi bora watoto wao kutokana na uwezo walionao.

Alisema miongoni mwa malezi hayo ni kuhakikisha watoto wanapatiwa haki zao ikiwamo haki ya kupata elimu ambayo ndio itakayoweza kuwasaidia katika maisha yao.

Sheha huyo alikemea kitendo cha watoto kuonekana baharini wakifanya shughuli za biashara wakati wa masomo kwa kuwa kinaweza kumwathiri mtoto.

"Mtoto anahitaji kupatiwa elimu na sio kupewa biashara kwa kuwa wakati wa kufanya hivyo bado haujafika, kwanza tuwape elimu watoto wetu," alisema.

# Viongozi watakiwa kusimamia sheria

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka viongozi wa ngazi mbalimbali wa chama na serikali mkoani humo, kuzingatia sheria ili kustawisha hali ya amani, utulivu na ustawi bora wa jamii. Aliyasema hayo katika ziara ya kikazi aliyoifanya katika Shehia za Fuoni Mnarani na Kijitoupele kufuatia kuwapo kwa malalamiko ya muda mrefu ya wananchi wa maeneo hayo kuhusu vitendo vya uhalifu na ukiukaji wa maadili vinavyofanywa na baadhi ya wananchi bila ya kuchukuliwa hatua stahiki.

Alisema ili amani na utulivu istawi katika nchi kuna haja ya kuimarisha ustawi wa jamii kwa kudhibiti vyanzo vya migogoro inayojitokeza ndani ya jamii badala ya kusubiri vyombo vya ulinzi na usalama.

Alieleza kuwa viongozi wa serikali na kisiasa kwa pamoja wanapaswa kusimamia sheria na kuwaeleleza wananchi juu ya umuhimu wa jambo hilo badala ya kuwakingia kifua pindi vyombo vya sheria au viongozi wenye dhamana wanapochukua hatua.

Akielezea nia ya ziara hiyo, Ayoub alisema ililenga kujiridhisha kabla ya kuchukua hatua juu ya malalamiko ya wananchi wa Shehia ya Mnarani ambao kwa muda mrefu wamelalamikia uwepo wa klabu ya pombe za kienyeji jirani na makazi yao.

Katika Shehia ya Kijitoupele, Mkuu huyo wa Mkoa alisema ziara inalenga kusikiliza malalamiko ya mkazi, pamoja eneo hilo anayedaiwa kuwa na tabia ya matusi, utapeli na unyang'anyi wa mali za watu. Akielezea uamuzi kuhusu mkazi huyo, Ayoub alieleza kuwa baada ya kubaini amekuwa na tabia ya kunyang'anya mali za wanaume anapoachana nao kwa vigezo vya kuchuma nao na kudanganya ofisi za mkuu wa wilaya, aliagiza ahamishwe. Katika ziara hiyo pia kiongozi huyo alikamata zaidi ya pikipiki tano zinazotumika kusafirishia abiria katika eneo la Melitano Msikitini na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kusimamia uamuzi wake wa kupiga marufuku hadi sheria itakaporuhusu zifanye biashara hiyo.

## Basi la shule latekwa, lateketezwa

**ROMA,** Italia

BASI lililokuwa limebeba watoto wa shule ya Vailati di Crema wapatao 51 lilitekwa na kuchomwa moto karibu na mji wa Milan nchini Italia.

Watoto hao wa shule baadhi yao walifungwa kamba, waliokolewa baada ya kuvunjwa vioo vya basi hilo upande wa nyuma na hakuna hata mmoja aliyejeruhiwa.

Watu 14 waliathiriwa na moshi uliotokana na kuteketea kwa basi hilo.

Dereva wa basi hilo mwenye umri wa miaka 47 raia wa Italia mwenye asili ya Senegal, alikamatwa na Jeshi la Polisi kwa uchunguzi zaidi.

Kisa cha kukamatwa kwa dereva huyo ni baada ya kusikika akiwaambia waliokuwamo katika basi hilo kwamba hakuna hata mtu mmoja atakaye nusurika. Mwalimu mmoja wa shule hiyo alikuwa ndani ya basi wakati tukio hilo likitokea, alimwelezea mtuhumiwa huyo kuwa alikuwa na hasira mara kwa mara.

Taarifa zingine zinaarifu kuwa dereva huyo alisikika akibwatuka akisema "sitisheni mauaji katika Bahari ya Mediterranean".

Mashuhuda wa tukio hilo walieleza kuwa makundi mawili ya wanafunzi waliokuwa wakisindikizwa na walimu wao wakielekea kwenye mazoezi, lakini baadaye ghafla gari lao lilibadili uwelekeo na kuelekea kwenye barabara kuu ya mkoa, halafu likaelekea barabara ya uwanja wa ndege wa Milan Linate **BBC**

## New Zealand yapiga marufuku mauzo ya silaha

**WELLINGTON,** New Zealand

NEW Zealand imepiga marufuku mauzo ya bunduki za kivita kama ile iliyotumiwa na mshambuliaji aliyeua watu 50 katika misikiti miwili nchini humo Ijumaa iliyopita.

Mbali na hilo pia imewataka watu wote wanaomiliki bunduki za aina hiyo kuzirejesha haraka.

Tangazo hilo lililotolewa na Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Jacinda Ardern, limekuja siku sita baada ya kutokea shambulizi katika misikiti miwili mjini Christchurch.

Awali Ardern aliliita shambulizi hilo kuwa la kigaidi na kuahidi kuwa sheria za New Zealand zingebadilishwa ili kuzuia upatikanaji kirahisi wa silaha zinazoweza kuua watu wengi.

"Tarehe 15 Machi, historia yetu ilibadilika milele na sasa sheria zetu zitabadilika pia. Leo hii tunatangaza hatua kwa niaba ya wa-New Zealand wote, kuimarisha sheria za umilikaji wa bunduki, ili nchi yetu iwe mahali salama zaidi," alisema Arden.

Waziri Mkuu huyo alisema ifikapo Machi 11, mwaka huu, anatarajia sheria nyingine itapitishwa ili kuweka mpango wa wale ambao tayari wanazimiliki silaha zilizopigwa marufuku kuzirejesha serikalini na kupatiwa fidia. **DW**

# Serikali ya Congo yakiri maofisa wake kuuawa

**KINSHASA,** Congo

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo imekiri kwa mara ya kwanza kwamba maofisa wa serikali walitumika katika mauaji ya mamia ya watu Desemba mwaka jana.

Takribani watu 535 waliuawa katika vijiji vitatu vya Yumbi, eneo la mashambani magharibi mwa nchi hiyo, ukingoni mwa Mto Congo umbali wa kilomita 350 Kaskazini mwa Kinshasa.

Mauaji hayo ambayo ni ya kikabila yalifanyika kwa siri kubwa kwa sababu yaliendeshwa siku kadhaa kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu wa urais.

Waziri wa Mashirika ya Haki za Binadamu Congo, Marie-Ange Mushobekwa, akizungumza katika mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa (UN) kufuatia kuchapishwa kwa ripoti ya UN, alisema siku zilizopita habari zilianza kuzagaa na ilichukua takribani muda wa mwezi mmoja kabla ya kiwango cha mauaji hayo kubainika.

**Tunataka kujua kwa nini walifanya hivyo, hatujui walitaka kuzuia uchaguzi ama sijui kwa malengo yapi. Kwa sasa tunasubiri ripoti ya makundi ya haki za kibinadamu juu ya mauaji hayo.**

"Kile kilichotokea katika eneo la Yumbi Desemba sio kitu cha fahari kwa taifa langu," alisema Mushobekwa ambaye kwa sasa yuko mjini Geneva.

Alisema wanasiasa na maofisa wa utawala walihusika katika mauaji hayo na kusababisha hali mbaya. Aidha, mauaji hayo yalihusisha kukatwa mapanga kwa wanawake wajawazito pamoja na kunyofolewa sehemu zao za siri.

Taarifa ya Mushobekwa inajili wakati wanaharakati wa haki za binadamu nchini humo wakishinikiza kuwasilishwa mahakamani kwa watuhumiwa wa mauaji hayo haraka iwezekanavyo.

Mwanaharakati wa haki za kibinadamu, Jean Claude Katende, alisema kuwa mashirika hayo yanataka kujua ni kina nani waliohusika kupanga mauaji hayo upande wa serikali pamoja na upande wa raia.

"Tunataka kujua kwa nini walifanya hivyo, hatujui walitaka kuzuia uchaguzi ama sijui kwa malengo yapi. Kwa sasa tunasubiri ripoti ya makundi ya haki za kibinadamu juu ya mauaji hayo," alisema Katende.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa mauaji hayo yalikuwa yamepangwa kwa siri na watu wa jamii ya Batende dhidi ya watu wa Banunu.

Shambulio hilo lilitekelezwa kwa mbinu za kijeshi, huku washambuliaji wakionekana kuvaa magwanda ya kijeshi.

Baada ya kutokea kwa tukio hilo, serikali iliwabadilisha maofisa waliokuwapo ikiwamo wa polisi na wakuu wa ujasusi, wanajeshi na wa serikali. Shambulio hilo linaweza kuorodheshwa miongoni mwa mashtaka ya uhalifu wa kivita. **BBC**



Mji wa Maputo nchini Msumbiji unavyoonekana kwa sasa baada ya kukumbwa na kimbunga Idai kilichosababisha mafuriko. **PICHA: REUTERS**

# Mvua zatatiza shughuli za uokoaji

**MAPUTO,** Msumbiji

MVUA zinazoendelea kunyesha nchini Msumbiji zimezuia shughuli za uokoaji kwa watu walioathirika na kimbunga Idai ambacho hadi sasa kimeua watu zaidi ya 200 nchini humo na watu 100 Zimbabwe.

Maelfu ya watu bado hawajafikiwa na misaada katika maeneo yao kutokana na mafuriko yanayoukumba mkoa huo.

Katika Mji wa Beira ulioathirika zaidi, bado kuna watu ambao wamekwama juu ya paa za nyumba na ambao wanahitaji kuokolewa.

Wakati huo huo, maelfu ya watu wamekwama na wanahitaji msaada wa kuondolewa katika baadhi ya maeneo yanayokumbwa na mafuriko kwa sasa.

Mashirika ya kihisani na watu wanaojitolea wanaendelea na shughuli ya uokoaji licha ya kuwa na ugumu katika zoezi hilo.

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya masuala ya kibinadamu imeonya kwamba kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, hali hiyo inaweza kuwa mbaya zaidi.

Gavana wa Mkoa wa Sofala, Alberto Mondlane, alithibitisha kutokea kwa hali mbaya endapo hakutakuwapo na msaada wowote wakati mvua hizo zikiendelea kunyesha.

"Mafuriko yanaendelea wakati kuna watu wengi ambao wamekimbilia juu ya miti au juu ya mapaa ya nyumba wakisubiri msaada," alisema Mondlane.

Shughuli za uokoaji na ugawaji wa misaada kwa waathirika wa kimbunga hicho zinatatizwa kutokana na uharibifu wa barabara pamoja na mawasiliano yaliyoharibiwa na kimbunga hicho.

UN imetoa wito kwa mataifa wanachama kujitokeza kufadhili operesheni ya misaada baada ya kimbuka hicho kilichotokea katika mataifa ya Msumbiji, Zimbabwe na Malawi. **RFI**

# TPA yapiga jeki elimu

**Na Abdallah Bakari,** MTWARA

MAMLAKA ya Bandari Tanzania (TPA), imejitosa kuinua hali ya elimu mkoani Mtwara kwa kusaidia kuboresha hali ya miundombinu shuleni kwa kuchangia madawati 76 na mabati 1,852 vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 65.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Profesa Ignas Rubaratuka, alisema msaada huo ni sehemu ya sera ya Mamlaka ya Bandari katika kusaidia sekta ya elimu ambayo ndio kipaumbele cha mamlaka hiyo.

Alisema kuwa aliamua kutoa msaada huo baada ya kupata taarifa ya uwapo wa upungufu wa vyumba 48 vya maradasa katika Mkoa wa Mtwara na hivyo kuathiri mwenendo wa masomo kwa wanafunzi.

"Vifaa hivyo vinalenga kusaidia madarasa 37 kati ya 48 katika ya shule 15 zilizokuwa na changamoto ya ukosefu wa mabati na madawati ili wanafunzi katika shule hizo waendelee na masomo katika mazingira bora," alisema.

Vifaa vilivyokabidhiwa jana mkoani hapo na kupokelewa na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Evod Mmanda, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mtwara ni mabati 1,852 na madawati 76.

Mmanda aliishukuru Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa msaada huo na kuahidi kuutumia kama ulivyokusudiwa.

"Msaada wa madawati umepelekwa kwenye Shule ya Msingi Naliendele pekee, haya mabati tutagawanya kwenye halmashauri sita za Mkoa wa Mtwara ili kila mmoja anufaike na msaada huu," alisema Mmanda.

"Manispaa ya Mtwara Mikindani itapata mabati 100, Nanyamba mjini (300), Tandahimba (300), Newala (450), Nanyumbu (400) na Masasi (300)," alifafanua Mmanda.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mhandisi Deudedit Kakoko, alisema mamlaka yake itaendelea kutoa misaada ya aina hiyo hasa kwenye sekta zenye uhitaji zaidi wa elimu na afya, lengo ikiwa ni kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano.

"Tutaendelea kuisaida serikali kutatua changamoto mbalimbali hasa katika sekta ya elimu na afya, tuligubswa na hali ya elimu na uduni wa miundombinu mkoani Mtwara, tukaona nasi tusaidie kutatua changamoto hizo," Kakoko alisema.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akipanda mti ikiwa leo ni Siku ya Maadhimisho ya Kupanda Miti Duniani, wakati alipotembelea katika Hifadhi ya Msitu wa Biharamulo upande wa Wilaya ya Chato mkoani Geita. **PICHA: WMU**

# Wataka mabadiliko sheria upimaji ardhi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAPIMAJI ardhi nchini wameiomba serikali kupitia na kubadilisha sheria za upimaji ardhi zilizopo ili kuendana na wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Upimaji Ardhi ya Cosmo-maps Consult Company Ltd, Simon Chuwa, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya Siku ya Upimaji Ardhi Duniani iliyofanyika kitaifa jijini hapa.

Chuwa aliiomba serikali kubadili sheria za upimaji ardhi zilizopo nchini ili kutunga mpya zitakazoendana na wakati uliopo.

"Sheria za ardhi zipo kweli, lakini zimepitwa na wakati. Tunaiomba serikali kuzipitia upya sheria hizi ili ziweze kwendana na wakati," alisema.

Alizitaja sheria hizo zinazoongoza na kuratibu shughuli za upimaji ardhi sura namba 324 na Sheria ya Usajili Wapimaji Ardhi Sura ya 270 ya Mwaka 1977.

Kwa mujibu wa Chuwa, kukua kwa teknolojia ya vifaa vya upimaji ramani na uchakataji wa taarifa za kijiografia kumewezesha mabadiliko kadhaa kufanyika katika fani ya upimaji ramani, hivyo hata sheria zinatakiwa kubadilika.

Aliitaja changamoto nyingine ni kuwa kukosekana kwa bodi ya upimaji ardhi jambo ambalo linawanyima baadhi ya mambo mengi kuhusu fani hiyo kushindwa kupitishwa.

Chuwa alisema katika maadhimisho hayo, wapima ardhi wamefanya maonyesho ya kazi zao katika eneo la Nyerere Square jijini hapo na mkoani Dar es Salaam viwanja vya Mlimani City ili kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kazi zinazofanywa na taaluma hiyo.

Pia alizitaja kazi zinazofanywa na wapimaji ardhi kuwa ni kufanya upimaji juu ya ardhi, chini ya ardhi, baharini, mito na kwenye maziwa na wanaweza kuzifanya kwa kushirikiana na wanataaluma wa fani zingine.


JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

115131902

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe 22-03-2019 kampuni ya **AB GILMANS CONTROLLED LOGISTICS LTD.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa .
2. Kutoka Dar es Salaam kuelekea TUNDUMA kupitia VIGWAZA , gari hilo lenye namba za usajili: **T 237 DFS / T 927 DFS**
3. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **20.00** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.00** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu(Kuanzia saa 12;30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Miili ya watu wawili waliofukiwa na kifusi yapatikana Nyangalata

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

TAKRIBANI siku 60 tangu kuanza kwa utafutaji wa watu watatu waliofunikwa na kifusi katika machimbo ya dhahabu Nyangalata yaliyoko wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, maiti mbili zimepatikana.

Kiongozi msaidizi wa uokoaji, Amos Mbaga, alitoa taarifa hiyo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Chama cha Wachimba madini Mkoa wa Shinyanga, Hamza Tandiko, wakati akizungumza na waandishi wa habari waliofika katika eneo la tukio kujionea maendeleo ya uokoaji.

Amos alisema watu hao wawili kati ya watatu walikuwa wamefukiwa na kifusi cha udongo tangu Januari 21, mwaka huu.

Mbaga alisema kuwatoa watu watatu waliomo ndani ya duara kumeshindwa kukamilika kwa wakati kutokana na magogo yaliyokuwa yanatumika kutengeneza mfumo wa uokoaji kukatika baada ya kuzidiwa na udongo na kulazimu kuanza upya matengenezo, jambo ambalo limefikia asilimia 50 mpaka sasa.

"Tulikuwa tumetegemea ndani ya siku saba zoezi liwe limekwisha, lakini kutokana na changamoto iliyojitokeza miti iliyokuwa inatumika haikuweza kuhimili udongo ilikatika, kwa hiyo ikatulazimu kutafuta magogo makubwa zaidi na tukaanza zoezi upya juzi usiku kwenda juu, target (lengo) yetu mpaka jioni ya leo (jana) tutakuwa tumefikia asilimia 50 katika zoezi hili," alisema.

Aidha, Kamanda Abwao alisema walioopolewa wakiwa wamekwishafariki dunia ni Shida Charles, Sebastian Mboje na Hamis Yusuph, huku Masunga Ngewe wakiendelea kumtafuta.

Kamanda Abwao alifafanua kuwa zoezi la kuitambua miili hiyo kwa ndugu zao ilikamilika na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja vinauzwa chanika mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika umeme upo bei kuanzia 2m vimebaki vichache. Mawasiliano: 0714-187555 au 0755-288879

### NAFASI ZA KAZI


**NAFASI ZA KAZI UALIMU / CERTIFICATE** au diploma / english/mathematics na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



### CHETI KIMEPOTEA



**BARAKA Y. KIBALE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1050/0106** kilichotolewa na Shule ya Sekondari ARAGE mwaka 2004. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWJ/RB/114/2019.**

115130002

### KUPOTEA KWA CHETI



**ARAPHAT R. MBWANA** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Enyoito chenye **Index No SC 16000160270** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2016. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **MOS/RB/1732/19.**

115132302

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**ORKEESWA SEKONDARY** SCHOOL ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE **NO T628 DKB,** ENGINE NO **1KB1793856,** CHASSIS NO **KDH2068006606**

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU.

MON/RB/1852/019.

115132702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Ijumaa tarehe **22-03-2019** kampuni ya **MAWAZO KHALID.** Itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa.

   1. **Kutoka DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA, kupitia VIGWAZA** gari hilo lenye namba za usajili:

   **AIB 6060ZM / AIB 6059ZM**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | **- mita** | **20.00** |
| **Upana** | **- mita** | **3.00** |
| **Kimo** | **- mita** | **5.20** |

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115132002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILAINO.**

Simu: +255 262324455.
Fax: +255 26232233.
Barua Pepe ps@mo.go.tz.
Tovuti: www:mwtc.go.tz.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAPILI tarehe 24/03/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka BOMANG'OMBE kuelekea DAR-ES-SALAAM gari hilo lenye No za usajili: **T891 ANR, T748 BBW, T567 CZX, T750 CUU**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   **Urefu - mita 24, Upana - mita 3.7 Kimo - mita 4.6**
3. Njia itakayotumika **BAGAMOYO hadi DAR** kupitia BAGAMOYO gari litasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni).***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitikeza.***

115132902

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 24-03-2019 kampuni ya ME &CO. itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Mlandizi kuelekea Dar es Salaam, gari hilo zenye namba za usajili:
   **T 232 AGE / T 261 AWR**
2. Garihilolinavipimovifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **4.80** |

3. Njia itakayotumika :**Mlandizi hadi Dar es Salaam kupitia M/Road,** Gari itasafiri muda wa mchana tu***(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115131602

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**MARUMBU TRADING COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 560 DPM SCANIA.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/03745/2019.**

115131402

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**SAID SIMON KIHWELLE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 525 AUX TOYOTA LANDCRUISER.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **CID/TR/RB/03747/2019.**

115131502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

Simu Namba: +255(0)28 250 1044
Simu Namba: +255(0)28 250 1045
Fax Na: 028-2500117
Unapojibu tafadhali taja:
Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Hakimu Makazi Mfawidhi
Mahakama ya Mwanzo Mjini
S.L.P 155
MWANZA

Kumb. Na. MADAI 81/2019

**YAH: SHAURI LA MADI NA 81/2019**

**MDAI........................ PUNUNTA'S COMPANY LTD**

**DHIDI YA**

**MDAIWA ..................................PILLY .M. KOMBO**

**Unaamriwa na Mahakama ya mwanzo mjini Mwanza kufika tarrehe 28/03/2019 saa 2:00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai tajwa hapo juu endapo hutafika mahakamani shauri litasikilizw na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.**

**F.K. Kubingwa**
**KNY: HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MWANZA**

215130902

---

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
21/03/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe 24-03-2019 kampuni ya M.M Corp. Ltd itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka Kiranjeranje kuelekea Dar es Salaam, gari hilo zenye namba za usajili:
   **T 898 APY HORSES / T 933 AFZ**
2. Garihilolinavipimovifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **22.00** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **4.80** |

3. Njia itakayotumika :**Kiranjeranje hadi Dar es Salaam** kupitia Kilwa road, Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115130802

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KIDY ABDUL MKAPUNDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **COROLA** yenye namba za usajili **T.590 BHN.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**SHY/RB/TR/157.**

215129002

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**KAHAMA OIL MILLS LTD** inatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya TATA yenye namba za usajili **T 864 DBU** Chassis no. MAT426035D7R25386, Engine no. 31H84123714

Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.

Taarifa ya polisi:
**KAH/TR/RB/212/2019**

115132502

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**KAHAMA OIL MILLS LTD** inatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya TATA yenye namba za usajili T676 DBV Chassis no. **MAT426035E7R07657,** Engine no. **41D84159115**

Yeyote atakayeiona a toe taarifa polisi.

Taarifa ya polisi:
**KAH/TR/RB/211/2019**

115132502

### TEGEMEZA FINANCE AND COURT BROKER

### NOTISI / MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **Prosher Capital Limited (Ltd)** Makao Makuu Dsm tunatoa notisi na taarifa ya mnada baada ya siku (7) toka tangazo litoke. Kwa taarifa hii tutalazimika kuuza mali zilizowekwa kama dhamana ili kufidia deni lote na gharama zingine za mnada. Gari zifuatazo zitauzwa: **Nissan Navara T 679 DET; Toyota Alphard T 638 DEX.** Siku ya tarehe 29/3/2019 saa 4:00 asubuhi. Mahali: Mikocheni/Mtaa Migombani/Ofisi za mikopo Prosher Capital Ltd.

**Mawasiliano:**
**0762 443118 / 0719 187677.**

115129802

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**KAHAMA OIL MILLS LTD** inatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya TATA yenye namba za usajili **T 678 DBV** Chassis no.**MAT426035E7RO7,** Engine no. **41D84158039**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi.

Taarifa ya polisi:
**KAH/TR/RB/213/2019**

115132502


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

***Tupigie 0767 223 311***



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# 'STEARLING HAPATI HESHIMA ANAYOSTAHILI'

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United na timu ya taifa ya Ufaransa, Paul Pogba, anaamini Raheem Sterling hapewi heshima anayostahili kwa kiwango chake na kile anachokifanya uwanjani akiitumikia timu yake ya Manchester City.

Sterling tayari amefunga mabao 21 katika mashindano yote msimu huu kwa kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola.

Winga huyo amefunga magoli 15 na kutoa msaada wa magoli tisa katika Ligi Kuu ya England, huku Sterling akijiimarisha kama mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye Ligi hiyo.

"Nadhani Raheem Sterling, kwa takwimu zote za mwaka jana na kila kitu alichofanya - hakuna mtu anayesema kuhusu hilo kama tunapaswa," amesema Pogba akiiambia Sky Sports.

"Labda kama angekuwa mtu mwingine, ingekuwa tofauti."

Sterling alishutumu vyombo vya habari kwa kuchochea ubaguzi wa rangi mapema msimu huu baada ya kutupiwa maneno machafu katika mechi dhidi ya Chelsea Desemba mwaka huu.

England leo Ijumaa itakabiliana na Jamhuri ya Czech kabla ya kuivaa Montenegro Jumatatu kwenye mchezo wa kufuzu kwa Euro 2020, wakati Ufaransa ya Pogba itachuana na Moldova na Iceland.

# City kumpa miezi 12 Kompany

**MANCHESTER,** England

BEKI wa Manchester City, Vincent Kompany, anapanga kusaini mkataba mpya wa muda mfupi ili kuendelea kubakia hapo kwenye uwanja wa Etihad kwa mwaka mmoja zaidi.

Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, unamalizika mwishoni mwa msimu huu, huku wengi wakiwa na wasiwasi juu ya ufiti wake kutokana na majeraha ya mara kwa mara.

Hata hivyo, City wanatarajia kupuuzia majeraha hayo na kumwongeza mkataba kama ambavyo gazeti la Evening Standard limeripoti. Kompany anatarajiwa kusaini mkataba mpya wa miezi 12 na kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola.

Ripoti zaidi zinasema kwamba, Guardiola anaamini kwamba, uwepo wa Kompany kwenye vyumba vya kubadilishia nguo kunaleta hamasa kubwa kwa wachezaji na hivyo ni muhimu mchezaji huyo akaendelea kuwapo.

Hajapewa nafasi ya kucheza kwa muda mrefu, huku Guardiola akiwatumia zaidi Aymeric Laporte na John Stones, lakini City yenyewe inaamini kwamba Kompany bado anaweza kuleta chachu ndani ya klabu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 anaweza kujikuta katika wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza msimu ujao kwa kuwa Guardiola amebainisha kuwa anataka kutafuta beki wa kati wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa kipindi cha miaka minne, Kompany amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara na kujikuta akicheza jumla ya mechi 108 tangu mwaka 2015.

Msimu huu, Kompany ameanza kwenye mechi 11, lakini bado ameweza kuonyesha kiwango cha kuridhisha.



# Man City yajipanga kumsajili Niguez

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Manchester City inajipanga kushinda mbio za kuwania kumsajili kiungo Atletico Madrid, Saul Niguez, kwa euro milioni 80 dhidi ya Barcelona.

City inapanga kusajili kiungo wa muda mrefu kwa ajili ya kuziba pengo la Fernandinho baada ya kushindwa kupata saini ya Frenkie de Jong kutoka kule Ajax, ambapo kiungo huyo wa Uholanzi akiwa tayari amekubali kujiunga na Barcelona.

Na sasa Man City wamejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi kumsajili kiungo huyo wa kimataifa Hispania na kuwashinda Barça.

Pep Guardiola amebainisha wazi kwamba Saul mwenye umri wa miaka 24 anatakiwa kutua hapo ili kuimarisha nafasi ya kiungo.

Wawakilishi wa Saul wamekuwa wakiwasiliana na Barcelona na Manchester City na walinukuliwa na ESPN wakisema: "Hawezi kuendelea kubakia na Atletico, mambo hayapo sawa pale."

Ripoti zinadai kwamba Atletico imepanga kiasi cha euro milioni 120 kwa ajili ya kumwachia kiungo, lakini inaamini kuwa wapo tayari kupokea euro milioni 80.



# Alexander Arnold aondolewa kikosi cha England

**LONDON,** England

BEKI wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold, ameondolewa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England kuelekea mchezo wa ufunguzi wa michuano ya kufuzu kwa Euro 2020, baada ya kuumia mgongo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 aliumia wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Burnley mapema mwezi huu, lakini aliripotiwa kwamba angekuwa fiti kujiunga na kikosi hicho cha Simba Watatu.

Beki huyo wa kulia ameanza msimu huu wa 2018/19 kwa kuwa na majeruhi ya mara kwa mara na kujikuta akikosa mechi kadhaa mwanzoni mwa mwaka huu baada ya kuumia goti.

Chama cha soka cha England kimethibitisha kupitia ukurasa wake wa Twitter, kwamba mchezaji huyo hatakuwapo kwenye mchezo wowote kati ya michezo miwili ya kikosi hicho.

England inayonolewa na kocha, Gareth Southgate, itacheza na Jamhuri ya Czech leo Ijumaa kwenye uwanja wa Wembley, kabla ya kuwafuata Montenegro Jumatatu.

Huku tayari kikosi hicho kikiwa na mabeki wengi wa kulia, Kieran Trippier na Kyle Walker, Southgate pengine hataweza kuita mchezaji mwingine wa kuziba pengo lake.

Hata hivyo, vyombo vya habari vya England vimebainisha kwamba kuna uwezekano wa beki wa Crystal Palace, Aaron Wan Bissaka anaweza kuitwa kuziba pengo hilo baada ya kuwa na kiwango bora katika klabu yake chini ya kocha, Roy Hodgson.






# POGBA: KUCHEZA REAL NI NDOTO YA KILA MCHEZAJI

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, amebainisha kwamba kuichezea Real Madrid inaweza kuwa ndoto ya kila mwanasoka na hasa kuwa chini ya kocha Zinedine Zidane hapo kwenye dimba la Bernabeu, ingawa amesisitiza kuwa ana furaha kubakia Old Trafford.

Pogba hakusema kama anataka kuondoka United, au kujiunga na Real, lakini alitoa kauli yake hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari akiwa na timu ya taifa ya Ufaransa inaweza kutoa tafsiri tofauti kwamba, hana maisha marefu pale Manchester.

"Kama ambavyo nimekuwa nikisema, kuichezea Real Madrid ni ndoto ya kila mmoja. Ni moja ya klabu kubwa kabisa duniani," amesema mshindi huyo wa kombe la Dunia akinukuliwa na Sky Sports.

"Pia kuna Zidane pale kama kocha na ni ndoto ya kila mmoja kucheza kama anapenda kweli soka."

Pogba, ambaye alikuwa anawaniwa na Real kabla ya kurudi England mwaka 2016, hivi karibuni alibainisha kwamba hana mpango wa kuondoka kwa klabu yake hiyo ya sasa.

"Kwa sasa, nipo hapa Manchester. Hatutaki kuzungumzia uvumi wa majaliwa ya baadaye. Nipo hapa Manchester na nina furaha kuwa hapa," aliongeza.

# *Man U yajiamini kumsajili Sancho*

**MANCHESTER,** England

INAAMINIKA kwamba Manchester United inajiamini zaidi kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, kipindi cha majira ya joto, huku akitajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 80.

Nyota huyo wa kimataifa wa England anatabiriwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa baadaye barani Ulaya, na amekuwa na mafanikio makubwa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, msimu huu, akifunga mabao 13 na kutoa pasi tisa za mwisho kwenye mashindano yote.

Sancho alijiunga na klabu hiyo akitokea Manchester City mwaka 2017, akitua kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 8.

Kwa mujibu wa gazeti la Evening Standard, United wanajiandaa kumsajili mchezaji huyo wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinasema kwamba, Dortmund imezipuuzia taarifa hizo na kwamba wamebainisha kuwa hawatakuwa tayari kumuachia mchezaji huyo.

Zaidi ni kwamba Manchester City nao wapo kwenye mipango ya kutaka kurudisha mchezaji huyo.






# WILLIAN NJIA PANDA CHELSEA

## ●●● Adai yupo tayari kuongeza mkataba mpya, lakini hana uhakika klabu kama...

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Willian amesema anataka kuongeza mkataba wa kuendelea kuichezea timu hiyo, lakini hana uhakika kama klabu hiyo bado inamuhitaji na itamwongezea mkataba mpya.

Nyota huyo wa kimataifa bado amebakisha mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia klabu hiyo aliousaini mwaka 2013 akitokea klabu ya Urusi ya Anzhi Makhachkala.

"Nimebakisha mwaka mmoja, lakini nataka kuendelea kucheza kwenye klabu hii," Willian alinukuliwa na gazeti la Evening Standard.

**"Sina uhakika kama wanitaka, lakini niseme ukweli nataka kuendelea kubaki hapa," aliongeza kusema Willian.**

Willian ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu na kombe moja la FA kwa miaka sita aliyokaa Chelsea.

"Klabu hii ni spesho kwangu, nimeshinda mataji na nina uhusiano mzuri na mashabiki wa timu hii, lakini nina uhusiano mzuri na wafanyakazi wa klabu," alisema Willian na kuongeza,

"Nijisikia vizuri kuwa hapa, nina furaha ninapocheza vizuri na kufunga mabao," alisema.

Willian anapambana kuisaidia Chelsea kurejea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kupitia kombe la Europa au kumaliza ndani ya nne bora kwenye Ligi Kuu England.

Kwa sasa Chelsea inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, ikiwa nyuma kwa pointi tatu dhidi ya timu inayoshika nafasi ya nne Arsenal.

## ZISIKUPITE

### MAN U YAMTAKA SANCHO

MANCHESTER United wanataka kumfuatilia winga wa England, Jadon Sancho, kwa ajili ya kumsajili kwenye dirisha lijalo hasa baada ya kubainika klabu yake ya Manchester City haijaweka kipengele chenye masharti ya kuzuia kumsajili klabu hiyo ya England baada ya kumuuza Ujerumani. ***(Evening Standard)***

### DORTMUND WATAJA DAU KUBWA

BORUSSIA Dortmund wataweka dau la pauni milioni 100 kama ada kwa nyota wake Sancho ambaye anawindwa na klabu mbalimbali Ulaya, timu hiyo ya Ujerumani imepanga kumgeukia winga wa Chelsea Callum Hudson-Odoi kama mbadala wa Sancho. ***(Mirror)***

### MAN CITY YAMTAKA NIGUEZ

MANCHESTER City inaongoza katika mbio za kutaka kumsajili kiungo wa Atletico Madrid Muhispania Saul Niguez mwenye miaka 24. ***(ESPN)***

### COUTINHO KUTIMKIA PSG

BARCELONA wapo tayari sasa kusikiliza ofa kwa ajili ya kiungo Philippe Coutinho, huku akihusishwa kutaka kutimkia PSG ya Ufaransa. ***(Goal)***

### MAN UNITED YAITIBULIA BARCA

BARCELONA wamepunguza kasi yao ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na timu ya taifa ya Ufaransa hasa baada ya Manchester United kuongeza kasi ya kumsajili mshambuliaji huyo mwenye miaka 27. ***(Mirror)***

### MORENO ANUKIA LAZIO

LAZIO wanakaribia kumpa mkataba wa awali wa makubaliano beki wa pembeni wa Liverpool, Alberto-Moreno raia wa Hispania ambaye amedumu Anfield kwa misimu mitano. ***(Independent)***

### BARCA OFA MEZANI KWA JOVIC

BARCELONA wanajiandaa kutuma ofa ya pauni milioni 43 kumsajili mshambuliaji Mserbia Luka Jovic na wanamatumaini kuanza makubaliano na klabu ya Eintracht Frankfurt ndani ya wiki chache zijazo. ***(Guardian)***

### AKANUSHA KUONGEZA MWAKA

BEKI wa kulia wa PSG, Dani Alves, amepuuza taarifa kuwa ameongeza mkataba wa mwaka mmoja wa kuendelea kuwachezea mabingwa hao wa Ufaransa. ***(Goal)***

### AWAFUNGULIA MLANGO MASTAA

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amewataka mshambuliaji raia wa Chile Alexis Sanchez, Muargentina Marcos Rojo na beki wa pembeni Antonio Valencia, kuondoka klabuni hapo kwenye dirisha lijalo la usajili. ***(Star)***

### KOVACIC AGOMA KUREJEA REAL

NYOTA anayecheza kwa mkopo kwenye klabu ya Chelsea, Mateo Kovacic, anajiandaa kujiunga na klabu nyingine ya Ligi Kuu England kuliko kurejea kwenye klabu yake ya Real Madrid. ***(Marca)***

### ARSENAL WAPATA UPINZANI

ARSENAL watakutana na upinzani kutoka kwa Bayern Munich katika mpango wao wa kutaka kumsajili winga wa Lille, Nicolas Pepe. ***(Bein Sports - via Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Arusha United yajitoa rasmi FDL

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KLABU ya Arusha United inayoshiriki Ligi Daraja kwanza Tanzania Bara, imetangaza kujiondoa rasmi kwenye ligi hiyo kwa kile walichodai vurugu za mara kwa mara pamoja na kukiukwa kwa kanuni za soka.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo, Otte Ndauka, alisema kuwa timu hiyo imeamua kujitoa rasmi katika mashindano hayo kutokana na vurugu wanazofanyiwa mara kwa mara viwanjani wakati wakicheza michezo yao.

Ndauka alisema kuwa timu yao imefanyiwa vurugu katika mechi mbalimbali ikiwamo mchezo nambari 69 wa ligi hiyo uliochezwa mjini Tabora Februari 2 mwaka huu, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja cha Ali Hassan Mwinyi.

"Mchezo huu tulifika siku moja kabla, kwa mujibu wa sheria tulitakiwa kufanya mazoezi kwa ajili ya mchezo husika, lakini jambo la kusikitisha sana na lisilo la kiungwana viongozi wa Rhino Rangers kwa kushirikiana na meneja wa uwanja walifanya kila jitihada kuhakikisha hatufanyi mazoezi.

"Pia katika mechi nyingine tulicheza na klabu ya Polisi pia tulifanyiwa vurugu kama hizo, sio timu tu au wachezaji wanafanyiwa vurugu hapana, pia waandishi wetu wanapigwa na hata kuna mmoja aliharibiwa vifaa vyake vya kazi," alisema Ndauka.

Alisema kuwa matukio yote ambayo yametokea wameiandika barua TFF kulalamika pamoja na Bodi ya Ligi, lakini hakuna uamuzi wowote wa kinidhamu ambao wameuchukua, hivyo ndio maana wameamua kujitoa katika ligi hiyo.

Kuhusiana na suala la mikataba ya wachezaji pamoja na mali za klabu hiyo, walisema kuwa bodi ya timu hiyo inakaa chini na wachezaji kujadili kuhusiana na mikataba hiyo, pia wanampango wa kuketi na bodi kujadili nini cha kufanya juu ya wachezaji wao.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2. Azam | 28 | 17 | 8 | 3 | 46 | 18 | 59 |
| 3. Simba | 21 | 17 | 3 | 1 | 45 | 7 | 54 |
| 4. Lipuli | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5. Kinondoni MC | 29 | 9 | 14 | 6 | 32 | 20 | 41 |
| 6. Mtibwa Sugar | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7. TZ Prisons | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8. Coastal Union | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9. Mbeya City | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10. Alliance | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11. Mwadui | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12. Kagera Sugar | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13. JKT Tanzania | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14. Mbao | 30 | 9 | 9 | 12 | 19 | 29 | 36 |
| 15. Stand Utd | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16. Ruvu Shooting | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17. Singida Utd | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18. Ndanda | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19. Biashara Utd | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20. African Lyon | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# KAGERE: HATUNA PRESHA KUWAVAA TP MAZEMBE



**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya Shirikisho la Soka Afrika 'CAF' kupanga droo ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, amesema hana hofu na timu waliyopangiwa nayo.

**Katika droo hiyo, Simba imepangwa kuumana na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambapo mchezo wa kwanza utachezwa hapa nchini kati ya Aprili 5 na 6 mwaka huu.**

Kagere, akizungumza na gazeti hili, alisema kama timu hawana hofu na mpinzani wao kwa kuwa kila mchezo ni kujipanga kuweza kupata ushindi.

Alisema anafahamu TP Mazembe ni moja ya timu kubwa Afrika, lakini pia Simba si timu ndogo na ndio sababu imefika hatua ya robo fainali.

"Tunajipanga kwa mchezo huo... hatua hii hakuna timu nyepesi na wala hakuna timu yenye uhakika wa kusonga mbele kabla ya dakika 90," alisema Kagere.

Alisema anafahamu kocha wao, Patrick Aussems ataandaa mbinu za kuwafikisha hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya vilabu Afrika.

"Ushindi tunaoupata kwenye michezo yetu unachangiwa pia na mashabiki wetu kwa hamasa kubwa wanayotupa...waendelee kutusapoti na kutupa hamasa kwenye hatua hii," aliongeza kusema.

Simba imetinga hatua hiyo baada ya kushika nafasi ya pili kwenye kundi lao, wakati hatua ya makundi ikichomoza nyuma ya Al Ahly ambao wamepangiwa kucheza na Mamelodi ya Afrika Kusini.



Wanachama wanawake wa Simba wakimsikiliza Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa timu hiyo, Asha Baraka (hayuko pichani) katika mkutano maalumu uliofanyika kwenye makao makuu ya klabu hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA : SOMOE NG'ITU**

# *Simba Queens, Yanga Princess zachapwa*

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Simba Queens imeendelea kuwa na wakati mgumu ugenini baada ya kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa wenyeji Alliance Girls katika mchezo wa raundi ya 14 wa Ligi Kuu wanaliocheza kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Kutokana na matokeo hayo Simba Queens inayonolewa na kiungo wa zamani wa Simba, Mussa Hassan "Mgosi" imebakia na pointi zake 28, wakati Alliance Girls wao wamefikisha pointi 29 na kupanda hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi unaoongozwa na JKT Queens yenye pointi 42.

Simba Queens, wao sasa wako katika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo inayochezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa juzi, Yanga Princess ilifungwa mabao 2-1 na wenyeji Tanzanite Queens kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Vinara na mabingwa watetezi wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12, JKT Queens wameendelea kutamba baada ya kuwachapa wenyeji Mapinduzi Queens katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Sabasaba mkoani Njombe.

Mabao ya JKT Queens katika mchezo huo yalifungwa na Asha Rashid aliyepachika magoli manne wakati Fatuma Mustapha akifunga mawili.

Mlandizi Queens wenyewe waliwafunga Kigoma Sisterz mabao 3-1 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, wakati Baobao Queens wakitoka sare ya bao 1-1 na Panama kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma, huku Marsh Queens wakipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Evergreen Queens.

Ligi hiyo ya wanawake inayodhaminiwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti itasimama kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) inayojiandaa na mchezo wake wa kuwania tiketi ya kucheza Michezo ya Olimpiki dhidi ya wenzao wa Jamhuri wa Kidemokrasia ya Kongo utakaochezwa Aprili 5, mwaka huu, jijini Dar es Salaam na kurudiana Aprili 9, huko Kinshasa.



Willian njia panda Chelsea

UKURASA. 30



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi (kushoto) na Jadon Sancho wakiwa katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa kuivaa Jamhuri ya Czech katika mchezo wa kuwania tiketi ya kucheza Fainali za Euro 2020 utakaochezwa leo. **PICHA: MTANDAO**

## Majaliwa kuiongoza Taifa Stars Jumapili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, atakuwa mgeni rasmi katika mechi ya kuwania tiketi ya kufuzu Fainali za Afrika kati ya wenyeji Timu ya Taifa (Taifa Stars) dhidi ya Uganda (Cranes) itakayochezwa keshokutwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars, Paul Makonda alisema kuwa wanaamini ujio wa kiongozi huyo utaongeza morali kwa wachezaji kwa ajili ya kusaka ushindi katika mchezo huo.

Makonda alisema kuwa kamati yake inawaomba wazalendo kujitokeza kushangilia katika mechi hiyo, ambayo Tanzania inajiandaa kuweka historia nyingine ya kufuzu fainali hizo baada ya kukosa kwa miaka 39.

Wakati huo huo, wasanii wa bongo flava, filamu, watangazaji na watu wengine mbalimbali maarufu akiwamo mrembo wa Tanzania wa mwaka 2006, Wema Sepetu wamewataka Watanzania kujitokeza kuishangilia Taifa Stars.

## Dante kuwakosa Alliance FA Cup

**Na Faustine Feliciane**

BEKI kisiki wa Yanga, Andrew Vincent 'Dante', ataukosa mchezo muhimu wa Kombe la FA dhidi ya Alliance FC utakaochezwa Machi 30, mwaka huu, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, imefahamika.

Dante ambaye anasumbuliwa na maumivu ya nyama za paja pia aliondolewa katika kikosi cha Timu ya Taifa 'Taifa Stars' na nafasi yake kuchukuliwa na Erasto Nyoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema kuwa katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika jana asubuhi wachezaji wote walikuwapo isipokuwa beki huyo.

"Mazoezi yanaendelea vizuri, tunashukuru hakuna majeruhi walioongozeka ukimuondoa Dante ambaye hatoweza kucheza mchezo dhidi ya Alliance," alisema Saleh.

# Aussems: Tutapambana

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Afunguka nyota wake wameimarika na kueleza hakuna timu ndogo robo fainali...

BAADA ya timu yake kupangwa na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa hakuna timu nyepesi kati ya klabu nane ambazo zimetinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa.

**Simba itawakaribisha mabingwa hao mara mbili wa Afrika, TP Mazembe kati ya Aprili 5 na 6 mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na kurudiana mjini Lubumbashi baada ya wiki moja.**

Aussems alisema kuwa alikuwa tayari kupangwa na timu yoyote katika hatua hiyo na kueleza kwamba kinachotakiwa kufanyika ni maandalizi bora kuelekea mchezo huo.

Mbelgiji huyo alisema kuwa bado anaipa nafasi timu yake kufanya vizuri kwenye mechi hizo mbili za hatua ya robo fainali kwa sababu watawakabili TP Mazembe wakiwa hawana wasiwasi wala hofu.

"Safari bado inaendelea, tutakwenda kama tulivyoanza, tulionekana hatuna nafasi, lakini tumefika hatua ya makundi, kikubwa bado tuko kwenye malengo yetu ya msimu huu, tunahitaji kuendelea kuipa ushirikiano timu kama tulivyoanza," alisema Aussems.

Aliongeza kuwa wachezaji wake wamepata uzoefu katika michezo 10 ya kimataifa waliyocheza, hivyo anaamini wataingia kuwakabili TP Mazembe wakiwa tofauti na walivyoanza michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika.

"Tulipambana na tutaendelea kupambana, kila timu inahitaji matokeo chanya kwa ajili ya kusonga mbele, kwa upande wangu hakuna timu nyepesi au ndogo, bado tuko kwenye mapambano na lolote linaweza kutokea, mwisho wa siku bingwa ni mmoja," alisema Aussems.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Haji Manara, alisema kuwa klabu yake iko tayari kuwavaa wapinzani wao nyumbani na ugenini.

"Silaha yetu kubwa ni kutokujali anayekuja mbele yetu, hatuna uoga hata kama tunajua wao wana rekodi nzuri kutuzidi, baada ya mechi ya Stars dhidi ya Uganda itakayochezwa Jumapili, nitakuja na kauli mbiu ya mechi hiyo na Wakongomani, sasa tujikite katika tui la Kiganda," alisema Manara.

Simba imetinga hatua ya makundi baada ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya AS Vita na kufikisha pointi tisa, huku Al Ahly ya Misri iliyomfunga JS Saoura ya Algeria magoli 3-0 ilifikisha pointi 10 na kuongoza Kundi D.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >